**CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA ZA KIAFRIKA**

# DHULUMA ZA KITABAKA KATIKA RIWAYA ZA *MKAMANDUME* NA *SHETANI MSALABANI*

**NA**

**KAUSI BARASA GEORGE**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**NOVEMBA, 2021**

# IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na wala haijapata kuwasilishwa kwa madhumuni ya shahada yoyote katika Chuo Kikuu kingine.

Sahihi…………………………… Tarehe 22/10/2021……………………………

Kausi Barasa George

(Mtahiniwa-C50/CE/26000/2014)

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi waliochaguliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Sahihi …………………………… Tarehe 25/10/2021……………………………

Prof. Kitula Kinge'i

(Msimamizi)

Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika.

Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Sahihi…………………………… Tarehe 03/11/2021……………………………

Bwana Japhet M. Mukobwa.

(Msimamizi)

Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika.

Chuo Kikuu cha Kenyatta.

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa babangu mzazi, Bw. Barasa Wanjala, mke wangu Laura Khavayi pamoja na wanangu wapendwa. Mungu awabariki na kuwapa maisha marefu kwa ushauri wenu na moyo wa uvumilivu.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa, ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, afya njema na kuniwezesha kukamilisha safari hii ya kupata shahada ya uzamili. Sifa na utukufu kwake.

Pili, ni kwa wasimamizi wangu Prof. Kitula King'ei na Bw. Japhet Mukobwa kwa juhudi na maarifa yao. Walinishauri na kunielekeza ipasavyo. Mola awazidishie hekima na maarifa zaidi.

Tatu, ni kwa wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa ushauri na maoni waliyonipa wakati wa utafiti. Hawa ni: Prof. Catherine Ndung'o, Prof. lreri Mbaabu, Dkt. Pamela Ngugi, Dkt Richard Wafula, Dkt. Miriam Osore, Dkt. Jacktone Onyango, Dkt. Timothy Arege, Dkt. Bonface Ngugi, Dkt. Leonard Chacha, Dkt. Titus Kaui, Dkt. Masinde na Bi Everline Mudhune.

Shukrani zingine ni kwa wasomi wenzangu tulioshirikiana nao vilivyo darasani na wakati wa kufanya utafiti. Kamwe siwezi kuwasahau wendani wangu; Kennedy Serede, Sarabina Karimi, Scott Oluoch, Lawi Kwendo, Jotham Muyumba na Lonah Kurema kwa kunishauri na kunitia motisha wakati wa utafiti. Nawatakia kila la heri maishani.

Mwisho, ni kwa wazazi wangu, mke wangu mpendwa na ndugu zangu. Walijitolea kwa hali na mali kunisaidia kimawazo na kifedha ili kufanikisha utafiti wangu. Mwenyezi Mungu awabariki na awazidishie maarifa na hela zaidi.

# IKISIRI

Utafiti huu umebainisha namna masuala ya dhuluma za kitabaka yanavyojitokeza katika riwaya za *Mkamandume* (2004) na *Shetani Msalabani* (1982). Waandishi wa riwaya hizi; Said A. Mohamed na Ngugi wa Thiong'o mtawalia wametuchorea picha halisi ya namna dhuluma za kitabaka zimekithiri katika jamii wanamoishi. Katika riwaya teule, wahusika wanyonge kutoka tabaka la chini wamedhulumiwa na wahusika wa tabaka la juu kwa misingi ya kiuchumi. Hali hii imechangia utengano uliopo baina ya wahusika maskini na matajiri katika riwaya za utafiti. Malengo ya utafiti yalikuwa ni kuonyesha jinsi dhuluma za kitabaka zinavyobainika katika riwaya teule, kubainisha athari zake kwa wahusika na kuchunguza mbinu wanazotumia wanyonge kujikomboa na kujiimarisha kimaisha. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Uhakiki wa ki-Marx ambayo iliasisiwa na Karl Marx na Engles (1959). Nadharia hii inaeleza kuwa historia ya maisha ya binadamu inaweza kuelezeka katika misingi yakinifu ya kiuchumi ambayo huchunguza njia kuu za uzalishaji na usambazaji mali. Tabaka la juu lenye watu wachache huwa na uwezo mwingi kiuchumi kuliko tabaka la chini lenye watu wengi wasiomiliki mali. Pia huonyesha namna jamii huimarika kutokana na migogoro ya kitabaka baina ya watu wa tabaka la chini dhidi ya wale wa tabaka la juu. Utafiti huu uligundua kwamba riwaya za *Mkamandume* na *Shetani Msalabani* zimeonyesha kwa undani namna tabaka nyonyaji linavyowanyonya wachochole wa tabaka la chini. Riwaya hizi zimebainisha suala la kiuchumi kama chanzo cha dhuluma zinazowakumba wahusika wanyonge. Aidha, dhuluma hizi zimesababisha athari chungu nzima katika tabaka la walalahoi. Vilevile, utafiti huu umebainisha kuwa wanyonge katika riwaya teule wanaungana na kujikomboa kiuchumi, kisiasa na kielimu. Mbinu walizotumia kupigania ukombozi ni: maandamano, migomo kazini, kuelimika kimasomo, uandishi wa vitabu vya fasihi na kuanzisha biashara ili kujikimu kimaisha. Utafiti huu utawazindua wahusika wanyonge kujikomboa dhidi ya dhuluma za kitabaka katika jamii.

## UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU

**Dhuluma:** Katika utafiti huu dhuluma inajumuisha; kudhulumiwa kimapenzi na kisaikolojia, kudunishwa, kutukanwa, kufanyishwa kazi nyingi, kupigwa, kuuawa kwa wanyonge, kubaguliwa katika ajira, kutengwa, kunyakuliwa kwa mashamba na kunyimwa uhuru.

**Utabaka:** Ni hali ya wahusika kuwa na hadhi na madaraja tofauti katika jamii kutokana na misingi ya kiuchumi na kisiasa.

**Tabaka:** Ni kundi la watu wenye hali moja linalotokana na jamii yenye mfumo wa kiuchumi ambao hugawanya watu kufuatana na uwezo wao wa kumiliki na kutawala njia kuu za kuzalisha mali.

**Tabaka la juu:** Ni kundi la watu wenye kumiliki mali nyingi na ndio husimamia mifumo ya uzalishaji na usambazaji mali katika jamii.

**Tabaka la chini**: Linaashiria kundi kubwa la wanyonge wenye mshahara na makazi duni.

**Dhuluma za kitabaka:** Dhuluma za kitabaka ni matendo ya kikatili ambayo yanafanyika kwa misingi ya kiuchumi na kisiasa ambapo wahusika wanyonge wa tabaka la chini wanadhulumiwa na wa tabaka la juu.

**Ubepari:** Mfumo wa kiuchumi unaowezesha watu wachache kumiliki raslimali na njia kuu za kiuchumi za uzalishaji mali ambayo hutumiwa na matajiri ili kujinufaisha huku wakiwadhulumu maskini wa tabaka la chini.

**Mafalahi:** Ni wakulima wadogo wa kujikimu tu, wasiomiliki misingi yoyote ya kiuchumi isipokuwa nguvu zao tu na ambao hutumiwa na mabepari kuzalisha mali nyingi shambani ili kuwanufaisha matajiri wenye kumiliki njia za uzalishaji mali.

**ABSTRACT**

This research has established the instances of social class injustices as portrayed in Kiswahili novels; *Mkamandume* (2004) and *Shetani Msalabani* (1982). The authors of these novels, Said A. Mohamed and Ngugi wa Thiong'o respectively, clearly depict to us a society where issues of social class injustices are evidently rampant. In these novels, several characters from the lower class have been oppressed and exploited by the characters from the upper class thereby contributing to the widening social gap between the rich and the poor. The objectives of the research were; to determine the instances of social class injustices in the selected novels, to establish the effects of the social class injustices among the characters and to evaluate the methods applied by the oppressed to free themselves from oppression. The research was guided by Classical Marxist theory of Marx and Engles (1959). This theory states that the history of human being life can be explained according to the economic status that examine the main means of wealth production and distribution. The upper class is made up of the rich people who owns wealth and oppress the poor who are many in the lower class. lt also shows how society progresses through the struggle between opposing forces that results in social transformation. lt views literary works as reflections of the social lnstitutions from which they originate. This research has found out various incidences of the class injustices against the poor based on economic factors as portrayed in Kiswahili novels: *Mkamandume* and *Shetani Msalabani*. The research has outlined the effects of the social class injustices among the characters and has also evaluated the methods that were applied by the oppressed to free themselves from oppression. The oppressed used the following methods: Demonstrations, strikes, acquiring higher education and starting of the business activities. This research will inspire the poor who are oppressed to fight for their rights and free themselves from oppression.

## YALIYOMO


**IKIRARI**......................................................................................................................**ii**

**TABARUKU**...................................................................................................................iii

**SHUKRANI** ...................................................................................................................iv

**IKISIRI**.............................................................................................................................v

**UFAFANUZI WA ISTILAHI MUHIMU**.........................................................................vi

**ABSTRACT**...................................................................................................................vii

**SURA YA KWANZA**…………………………………………………………………..1

1.0 Usuli wa mada..............................................................................................................1

1.1 Suala la utafiti..............................................................................................................3

1. 2 Malengo ya utafiti .......................................................................................................3

1.3 Maswali ya utafiti.........................................................................................................3

1.4 Sababu za kuchagua mada............................................................................................4

1.5 Upeo wa utafiti .............................................................................................................5

1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada .......................................................................................5

1.7 Misingi ya nadharia .......................................................................................................9

1.7.1 Mihimili ya nadharia ya Uhakiki wa Ki-Marx .........................................................12

1.8 Mbinu za utafiti ...........................................................................................................13

1.8.1 Uteuzi wa Sampuli.....................................................................................................14

1.8.2 Ukusanyaji wa data ....................................................................................................14

1.8.3 Uchanganuzi wa data .................................................................................................14

1.8.4 Uwasilishaji wa matokeo ...........................................................................................15

1.9 Hitimisho.......................................................................................................................15

**SURA YA PILI** ........ 16

**NAMNA DHULUMA ZA KITABAKA ZINAVYOJITOKEZA KATIKA RIWAYA TEULE** ........ 16

2.0 Utangulizi ........ 16

2.1.1 Muhtasari wa riwaya ya *Mkamandume* ........ 16

2.1.2 Muhtasari wa riwaya ya *Shetani Msalabani.* ........ 18

2.2 Kudhulumiwa kazini ........ 20

2.3. Kudhulumiwa kwa Mwanamke ........ 25

2.4 Kubaguliwa kwa Misingi ya Rangi ........ 29

2.5 Kudhulumiwa Kisaikolojia ........ 36

2.6 Ukiukaji wa Haki za Binadamu ........ 41

2.6.1 Dhuluma dhidi ya watoto ........ 41

2.6.2 Kudhulumiwa kwa Wapiga Kura ........ 44

2.6.3 Dhuluma dhidi ya Wafungwa ........ 48

2.7 Hitimisho ........ 50

**SURA YA TATU** ........ 51

**ATHARI ZA DHULUMA ZA KITABAKA KWA WAHUSIKA WA RIWAYA TEULE.** ........ 51

3.0 Utangulizi ........ 51

3.1 Ukosefu wa Mahitaji ya Kimsingi ........ 52

3.2 Ukosefu wa Ajira ........ 56

3.3 Kuuawa kwa Wanyonge ........ 60

3.4 Kutengwa kwa Wanyonge ........ 62

3.5 Uhasama Baina ya Wahusika ........ 67

3.6 Utengano wa Kifamilia ........ 69

3.7 Majuto ........ 72

3.8 Hitimisho .......... 77

**SURA YA NNE** .......... 78

**MBINU WANAZOTUMIA WANYONGE KUJIKOMBOA KUTOKANA NA DHULUMA ZA KITABAKA** .......... 78

4.0 Utangulizi .......... 78

4.1 Ukombozi wa kisiasa .......... 79

4.1.1 Kabla ya uhuru .......... 79

4.1.2 Baada ya Mapinduzi .......... 83

4.2 Ukombozi wa kiuchumi .......... 85

4.3 Ukombozi wa kielimu .......... 93

4.4 Hitimisho .......... 101

**SURA YA TANO** .......... 104

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** .......... 102

5.1 Utangulizi .......... 102

5.2 Muhtasari wa matokeo .......... 102

5.3 Mchango wa utafiti .......... 108

5.4 Mapendekezo .......... 108

**MAREJELEO** .......... 110

KIAMBATISHO 1 .......... 114

KIAMBATISHO 2 .......... 115

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Usuli wa mada

Bakhress (2010) anaeleza kuwa dhuluma ni kinyume cha haki na usawa. Ni kitendo cha kumnyima mtu haki. Katika utafiti huu dhuluma imejumuisha; kudhulumiwa kimapenzi na kisaikolojia, kudunishwa, kutukanwa, kufanyishwa kazi nyingi, kuuawa kwa wanyonge, kubaguliwa katika ajira, kunyakuliwa kwa mashamba na kunyimwa ajira.

Kwa mujibu wa utafiti huu, dhuluma za kitabaka ni matendo ya kikatili ambayo yanafanyika kwa misingi ya kiuchumi na kisiasa ambapo wahusika wanyonge wa tabaka la chini wanadhulumiwa na wa tabaka la juu. Marx na Engles (1959) wanaamini kuwa dhuluma za kitabaka hutokana na sababu za kiuchumi, ambapo tabaka la juu humiliki nyenzo zote za uzalishaji mali hivyo kulifanya kuwa na nguvu na uwezo mwingi kiuchumi. Tabaka hili huwa la watu wachache katika jamii lakini wenye uwezo kifedha. Kwa upande mwingine, tabaka la chini ndilo la watu wengi wasiomiliki chochote ila jasho lao na nguvu zao ambazo wanaziuza kwa wenye mali ili kujipatia mahitaji yao.

Osango (2015) anadai kuwa mazingira wanamoishi waandishi ambayo ni nchi ya Kenya pamoja na Visiwa vya Zanzibar na Pemba yameshuhudia dhuluma hizi wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni. Katika nchi ya Kenya Waingereza walipofika kabla ya uhuru walinyakua mashamba ya Wakenya na kuanza kuwadhulumu. Wao ndio waliomiliki mali katika tabaka la juu na waliwatumia Waafrika wa tabaka la chini kuzalisha mali zaidi. Visiwa vya Zanzibar na Pemba pia vilitawaliwa na Waingereza kuanzia mwaka wa 1890 baada ya Kongamano lililoandaliwa mjini Berlin nchini Ujerumani. Kongamano hilo liliamua kuligawa Bara la Afrika kwa mabepari.

Waingereza waliowatawala Waafrika kabla ya ukoloni, walikuwa na athari kubwa sana kwa utamaduni, uchumi, siasa na hata dini za kienyeji. Njogu (1987) anaeleza kwamba ukoloni kwa jumla ulivuruga muundo wa kijamii visiwani na kusababisha kuimarishwa kwa muundo wa kitabaka. Hii ni kwa sababu mali ilimilikiwa na wakoloni na kundi kubwa la Waafrika lililazimika kulitumia kundi ndogo.

Mwaka wa 1963 nchi ya Kenya ilijipatia uhuru baada ya mkoloni kuondoka na ikaanza kutawaliwa na viongozi wa Afrika. Taifa la Zanzibar pia lilijinyakulia uhuru mnamo mwaka wa 1963 kisha kukawa na mapinduzi mwaka wa 1964 yaliyoongozwa na Sheik Abedi Karume kupinga utawala wa Waarabu. Licha ya vifo vingi vilivyoshuhudiwa viongozi waliochaguliwa walitumia mamlaka yao vibaya kwa kuendeleza utabaka.

Watafiti wengi wamelishughulikia swala la dhuluma katika kazi mbalimbali za kifasihi. Baadhi ya watafiti hawa ni; Kamunde (1983) amewajadili wahusika mbalimbali kulingana na matabaka yao katika riwaya za; *Asali Chungu*, *Utengano* na *Dunia Mti Mkavu*. Gitau (2005) alitafiti juu ya unyanyasaji dhidi ya wanaume katika fasihi andishi ya Kiswahili naye Kavuria (2008) alichunguzu dhuluma dhidi ya watoto katika riwaya za Kiswahili. Pia, Kipyegon (2013) alitafiti namna mwanamke alivyonyanyaswa katika jamii ya ki-ubabedume. Tafiti hizi zimeangazia tu baadhi ya wahusika wanaodhulumiwa kutokana na mitazamo duni ya kijamii kama vile; taasubi ya kiume, mila na desturi ya jamii mbalimbali.

Hata hivyo, wahusika wanyonge wa tabaka la chini bado wanadhulumiwa na tabaka nyonyaji kwa misingi ya kiuchumi katika kazi za kifasihi. Utafiti huu umechunguza maudhui ya dhuluma za kitabaka kwa kurejelea riwaya za *Mkamandume* na *Shetani Msalabani*. Utafiti umelenga; kubainisha jinsi dhuluma za kitabaka zinavyodhihirika

katika riwaya teule, kueleza athari za dhuluma za kitabaka na kuchunguza mbinu wanazotumia wanyonge kujikomboa na kujiimarisha kimaisha katika riwaya teule.

### 1.1 Suala la utafiti

Utafiti huu umechunguza dhuluma za kitabaka katika riwaya za *Mkamandume* (2004) na *Shetani Msalabani* (1982). Msukumo wa utafiti huu ulitokana na visa vingi vya wanyonge wa tabaka la chini kudhulumiwa na tabaka nyonyaji katika riwaya teule. Pia, tafiti ambazo tayari zimefanywa hazikuangazia jinsi dhuluma za kitabaka zinavyojitokeza kwa misingi ya kiuchumi. Mathalan, Kimani (2003) ametafiti kuhusu dhuluma dhidi ya wanawake katika fasihi ya Kiswahili. Amebainisha kuwa mwanamke anakabiliwa na aina nyingi za dhuluma zinazotokana na wanaume. Utafiti wake umeangazia tu wanaume kama chanzo cha dhuluma zinazowakumba wanawake. Utafiti huu ni tofauti kwa kuwa umechunguza namna dhuluma za kitabaka zinavyojitokeza katika riwaya za utafiti, athari za dhuluma hizi na mbinu wanazotumia wanyonge kujikomboa kutokana na dhuluma za kitabaka. Kwa hivyo kuna umuhimu wa kutafiti kuhusu dhuluma za kitabaka katika riwaya teule.

### 1. 2 Malengo ya utafiti

Malengo ya utafiti huu ni :

1. Kubainisha jinsi dhuluma za kitabaka zinavyodhihirika katika riwaya teule.
2. Kueleza athari za dhuluma za kitabaka kwa wahusika wa riwaya teule.
3. Kuchunguza mbinu wanazotumia wanyonge kujikomboa na kujiimarisha kimaisha katika riwaya teule.

### 1.3 Maswali ya utafiti

Utafiti huu umeongozwa na maswali yafuatayo:

1. Dhuluma za kitabaka zimejitokeza kwa njia gani katika riwaya teule?
2. Dhuluma za kitabaka zina athari gani kwa wahusika wa riwaya teule?
3. Ni mbinu zipi wanazotumia wanyonge kujikomboa na kujiimarisha kimaisha katika riwaya teule?

**1.4 Sababu za kuchagua mada**

Mada hii ilichaguliwa ikizingatiwa kwamba, visa vya wanyonge kudhulumiwa na tabaka la juu vimekithiri katika kazi za fasihi. Aidha, wahusika wanyonge bado wanaendelea kudhulumiwa na mabepari wa tabaka la juu. Riwaya za *Mkamandume* na *Shetani Msalabani* zimeangazia maudhui ya dhuluma za kitabaka.

Sababu nyingine ni kuwa, waandishi wa riwaya teule ni wakazi wa nchi ya Kenya na Visiwa vya Zanzibar. Kwa hivyo, huenda wana ufahamu kuhusu dhuluma za kitabaka zilizotendeka katika kipindi cha kihistoria cha kupigania ukombozi na mapinduzi katika nchi zao za maeneo ya Afrika Mashariki. Njogu na Chimera (1999) wanaeleza kuwa msanii ni zao la jamii na anajaribu kuwasilisha matukio ya jamii katika uhalisia wake. Msanii anachota maudhui yake kutokana na hali halisi zinazomzunguka za kitamaduni, kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Kutokana na sababu hizi, kuna umuhimu wa kuchunguza dhuluma za kitabaka zinazotokana na tabaka nyonyaji linalowanyonya na kuwakandamiza wanyonge wa tabaka la chini. Utafiti huu unalenga kuihamasisha jamii kwa ujumla kuhusu masuala ya dhuluma za kitabaka yanavyojitokeza katika riwaya teule. Pia utachangia kuwazindua wanyonge wanaodhulumiwa kuungana na kupigania haki zao.

## 1.5 Upeo wa utafiti

Utafiti huu umejikita katika riwaya za *Mkamandume* na *Shetani Msalabani*. Riwaya hizi zimeteuliwa kwa kuwa zimeangazia masuala ya dhuluma za kitabaka miongoni mwa wahusika wa tabaka la juu na chini. Dhuluma hizi zilizoangaziwa ni; kupigwa, kutukanwa, kudharauliwa, kuuliwa, kunyimwa uhuru wa kujieleza na kufanya maamuzi katika ndoa, kufanyishwa kazi nyingi, kudhulumiwa kimwili na kisaikolojia, kulipwa mishahara duni na kubaguliwa kazini. Mazingira ya nchi ya Kenya na Visiwa vya Pemba na Zanzibar yamezingatiwa kwa kuwa riwaya teule zimejikita katika maeneo haya.

## 1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Kuna tafiti mbalimbali ambazo zimefanywa kuhusu suala la dhuluma na utabaka katika kazi za fasihi zinazorejelea mazingira wanamoishi waandishi:

Kamunde (1983), amewajadili wahusika mbalimbali katika *Asali Chungu*, *Utengano* na *Dunia Mti Mkavu*. Lengo lake lilikuwa kuonyesha tabia ya wahusika mbalimbali kulingana na matabaka yao. Kamunde anasema kuwa mifumo itumiwayo kuwadhalilisha wanyonge ni: siasa, uchumi na masuala ya jamii. Kulingana naye, kiini cha uovu ulimwenguni ni; mali, cheo, madaraka, ubinafsi, uroho, chuki na kadhalika. Anasema kuwa hali hii hutokea katika jamii ambapo mifumo ya siasa, uchumi, jamii na utamaduni imemilikiwa na watu wachache katika jamii. Aidha, anasema kuwa Said A. Mohamed anaamini kuwa hapatakuwa na amani mpaka matabaka ya kijamii yatakapovunjwa na kupondwapondwa na haki zitakapotambuliwa. Utafiti huu umetusaidia kuonyesha jinsi dhuluma za kitabaka zinavyobainika katika riwaya za utafiti. Tumebainisha namna masuala ya kisiasa na kiuchumi yanavyochangia kuwepo kwa dhuluma za kitabaka.

Gitau (2005) ametafiti juu ya unyanyasaji dhidi ya wanaume katika fasihi andishi ya Kiswahili. Anaonyesha kuwa ingawa wanaume wanasawiriwa kama viumbe walio na nguvu na ukakamavu pia hukabiliwa na unyanyasaji wa aina nyingi katika maingiliano yao na wanawake au wanaume wengine. Anaonyesha baadhi ya unyanyasaji kama vile; matusi, kupigwa na utengano wa kijamii kati ya mengine. Utafiti wake ni tofauti na huu kwa kuwa umewaangazia wanaume na wanawake kwa kutumia nadharia ya ki-Marx ilhali wao walitumia nadharia ya umuundo tekelezi. Hata hivyo umetufaa katika kuziba pengo lililoachwa na utafiti huo la kuangazia wahusika wote wanaodhulumiwa katika jamii.

Karanja (1990) amezihakiki tamthilia za kiukombozi za *Mzalendo Kimathi*, *Mukwava wa Uhehe* na *Kinjeketile.* Amezihakiki tamthilia hizi ili kubaini taswira yakinifu ya Mwafrika katika vita vya mapinduzi. Utafiti wake ulionyesha kuwa fasihi haina budi kuwa yakinifu ili itimize lengo lake la ukombozi. Aidha, kupitia kwa tamthilia hizi Mwafrika anajitokeza kupigania mapinduzi ili kujikomboa kutokana na dhuluma za mkoloni. Utafiti huu umetofautiana na wa Karanja kutokana na uteuzi wa vitabu vya utafiti. Licha ya utofauti, utafiti huu umetusaidia pakubwa kuchunguza mbinu walizotumia Waafrika kujikomboa kisiasa wakati wa utawala wa mkoloni katika riwaya za *Mkamandume* na *Shetani Msalabani.*

Kimani (2003) ametafiti kuhusu swala la dhuluma dhidi ya wanawake. Utafiti wake umebainisha hali tofauti za dhuluma zizazowakumba wanawake katika fasihi ya Kiswahili. Amedhihirisha kuwa mwanamke wa kiafrika anakabiliwa na dhuluma zinazomfanya ajihisi kuwa kiumbe duni. Utafiti wake ni tofauti na huu kwa kuwa wake umeangazia tu wanaume kama chanzo cha dhuluma zinazowakumba wanawake. Huu utafiti

umechunguza namna dhuluma za kitabaka zinavyojitokeza katika riwaya teule kwa misingi ya kiuchumi na kisiasa.

Kavuria (2008) ametafiti kuhusu dhuluma dhidi ya watoto katika riwaya za Kiswahili. Anasema kuwa watoto wanakumbwa na dhuluma zinazoviathiri viungo vyao, dhuluma za kimapenzi zinazotokea kwa kubakwa, dhuluma za kihisia kama vile; kutishwa, kuaibishwa, kutopendwa na kutotunzwa vizuri. Utafiti wake haukuangazia wahusika wote wanaodhulumiwa katika jamii kwa misingi ya kiuchumi. Utafiti huu umechunguza jinsi dhuluma za kitabaka zinavyobainika katika riwaya za *Mkamandume* na *Shetani Msalabani*. Riwaya hizi zinaangazia dhuluma zinazowakumba wanyonge wa tabaka la chini na mbinu wanazotumia kujikomboa dhidi ya dhuluma za kitabaka. Waandishi wa riwaya teule wamezingatia masuala ya kisiasa na kiuchumi kama visababishi vinavyochangia tabaka la juu ambalo ni nyonyaji kuendelea kukandamiza tabaka la chini kupitia mfumo bepari wa uzalishaji mali.

Dini inatumiwa kama chombo cha kuwadhulumu waumini katika jamii ya kisasa. Ng'etich (2011) amejadili kuhusu aina mbalimbali za dhuluma, athari za dhuluma hizo na namna ambavyo waandishi wanatumia mbinu za kisanaa kupinga udhalimu wa kidini. Katika jamii ya kisasa, waja wanaitumia dini kujinufaisha kihali na mali. Utafiti huu ni tofauti na wake kwa sababu alizingatia dini ya kikristo ila utafiti huu umechunguza dini za kiislamu na kikristo katika riwaya tofauti.

Kipyegon (2013) amesawiri mwanamke akinyanyaswa katika jamii ya ki-ubabedume. Ametumia nadharia ya ufeministi katika uchanganuzi wake. Ameonyesha jinsi mwanamke anavyochukiwa katika jamii. Kazi hii imetufaa katika kuangazia jinsi dhuluma za kitabaka zinavyojitokeza katika riwaya teule licha ya kuwa haijaonyesha kwa kina athari zake

miongoni mwa wahusika wa tabaka la chini. Utafiti huu umechunguza mbinu wanazotumia wanyonge kujikomboa, jinsi dhuluma za kitabaka zinavyojitokeza na athari zake katika riwaya teule na jamii.

Suakei (2013) anaangazia usasa na mwanamke wa kisasa katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke*. Anaongozwa na nadharia ya ufeministi kuzieleza changamoto zinazomkabili mwanamke wa kisasa mikononi mwa wanaume wenye ubabedume. Mhusika mkuu anajikomboa kimawazo na yuko tayari kuzipigania haki zake. Utafiti huu ni tofauti kwa kuwa tumeteua riwaya mbili na nadharia tofauti. Hata hivyo imetufaa katika kueleza jinsi wahusika wanyonge kama vile; Wariinga na Wangari wanavyojikomboa kutokana na dhuluma za kitabaka wanazopitia.

Osango (2015) ametafiti kuhusu ukombozi wa kisiasa na kiuchumi kwa kurejelea mazingira ya Zanzibar na Pemba. Alitumia nadharia ya uhalisia wa kijamaa katika riwaya ya *Mkamandume*. Utafiti huu unarejelea riwaya mbili ambazo ni; *Shetani Msalabani* na *Mkamandume* kwa kutumia nadharia ya uhakiki wa ki-Marx. Suala letu kuu la utafiti ni dhuluma za kitabaka. Licha ya utofauti huu, maelezo yake yametufaa katika kuangazia dhuluma zilizotokea katika Visiwa vya Zanzibar na Pemba wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni.

Kimeu (2016) amechunguza kuhusu maudhui ya ukombozi katika *Wimbo Mpya* na *Msururu wa Usaliti*. Ametumia nadharia ya umarksi kuelezea namna migogoro ya kitabaka hupelekea tabaka la chini kujikomboa kutokana na mfumo wa kibepari unaoendelezwa na tabaka la juu dhidi ya tabaka la chini. Utafiti huu umetufaa katika kuchunguza mbinu wanazotumia wahusika wanyonge kujikomboa kutokana na dhuluma za kitabaka. lmetuelekeza kuonyesha namna tabaka la juu linavyovunjiliwa mbali na wanyonge wa

tabaka la chini. Pia, nadharia hii imetusaidia katika kufafanua malengo kupitia kwa mihimili ya nadharia ya utafiti.

### 1.7 Misingi ya nadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Uhakiki wa ki-Marx ambayo iliasisiwa na Karl Marx na Fredrich Engles (1959). Wanadai kuwa kutokana na sababu za kiuchumi, hutokea matabaka ambapo tabaka moja humiliki nyenzo zote za uzalishaji mali hivyo kulifanya kuwa na nguvu na uwezo mwingi kiuchumi. Tabaka hili huwa la watu wachache katika jamii lakini wenye uwezo kifedha. Kwa upande mwingine tabaka la chini ndilo la wengi wasiomiliki chochote ila jasho lao na nguvu zao ambazo wanaziuza kwa wenye mali ili wayakidhi mahitaji yao. Tabaka la juu hutawala na kudhulumu tabaka maskini lisilokuwa na nguvu za kiuchumi bila hiari yao. Ni kutokana na dhuluma hizi ndiposa wanyonge huamua kujiondoa katika mtego huu kwa kushiriki mapambano ya nguvu ili kuwaondoa wenye nguvu kiuchumi.

Williams (1977) anadai kuwa nadharia hii ya Uhakiki wa ki-Marx, inasawiri kazi za kifasihi kama matukio halisi yanayorejelewa na mwandishi kutokana na mazingira anamoishi. Kulingana naye, fasihi ni taasisi ya kijamii na ina malengo mahususi yanayotokana na falsafa na mawazo ya mwandishi. Waandishi wa ki-Marx huandika kazi zao zinazoonyesha uwiano kati ya masuala yanayojadiliwa katika fasihi na namna yanavyojitokeza katika jamii ya mwandishi. Dhamira ya kimsingi ya Uhakiki wa ki-Marx inaweza kujumuisha uchunguzi wa kazi za fasihi zenye mwegemeo wa kisiasa ili kutathmini kama maudhui yake yanaangazia kuimarika kwa kazi hizi za kifasihi. Vilevile, inajumuisha kuhakiki utaratibu wa kitabaka unavyojitokeza katika kazi za fasihi.

Wahakiki wanasisitiza kuwa; kuna mwelekeo mkubwa wa kuitazama sanaa katika nadharia hii kwa kutilia mkazo mkubwa kwenye dhamira ya mwandishi. Lengo kuu huwa ni kuonyesha tofauti za kijamii, kisiasa na kiuchumi na kazi husika. Hii inaonyesha itikadi ya kijamii ya mwandishi na kuweka uhusiano kati ya uzoefu wa kijamii wa mwandishi na wahusika wake. Nadharia hii huiangalia fasihi kwa kuihusisha na mazingira yake ya kihistoria pamoja na shughuli zingine za kibinadamu. Wanadai kuwa ni nadharia inayopinga mtazamo wa kubagua au kutenga fasihi na mazingira yanayoizaa.

Wamitila (2006) anabainisha mawazo ya kimsingi ya nadharia ya ki-Marx. Kwanza, anaeleza kuwa historia ya maisha ya binadamu inaweza kuelezeka katika misingi yakinifu ya kiuchumi. Misingi hii itachunguza njia za uzalishaji mali pamoja na miundo ya kiuchumi inayoathiri sio uzalishaji mali hiyo tu bali na usambazaji wake. Pili, anaamini kuwa daima historia ya binadamu itadhihirisha au kuakisi harakati zinazoendelea katika matabaka ya kiuchumi. Historia ya maisha ya binadamu ni ya harakati za kitabaka.

Nadharia ya ki-Marx inaangalia matabaka katika ngazi mbalimbali za kifamilia, elimu na dini. Mwisho, matamanio na matakwa ya matabaka yaliyopo katika jamii na hasa tabaka lenye nguvu yanaakisiwa katika itikadi iliyopo katika jamii na miundo ya mawazo ambayo aghalabu huwa imeshika kwa nguvu na huwapo kila mahali kiasi cha wanajamii wasiitambue kwa haraka. Fasihi inayojitokeza inaweza kuyaakisi au kuyadhihirisha mahusiano ya nguvu katika jamii.

Nadharia hii huhitaji fasihi ieleze ukweli wa migogoro ya kimatabaka katika uhalisia wake. Kwa hivyo fasihi inapewa jukumu la kuonyesha dhuluma katika ubepari na pia kuonyesha juhudi za wanyonge kuondoa ubepari huo. Aidha, mwandishi sharti aonyeshe mabadiliko

ya kijamii hufuata kanuni za kiuchumi kwani ndicho kipengele muhimu kinachotawala mahusiano yote katika jamii.

Eagleton (2011) ambaye ni mwasisi wa hivi karibuni wa nadharia ya ki-marx, anadai kuwa ubepari ni mfumo wa ulafi, ukandamizaji na uangamizaji. Ubepari kama mfumo wa mashindano ya kiuchumi na ambao ni wa kuangamiza ndio unaosababisha kiwango cha juu cha kutoajiriwa na matokeo yake huwa ni uhalifu mwingi unaowafanya wahalifu kufungwa katika magereza ya kimagharibi. Kwa kudumisha viwango vya chini vya ujira waajiri wa kibepari hutofautiana na wafanyakazi wa kiwango cha chini wanaojaribu kupigania haki zao ili ujira wao uongezwe, hivyo basi kusababisha mapinduzi ya ki-marx.

Tabaka la wafanyakazi linalonyonywa kila wakati huamini kuwa litafaidika kutokana na juhudi zao. Eagleton anaeleza ndoto yake isiyokamilika kuhusu jamii yenye matabaka ya kategoria nne. Kategoria ya kwanza ni ya watawala ambao humiliki njia za uzalishaji mali. Kategoria ya pili ni ya matajiri wa kiwango cha kati huku kategoria ya tatu ikiwa ya kiwango cha chini. Kategoria ya nne ni ya wafanyakazi. Eagleton anapendekeza mfumo wa kiuchumi ambao unaweza kuthibitiwa na watu wote katika jamii. Anatusisitizia kuwa elimu na usimamizi mzuri wa nchi unaweza kupunguza athari ya ubepari.

Kwa ujumla wahakiki wote waliozungumzia nadharia hii wanasisitiza sana kuhusu ukombozi wa tabaka la chini dhidi ya tabaka la juu, ambalo ndilo humiliki mali nyingi zaidi na hunufaika kutokana na jasho la wanyonge. Wanasisitiza kuwa ukombozi utapatikana iwapo wanajamii wanaodhulumiwa wataungana pamoja kwa lengo la kuliondoa tabaka tawala na mifumo ya kibepari.

### 1.7.1 Mihimili ya nadharia ya Ki-Marx

Utafiti huu umeongozwa na mihimili ya nadharia ya ki-Marx kama ilivyofafanuliwa na Wamitila (2006):

1. Historia ya maisha ya binadamu inaweza kuelezeka kwa misingi yakinifu ya kiuchumi ambayo itachunguza njia ya uzalishaji mali pamoja na miundo ya kiuchumi na pia huathiri uzalishaji na usambazaji wa mali hizo. Kuna uwiano kati ya mhimili huu na maelezo ya waandishi katika riwaya teule. Mhimili huu umetusaidia kuangazia namna matajiri wa tabaka la juu walivyowadhulumu wanyonge wa tabaka la chini kwa lengo la kuzalisha mali. Katika riwaya za *Mkamandume* na *Shetani Msalabani* tumeonyesha mbinu wanazotumia matajiri kujinufaisha kutokana na jasho la wanyonge. Tumeelezea kwa kina namna mali inayozalishwa na wanyonge inamilikiwa na kutumiwa na matajiri pekee kuishi maisha ya kifahari ilhali maskini wanaishi maisha duni ya uchochole.
2. Wahakiki wa ki-Marx wanaamini kuwa historia ya maisha ya binadamu itadhihirisha au kuakisi harakati zinazoendelea katika matabaka ya kiuchumi na kijamii. Maelezo haya yamejitokeza bayana katika riwaya teule. Mhimili huu umetuwezesha kuchunguza suala la utabaka na uzukaji wa mfumo wa ubepari. Pia, tumeangazia tabaka la chini lenye maskini ambao huendeleza maisha yao kutokana na ujira mdogo wanaoupata kwa kufanya kazi kwa matajiri wa tabaka la juu. Mifano ya wanyonge katika riwaya teule ni wanabiashara wadogo, mafalahi na wale wasioelimika.
3. Ubepari kama njia ya uzalishaji mali utaharibiwa na kuvunjiliwa mbali na wafanyakazi wa tabaka la chini au wenyewe utaishia kujiangamiza kutokana na

mbegu za maangamizi zinazozisheheni. Hii imetufaidi kuonyesha namna ambavyo wanyonge katika riwaya teule wanajiimarisha kiuchumi na kujikomboa kutokana na dhuluma wanazopitia. Pia, imetusaidia kuelezea mbinu wanazotumia wanyonge kumaliza mfumo dhalimu wa uzalishaji mali unaowanufaisha matajiri pekee.

4. Migogoro ya kitabaka hutokana na kudhulumiwa kwa tabaka la chini kwa muda mrefu. Imebainika kuwa katika jamii ambayo imegawanyika kwa misingi ya kiuchumi, tabaka la juu lenye kumiliki mali ndilo huwadhulumu wanyonge wa tabaka la chini. Hali hii husababisha mgogoro wa kitabaka kati ya makundi haya mawili. Mhimili huu umetusaidia kuonyesha jinsi dhuluma za kitabaka zinavyobainika katika riwaya teule. Pia, umetuelekeza kuonyesha chanzo cha dhuluma za kitabaka na athari kwa wahusika wa riwaya teule. Masaibu yanayowakumba wanyonge wa tabaka la chini kutokana na dhuluma za kitabaka yameangaziwa kwa undani.

**1.8 Mbinu za utafiti**

Utafiti huu ni wa kimaelezo. Muundo wa kimaelezo umetumiwa kubainisha dhuluma za kitabaka katika riwaya za *Mkamandume* na Shetani *Msalabani* kwa kuzingatia malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia teule.

Utafiti huu ni wa maktabani. Mtafiti amesoma riwaya teule. Pia amepitia makala, majarida, vitabu na tasnifu mbalimbali zilizoandikwa kuhusu dhuluma za kitabaka.

Mbali na maktaba ya Chuo cha Kenyatta amezuru maktaba ya Chuo cha Nairobi na Mt. Kenya kwa minajili ya kusoma na kuchunguza vitabu na makala yanayohusiana na mada ya utafiti ili kupata maelezo zaidi.

### 1.8.1 Uteuzi wa Sampuli

Uteuzi wa sampuli ni wa kimaksudi. Kazi teule za fasihi andishi ya Kiswahili zimeteuliwa. Kazi hizi ni riwaya mbili ambazo *ni: Mkamandume* (2004) ya Said A. Mohamed na *Shetani Msalabani* (1982) ya Ngugi wa Thiong'o. Katika kubainisha jinsi dhuluma za kitabaka zimejitokeza riwayani, tumerejelea maelezo ya waandishi wa riwaya teule Mihimili minne ya nadharia ya ki-Marx ambayo imeteuliwa na mtafiti imetuongoza kuchanganua data inayohusiana na maswali na malengo matatu ya utafiti.

### 1.8.2 Ukusanyaji wa data

Data ya msingi imekusanywa kutoka maktabani kupitia mbinu ya kusoma riwaya za *Mkamandume* na *Shetani Msalabani*. Data ya upili imepatikana kwa kusoma machapisho na makala yanayohusu dhuluma za kitabaka na nadharia ya ki-Marx. Pia, mtandao na tovuti zimetumika ili kupata maelezo zaidi kuhusu mada ya utafiti.

### 1.8.3 Uchanganuzi wa data

Data ambayo imepatikana kupitia kusoma vitabu vilivyoteuliwa imechanganuliwa kwa njia ya kimaelezo. Kwanza, tumebainisha namna masuala ya dhuluma za kitabaka yamejitokeza katika riwaya teule kwa kutumia mhimili unaozungumzia njia za uzalishaji mali pamoja na miundo ya kiuchumi na usambazaji wa mali hizo. Mambo yanayochangia kuwepo kwa dhuluma za kitabaka dhidi ya wahusika wanyonge yametafitiwa. Masaibu yanayowakumba wahusika wanyonge wa tabaka la chini yameangaziwa ili kubaini chanzo chake.

Pili, tumechanganua athari za dhuluma za kitabaka miongoni mwa wahusika na katika jamii ya mwandishi kwa kuzingatia mhimili unaoeleza kuwa migogoro ya kitabaka hutokana na kudhulumiwa kwa tabaka la chini kwa muda mrefu. Tumeonyesha namna

dhuluma za kitabaka zimewaathiri wahusika pamoja na jamii husika. Tumeangazia wahusika wanyonge wa tabaka la chini ambao wamedhulumiwa na matajiri wa tabaka la juu. Baadhi ya athari za dhuluma hizi ni kama vile ; kupigwa, kuuawa kwa wanyonge, kubaguliwa katika ajira, kunyakuliwa kwa mashamba, kudhulumiwa kimapenzi, kufanyishwa kazi nyingi, kudunishwa na kunyimwa uhuru wao.

Mwisho, tumebainisha mbinu wanazotumia wanyonge kujikomboa kutokana na dhuluma za kitabaka. Uchanganuzi umeongozwa na mhimili unaoeleza kuwa ubepari kama njia ya uzalishaji mali utaharibiwa na kuvunjiliwa mbali na wafanyakazi wa tabaka la chini. Utafiti umeonyesha namna ambavyo wanyonge wa tabaka la chini katika riwaya teule wanavyojiimarisha kiuchumi na kujikomboa kutokana na dhuluma za kitabaka wanazopitia.

### 1.8.4 Uwasilishaji wa matokeo

Matokeo ambayo yanapatikana kutokana na uchanganuzi wa data yamewasilishwa kwa njia ya kimaelezo. Maelezo haya yamezingatia ufafanuzi wa dhuluma za kitabaka katika riwaya teule. Uwasilishaji wa matokeo umefanywa kwa kuzingatia maswali ya utafiti, malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia teule.

## 1.9 Hitimisho

Katika sura hii, tumeshughulikia mambo ya kimsingi ambayo ni ; usuli wa mada, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo wa utafiti, misingi ya nadharia, mihimili ya nadharia ya ki-Marx, yaliyoandikwa kuhusu mada, mbinu za utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo. Sura inayofuata tumeonyesha namna dhuluma za kitabaka zinavyobainika katika riwaya za *Mkamandume* na *Shetani Msalabani*.

# SURA YA PILI

# NAMNA DHULUMA ZA KITABAKA ZINAVYOJITOKEZA KATIKA RIWAYA TEULE

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inachunguza namna dhuluma za kitabaka zinavyojitokeza katika riwaya za *Mkamandume* na *Shetani Msalabani*. Dhuluma zinazobainika ni: kudhulumiwa kazini, kudhulumiwa kwa mwanamke, kubaguliwa kwa misingi ya rangi, kudhulumiwa kisaikolojia na ukiukaji wa haki za binadamu. Nadharia ya uhakiki wa ki-maksi imebainisha matabaka yanayotokana na sababu za kiuchumi. Kuna uwiano kati ya haya maelezo na masuala yanayojadiliwa na waandishi katika riwaya teule.

Kavuria (2008) anadai kuwa, dhuluma ni dhana inayojumuisha vitendo visivyo vya haki, maonevu ya kimwili, kijinsia, kihisia na matumizi ya lugha anayofanyiwa mtu kwa namna ambayo inamvunjia heshima na kumnyima haki zake za kibinadamu. Kwa mujibu wa utafiti huu, dhuluma za kitabaka ni matendo ya kikatili ambayo yanafanyika kwa misingi ya kiuchumi na kisiasa ambapo wahusika wanyonge wa tabaka la chini wanadhulumiwa na tabaka la juu.

### 2.1.1 Muhtasari wa riwaya ya *Mkamandume*.

Riwaya ya *Mkamandume* inaangazia vipindi mbalimbali vya utawala; kabla ya kuja kwa mkoloni wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni. Hadithi inaanza kwa masimulizi ya usuli wa Mkamandume ambaye ni mhusika mkuu. Historia ya nchi ya Malelejimema inasimuliwa. Inadaiwa kuwa binadamu wa mwanzo ndio walioipa nchi hiyo jina la Maleleji mema. Kizazi cha awali cha watu kilitokana na viwiliwili viwili vilivyopuliziwa roho kisha

baadaye vikachukua sura ya ndume na mke. Nchi ya Malelejimema ilijengeka kwa misingi ya wema uliowavutia wageni kutoka karibu na mbali. Mkamandume alikuwa na familia iliyojumuisha Tufaa mkewe, watoto wake Time, Fikirini, Mtumwa, Msimu, Viwe, Katija na mamake Bi. Fuu. Mkamandume alionyesha mabadiliko katika ndoa yake jambo lililomshangaza mkewe. Hali hii inadhihirika anavyomwadhibu kikatili bintiye Viwe baada ya kugundua alikuwa mja mzito. Jambo hili linasababisha utengano wa kifamilia kati yake na Viwe.

Kazini, Mkamandume alidhulumiwa sana na Bosi wake. Alifanya kazi ya kusafisha vyoo bila vifaa vya kuosha hali iliyochangia kazi yake kuwa ngumu zaidi. Tuzo ya mfanyikazi bora ilitolewa kwa mapendeleo. Licha ya bidii yake kazini, hakutuzwa hata siku moja. Tuzo ilimwendea Zuhura Saleh Mcheshi kinyume na matarajio ya wengi waliomtarajia Mkamandume kutokana na bidii yake kazini.

Mwishowe, Mkamandume alipewa likizo ya miezi mitatu bila malipo yoyote. Hali hii ilimkera sana Mkamandume na kumfanya awe na uhasama dhidi ya Bosi wake. Alianza kulipiza kisasi dhidi ya mahasimu wake wa jadi akiwemo babake Soud. Kutokana na chuki alipuuzilia mbali posa ya Soud aliyekuwa akimchumbia bintiye, Nadia. Licha ya uhasama huu Soud anajitolea kumsaidia Mkamandume kwa kila hali ngumu anayokumbana nayo.

Mzee Mkasi na Bw. Sleyyum wanamsimulia Soud masaibu yaliyowakumba wakati wa vita vya wenyewe kwa wenyewe. Mzee Mkasi hakutaka kukumbuka vita vya pili vya dunia vilivyofanyika kwa njia ya kikatili. Kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe aliwapoteza Mkewe Biti Sahera na Masudi mwanawe. Anaeleza namna alivyodhulumiwa wakati wa vita vya ukombozi katika nchi ya Malelejimema. Alishikwa na kuwekwa kizuizini bila hatia yeyote. Aliteswa sana kizuizini.

Mkamandume alisafiri kwenda makao makuu kumtafuta bintiye Viwe. Njiani alipoteza fahamu na akaokotwa na wavuvi. Alishangazwa na mabadiliko ya makao makuu kwani awali ilikuwa duni kuliko Malelejimema. Alikutana na Soud hotelini baada ya kushindwa kulipia gharama ya chakula alichokula. Soud alimlipia na kumfahamisha hatua alizopiga katika uhusiano wake na Nadia. Pia, alikutana na mwanawe Viwe ambaye alikuwa amebadilika sana. Alikuwa msomi na mwanabiashara. Alishirikiana na Soud kuanzisha michezo ya tamthilia ya kuwazindua wanajamii. Mwishowe, alirudi tena Msera kwenda kukabiliana na adui yake Bw. Shombo. Baada ya kumkata shingo kwa upanga alimwendea. Bosi wake na kumwangamiza kisha akajiunga na umati wa waandamanaji. Polisi waliwavamia waandamanaji na kuwafyatulia risasi, Mkamandume alifyatuliwa risasi na akaangamia alipokuwa akimkinga Soud.

### 2.1.2 Muhtasari wa riwaya ya *Shetani Msalabani.*

*Shetani Msalabani* ni hadithi ya wazalendo wanne: Wariinga, msichana aliyenyanyaswa sana na vibaraka wa wabeberu, Wangari, mkulima mdogo aliyetaabishwa na mabepari, Muturi mfanyikazi mwerevu na Gatuiria, kijana aliyeelimika sana.

Wariinga analelewa na shangaziye baada ya wazazi wake kutiwa gerezani wakipigania uhuru. Kutokana na hali ya umaskini anashawishika kufanya uhusiano wa kimapenzi na tajiri la Ngorika. Baada ya kupachikwa mimba, Tajiri anajitenga naye kabisa, analazimika kuacha shule. Hali inaendelea kuwa ngumu na baada ya kujifungua anasafiri kwenda Nairobi ili kutafuta ajira ya kujikimu. Anabahatika kupata kazi ya kupiga chapa na kuandika habari kwa njia ya mkato katika ofisi ya *Champion Construction Company*. Bosi wake Kihara alianza kumnyemelea akitaka awe mpenziwe. Alipokataa katakata anaamua kumwachisha kazi.

Siku hiyo pia mchumba wake alivunja uhusiano wao wa kimapenzi kwa kumshuku kuwa alikuwa amelala na Bepari Kihara. Tajiri wake wa nyumba alimwendea na kutaka aongeze kodi ya nyumba. Aliposhindwa alihamishwa kwa kurushiwa vitu vyake vyote nje. Wariinga alijaribu kujiua lakini aliokolewa na kijana mmoja. Mwishowe, alijiunga na wasafiri wenzake kuelekea Ilmorog. Wote wanasafiri kwa matatu ya jambazi moja linaloitwa Mwaura ambalo limeajiriwa na mabepari kutaabisha na kunyanyasa jamii.

Wote walikuwa wanaelekea Ilmorog kujionea mashindano ya wizi na unyang'anyi wa kisiasa ili wavikwe taji na kuteuliwa kuwa wanyapara wa mali ya Wabeberu nchini. Njiani Wangari aliwasimulia hadithi yake namna alivyokuja Nairobi kutafuta ajira kisha akashikwa na kutiwa gerezani. Baada ya kufungiwa kitunduni kwa siku tatu alipelekwa mahakamani na kushtakiwa kwa mambo mawili; kudhaniwa wizi na uhuni. Alitozwa faini ya shilingi mia mbili ya kuzurura mjini bila kibali. Mwaura pia aliwafichulia namna ambavyo alijipatia utajiri wake kutokana na dhuluma alizowatendea wanajamii kwa tamaa ya kutajirika haraka. Alieleza namna alivyokuwa akiwakata watu vichwa wakati wa kupigania mapinduzi ili kujinufaisha na mali.

Walipofika Ilmorog walijionea namna wezi wa mali ya jamii walivyojigamba kutokana na unyonyaji wa tabaka la chini. Walijidai na mbinu dhalimu walizotumia kulinyonya tabaka la watu wachochole. Katika harakati za kutapatapa walifumaniwa na wazalendo wa Ilmorog pamoja na wananchi wengine mashujaa. Kwa upande mwingine, Wariinga walisafiri na mpenziwe kwenda kwao kwa ajili ya ndoa iliyokuwa imeandaliwa. Ilijitokeza bayana kwamba lile tajiri la Ngorika lililompachika Wariinga mimba ndilo lililokuwa babake mpenziwe. Lilijaribu kusimamisha harusi isiendelee lakini Wariinga akaliangamiza

kwa kulipiga risasi. Kuangamizwa kwake kukawa mwanzo wa kizazi kipya chenye usawa kwa kila mwanajamii.

Utafiti huu umeangazia aina mbalimbali za dhuluma zinazojitokeza katika riwaya za *Mkamandume* na *Shetani Msalabani*.

**2.2 Kudhulumiwa kazini**

Hii ni aina ya dhuluma ambapo wahusika wa tabaka la juu ambao ni waajiri huwadhulumu waajiriwa wa tabaka la chini. Waajiri ndio humiliki nyenzo za uzalishaji mali na huwatumia waajiriwa kuzalisha mali zaidi kwa manufaa yao pekee. Hali hii husababisha utengano ambapo kundi la waajiri huishi maisha ya kifahari ilhali waajiriwa huishi maisha duni ya uchochole.

Mayieka (2015) anadai kwamba wafanyakazi ni kiungo muhimu katika kuendeleza taifa. Juhudi zao kazini huchangia ukuaji wa uchumi na maendeleo katika sekta mbalimbali. Kwa hivyo, maslahi yao sharti yazingatiwe na waajiri ili kuwapa motisha ya kufanya kazi kwa bidii na kuzalisha mali zaidi. Kupitia kwa vyombo vya habari tumeshuhudia namna waajiri wengi barani Afrika wamepuuza mahitaji ya wafanyakazi wao. Hali hii imechangia migomo na kuzorota kwa uchumi.

Unyanyasaji wa wafanyakazi unajitokeza wazi katika riwaya za utafiti. Said A. Mohamed (2004) anadhihirisha namna Mkamandume na wafanyakazi wengine ambao walikuwa wameajiriwa walidhulumiwa kazini na bosi wao. Licha ya wao kufanyishwa kazi nyingi za sulubu na kukejeliwa hawakutambuliwa kama wafanyakazi bora. Mwandishi anasema kuwa:

*Vicheko vya wafanyakazi wake wengi havikuwa vicheko vya furaha hata chembe. Vilikuwa vicheko vya maumivu. Bosi aliwadunisha wafanyakazi na kuwaona wajinga (uk 27).*

Mazingira ya kazini hayakuwa ya kupendeza. Mkamandume alitatizika kuosha vyoo kutokana na ukosefu wa maji. Mwandishi anaeleza kuwa:

*... na kwa kawaida yake huanza kazi ngumu kwanza na kazi ngumu ni ipi zaidi kuliko ya kufagia vyoo vya ofisi hii hasa siku hizi ambapo mara nyingi hakuna maji wala vifaa. Kuvisafisha vyoo bila ya maji bila ya sabuni. Tena kwa fagio bovu (uk 323).*

Mbali na kazi aliyoajiriwa kufanya ya kusafisha vyoo, aliongezewa kazi nzito ya kuziteremsha fanicha na kuzitia ndani. Hali hii inakiuka haki za wafanyakazi kwa kuwa mwajiri anamdhulumu Mkamandume kwa kumwongezea kazi bila malipo zaidi licha ya kazi hiyo kuwa ngumu zaidi. Aidha alipewa vitisho bila kuhurumiwa. Katika riwaya ya *Mkamandume*, tunaambiwa kwamba:

*Samani zilikuwa nzito kwelikweli na mara kwa mara mkuu wa ofisi aliwaonya. Mkija kuvunja chochote itabidi msipate mishahara yenu miezi sita mnajua bei za vitu hivyo? (uk. 324).*

Wafanyakazi hawakulipwa wakati wa likizo. Mkamandume halipwi mshahara anapoomba likizo ya miezi mitatu kutokana na kazi ya sulubu iliyomfanya kuwa mgonjwa. Mwandishi anaeleza kuwa:

> *Barua ilisema wazi kwamba amepewa likizo ya miezi mitatu, lakini wizara ilisikitika sana kwamba haikuwa na pesa za kumpa kwa ajili ya likizo yake. (uk332).*

Walimu pia ni miongoni mwa wanyonge waliodhulumiwa na waajiri wao. Katika riwaya ya *Mkamandume*, mazungumzo kati ya Soud na Bilal aliyekuwa mwendawazimu yanaonyesha namna mwalimu Seyyid Kakhtan alivyodhulumiwa kazini. Tunaambiwa kwamba:

> *Marehemu maskini, Mungu amlaze pahala pema huko aliko-walimdhulumu vibayavibaya. Walimwachisha kazi na kumwacha atambe na njia ugenini. Mbali na kazi ya kufundisha walimu waliongezewa kazi zingine kwa lazima. Soud alikumbuka dhuluma walizofanyiwa walimu katika kazi zisizokuwa zao kwa jina la kujitolea (uk 244).*

Ajira kazini ilitolewa kwa mapendeleo. Waajiri waliwapendelea watu wao waliotoka katika tabaka la juu na kuwatenga wale wa tabaka la chini ambao hawakuwa na usemi. Kwa kurejelea riwaya ya *Mkamandume* Meneja wa Shirika la Biashara alikuwa mwanawe mwenyekiti wa chama tawala na mwakilishi wa jimbo la kaskazini. Cheo hicho alichopewa si kwa uwezo, ujuzi au busara, bali kwa sababu ya babake. Tunaambiwa kuwa:

> *Jengine ni la mwanawe mwenyekiti ambaye ni Meneja wa Shirika la Biashara –Cheo alichopewa si kwa uwezo, ujuzi au busara, bali kwa sababu tu alikuwa mtoto wa mwenyekiti wa chama na mwasisi (uk 114).*

Vilevile, dhuluma kazini inajitokeza katika riwaya ya *Shetani Msalabani*. Wangari alilazimika kuhamia jijini Nairobi kutafuta kibarua baada ya kishamba chake cha ekari

mbili kunadiwa na Benki aliposhindwa kulipa mkopo wao wa shilingi elfu tano. Alishangazwa ni kwa nini pesa nyingi wanazokopeshwa na nchi za kigeni hutumika kustawisha jiji la Nairobi na miji mingine mikubwa wanakoishi matajiri wa tabaka la juu. Isitoshe mafalahi walimapo, mavuno yao yote huyapeleka Nairobi na miji mingine mikubwa yote kuyauza. Kwa hivyo jasho la maskini huwanufaisha watu wa tabaka nyonyaji pekee jijini ilhali wanaozalisha mali hiyo huteseka na kuishi maisha duni.

Gatuiria anamweleza Wariinga kuhusu utajiri wa babake alioupata kwa kuwadhulumu wanyonge kazini. Alikuwa mfanyibiashara mwenye kumiliki maduka mengi mjini Nakuru na mashamba makubwa katika eneo la Rift Valley. Pia alikuwa na biashara nyingine nyingi za kuagiza na kupeleka vitu ulaya kwa eropleni. Licha ya kuwa mwanawe wa pekee hakupendelea mienendo ya babake kwa kuwa wafanyakazi wao walikula vyakula duni na kuvaa matambara. Katika riwaya ya *Shetani Msalabani* tunaambiwa kuwa:

> *Mara kwa mara babangu aliwapiga bakora huku akiwatukana vibaya na kuwaita ng'ombe. Wakati mmoja nilishuhudia akimpiga mama yangu eti kwa sababu alimwambia asimpige mfanyakazi mkongwe kabisa* (uk 139).

Ushahidi wa Nditika wa Ngunji kutoka tabaka la juu unaaonyesha namna alivyowadhulumu wafanyakazi kazini. Kazi yake maalumu ilikuwa ni kunyang'anya na magendo. Alinunua nafaka wakati wa mavuno na kuwauzia wakulima walewale kwa kuwanyonya. Pia alinunua bidhaa kabla ya bajeti kutangazwa na kuiuza kwa bei ghali. Hakujali maslahi ya wafanyakazi wake. Mwandishi anadai kuwa:

> *Wafanyakazi wake walijaribu kugoma siku moja na akawafuta kazi wote bila notice (uk 189).*

Kimeenderi wa Kanyuanji pia alikuwa mtu katili sana. Alipewa jina hilo wakati wa hali ya hatari kwa kuwasaga wafanyakazi na mafalahi. Katika riwaya ya *Shetani Msalabani*, tunaambiwa kwamba:

> *… alikuwa hayawani kabisa. Aliwaamuru wanaume na wanawake walale barabarani halafu akapitisha gari la Land Rover juu ya miili yao. Licha ya ukatili huu alipandishwa cheo akawa katibu wa kudumu. Baadaye aliajiriwa na Makampuni ya wageni hasa yaliyohusika na pesa. Mashamba yake hayana idadi* (uk 199).

Mazungumzo kati ya Muturi na akina Wariinga yanaonesha namna Askari wakiwa kazini hushirikiana na mabepari kuwadhulumu raia. Kwa kurejelea riwaya ya *Shetani Msalabani* Muturi anasema kwamba:

> *Mimi ni mfanyakazi na ninajua waziwazi kuwa askari huwa upande wa wanyang'anyi na wezi wanaowaibia wafanya kazi mali zinazotokana na jasho lao na wawanyang'anyao mafalahi mavuno na ardhi yao. Amani wanayoilinda ni ya mabepari wanaokula na kunywa ili wasisumbuliwe na wale wanaotaabika kwa njaa na kiu (uk 217).*

Kupitia kwa mbinu rejeshi Muturi aliwasimulia wenzake namna alivyoachishwa kazi na Boss wake Kihara. Hali hii ilitokea alipoungana na wafanyakazi wengine kuitisha nyongeza ya mishahara jambo lililowasababishia balaa. Mwajiri wake alidai kuwa mgomo wowote ulikuwa ni marufuku kufuatana na amri ya rais. Mwishowe, aliamuru kuwa mfanyakazi ambaye hataki kuendelea na kazi aende zake kwani kulikuwa na watu wengi waliokuwa wakitafuta kazi. Msimulizi anaeleza kuwa:

> *Viongozi wote wa wafanya kazi hao wakaachishwa kazi. Hii ni ukiukaji wa haki za wafanyakazi kwa kuwa wao wana haki ya kutetea maslahi yao na waajiri sharti wawasikilize (uk 73).*

Mwaura, mmiliki wa matatu, alikiuka haki za wananchi wenzake. Wakati wa vita vya ukombozi alikuwa msaliti mkali kama pilipili. Alikuwa katika kikundi cha wauaji kilichoongozwa na mzungu. Wakati huo alilipwa shilingi tano kwa kila kichwa kimoja cha Mau Mau. Aliwatendea Waafrika wenzake ukatili bila kujali. Hakuchagua, si mwanaume, si mwanamke, si msichana wala mvulana. Nia yake ilikuwa tu kujinufaisha na pesa bila kujali ukiukaji wa haki yao ya kuishi. Alikuwa ni mtu katili aliyeabudu pesa sana. Mwaura alidhihirisha ukatili wake alipokosana na mtu aliyekodi gari lake na akakataa kumlipa shilingi tano. Alimwangamiza bila kujali haki yake ya kuishi. Msimulizi anasema kuwa:

> *Asubuhi moja huyo mtu alionekana kwake akiwa mkavu wa juzi huku ameninginia kwenye kitanzi cha kamba (uk 30).*

Nadharia ya uhakiki wa ki-Marx inaeleza kuwa historia ya binadamu inaweza kuelezeka kwa misingi yakinifu ya kiuchumi ambayo itachunguza njia ya uzalishaji na usambazaji wa mali. Ni kutokana na mhimili huu ndiposa tumeangazia namna matajiri wa tabaka la juu wanavyowadhulumu wanyonge wa tabaka la chini kwa lengo la kujinufaisha kiuchumi.

### 2.3. Kudhulumiwa kwa Mwanamke

Kwa mujibu wa utafiti huu wanawake wanaodhulumiwa ni wa tabaka la chini. Dhuluma ambazo zimejitokeza ni; kudunishwa, kutukanwa, kupigwa kikatili, kudhulumiwa kimapenzi na kisaikolojia.

Katika riwaya ya *Shetani Msalabani* (1982) visa vingi vya kudhulumiwa kwa wanawake vinabainika. Mwandishi anasimulia matukio mengi ya namna waajiri walivyowadhulumu

wanawake wanyonge hasa wa tabaka la chini kazini. Mwandishi anaeleza kuwa baada ya Wariinga kumaliza masomo yake na kufaulu katika Kiingereza, Kiswahili na Dini alianza kutafuta kazi. Bosi wake wa kwanza alimtaka wafanye mapenzi naye ili apate kazi. Bosi wake anamwambia kuwa:

> *… lakini msichana kama wewe hawezi kukosa pahali ambapo anaweza kupachikwa. Lakini mambo haya yote hayawezi kuzungumziwa hapa afisini. Twende pahala paitwapo Upendo Mamboleo Bar and Lodging tukazungumze zaidi* (uk 16).

Jacinta Wariinga anakiri kwamba mambo haya aliyotendewa yalifanyika katika ofisi zote na yaliwaathiri wanawake waliokuwa wakitafuta kazi mjini kwa matajiri.

> *Hebu aingie katika ofisi nyingine na kumkuta bwana Boss mwingine. Vicheko ni vile vile; maswali ni yale yale. Maagano ni yale yale na vihoteli. Shabaha ni pale mapajani pa Kaledi. Upendo Mamboleo Bar and Lodging ndiyo afisi ya kuajiria wasichana na mapaja yao ndiyo yanayotiliwa sahihi (uk 16).*

Baada ya Wariinga kupata kazi kwa Boss Kihara, tajiri wake anajaribu kumshawishi kwa kumpa mali na pesa ili awe mpenzi wake kazini. Kihara alimwahidi kuwa:

> *Nitakupangisha nyumba Furaha Leo Estate au hata mjini Kenyatta Avenue au upande mwingine wowote wa Nairobi. Wewe chagua tu uniambie nyumba hiyo niipambe hata kwa kila kitu; vitanda, meza, viti, magodoro, mapazia, mazulia, vitambaa, chochote unachotaka.*

*Nitaviagizia vitu vyote kutoka Paris, London, Berlin, Rome, New York, Tokyo, Stockholm na hata Hong Kong (uk18).*

Licha ya kuahidiwa haya yote Wariinga anakataa katakata kushawishika hali inayomfanya Boss kutumia nguvu wakiwa afisini mwake. Tunaambiwa kuwa:

*Ghafla anamrukia Kaledi kama paka amrukiavyo panya. Boss anamshika Kaledi kiunoni kwa mkono mmoja na kwa mwingine anampapasapapasa mwilini, Kaledi anajaribu kujinasua huku akimchapa makonde kifuani.* (uk 20).

Wariinga anakumbwa na dhuluma kutoka kwa tajiri aliyekuwa amemkodishia nyumba ya kupanga. Baada ya kufutwa kazi, Wariinga aliandamwa na matatizo mengi. Tajiri wa nyumba aliyekodi alimwendea na kumtaka amwongezee kodi ya nyumba. Hii ilikuwa kinyume na makubaliano yao hasa ikizingatiwa mazingira yalikuwa duni sana. Wariinga anachora taswira ya makazi yenyewe anaposema kuwa:

*… lakini jamani, hii ilikuwa nyumba au kiota cha ndege? Sakafu ilikuwa na mashimo, ukuta ulikuwa na mianya mingi mikubwa na paa lilikuwa linavuja (uk. 6).*

Wariinga alipokataa kuongeza kodi, tajiri wake alimletea majambazi wakamvurumisha nje bila kujali. Yule tajiri alimwambia Wariinga kuwa:

*Nimekuletea maafisa wa mahakamaa kodi za nyumba (uk.6).*

Vitu vyote vya Wariinga vilivurumishwa nje kama takataka na kijumba kikafungwa kwa kufuli nyingine.

Katika riwaya ya *Mkamandume*, wanawake walidunishwa na kudhulumiwa. Walipigwa kikatili na waume wao kwa makosa madogo madogo. Mwandishi anasema kuwa:

> *Wanawake walilia na kutoa ukwenzi kila usiku na mchana walipopigwa na waume wao kwa makossa madogo madogo kama kuzidisha chumvi katika chakula (uk.85).*

Kupitia kwa maswali ya balagha Time, bintiye Mkamandume alikerwa sana na jinsi wanaume walivyomzungumzia vibaya na kumwita janajari lililo jina la dadake, Mtumwa. Kulingana nao hakuwa na tamaa ya kupata mume. Time anajiuliza maswali mengi anaposema kuwa:

> *Wanaume sijui lini watamwacha mwanamke huru? Sijui lini watajali mambo yao wenyewe badala ya kuyajali mambo ya wanawake kila siku? (uk 89).*

Mazungumzo kati ya mzee Mkasi na Time yanaonyesha wazi namna wanawake wanavyodhalilishwa na kufanyiwa maamuzi katika ndoa. Time anamuuliza mzee Mkasi kuwa:

> *… hivi wakati wenu kwa nini mlioa au mliozwa wake kwa kuchaguliwa au kwa nguvu na wazee? (uk 177).*

Mzee Mkasi anamuelezea bayana kuwa mambo hayo bado yanaendelezwa na baadhi ya koo. Anadai kuwa wazee waliamini kwamba watoto wao wanabaki watoto tu hata wakiwa watu wazima na kwa hivyo hawana uwezo na maarifa ya kuchagua baya na zuri. Bi. Mbunjaki alilalamika kuwa mumewe alimwachia kazi zote za nyumbani kutekeleza. Alitumiwa kama chombo cha kuzaa, kupika, kuosha na kulea watoto. Analalama kuwa*:*

> *Mwangalizi wa kibanda ni mimi- chumbani, ukumbini, jikoni, uani, msalani… Pia mimi mtafuta riziki katika ulimwengu mgumu usiokamulika riziki (uk 420).*

Mhimili wa nadharia ya utafiti huu unaeleza kuwa, migogoro ya kitabaka hutokana na kudhulumiwa kwa tabaka la chini kwa muda mrefu. Katika riwaya za utafiti wahusika wanawake kutoka tabaka la chini wamedhulumiwa na wahusika wanaume wa tabaka la juu wanaomiliki nyenzo za uzalishaji mali. Hali hii imechangia mgogoro baina ya makundi haya mawili.

### 2.4 Kubaguliwa kwa Misingi ya Rangi

Dhuluma hii inajitokeza bayana wakati wa utawala wa mkoloni ambapo wazungu waliomiliki mali nyingi walijiona bora sana kuliko Waafrika ambao walikuwa maskini. Osango (2015) anasema kuwa tofauti za rangi zilikuwa misingi ya kuwagawanya watu. Ubaguzi huu ulikuwa umepandikizwa na Mwingereza. Mifumo yote ya kisiasa, kiuchumi na kijamii iliongozwa na ubaguzi.

Wazungu waliendeleza ubaguzi kazini dhidi ya Waafrika kwa misingi ya rangi. Ajira ya malipo duni ilipewa Waafrika waliozalisha mali zaidi kwa manufaa ya Wazungu wa tabaka la juu.  Utabaka kwa misingi ya kiuchumi ulikithiri baina ya wazungu wa tabaka la juu na Waafrika wanyonge wa tabaka la chini. Hali hii ilichangia maisha duni walioishi Waafrika kutokana na dhuluma walizopitia kutoka kwa watawala wao.

Katika riwaya ya *Mkamandume*, mwandishi anaeleza namna Waafrika walidhulumiwa na wazungu kutoka tabaka tawala. Kupitia kwa mazungumzo kati ya Soud na Nadia tunafahamu namna wazungu walivyowadhulumu waafrika. Soud anaeleza kwamba:

> *Afrika au waafrika ni maskini na hawajafanya maendeleo ya maana kwa sababu wamenyonywa kwa muda mrefu na wanaendelea kunyonywa* (uk 149).

Kahara (2011) anadai kuwa ukoloni uliwafanya Waafrika kupoteza uhuru wao, mashamba yao na kuathiri mifumo yao ya kiuchumi. Mwishowe, Mwafrika anajikuta amejikita katika mfumo wa kibepari ambapo alijikuta kama skwota katika mashamba ya walowezi. Katika mfumo huo, alijikuta ni mzalishaji mali tu na hakuwa na udhibiti wowote wa njia za kuzalisha mali yenyewe.

Mali ambayo inazalishwa na Waafrika inatumiwa tu kuwafaidi wazungu pekee ilhali Waafrika wanaendelea kuishi katika hali duni. Wazungu walikuwa na mtazamo finyu kuhusu Waafrika. Rangi nyeusi ya ngozi ya Waafrika pamoja na utamaduni wao ulichochea wazungu kuwabagua kwa kuwaona kuwa watu duni zaidi. Nchi za Afrika zilisawiriwa kama nchi za jehanamu kwa wazungu waliojiona bora zaidi. Iliaminiwa kuwa Waafrika wanaishi motoni kuliko na mateso mengi.

Utengano wa kitabaka ulikuwepo baina ya maisha ya wazungu na waafrika ambao walikuwa wa tabaka la chini. Hali hii iliibuka kutokana na walio wachache kumiliki nyenzo zote za uzalishaji mali huku walio wengi hawakuwa na chochote isipokuwa nguvu zao walizozitumia kufanya kazi ili walipwe mishahara midogo ya kuyakimu maisha yao.

Nadharia ya uhakiki wa ki-Marx inasisitiza kuwa historia ya binadamu inaweza kuelezeka kwa misingi yakinifu ya kiuchumi ambayo huchunguza njia ya uzalishaji mali pamoja na miundo ya kiuchumi. Wakati wa ukoloni, Waafrika waliishi katika hali ya uchochole. Hali hii iliwasababishia watu wengi kutamani kujinasua kutokana na hali hii ili kuwa na maisha

bora kama vile mabwana zao walivyokuwa wakiishi. Kinyume na matarajio, baada ya mageuzi tunaona kuwa hali ambayo Waafrika walikuwa wakitarajia imekuwa mbaya zaidi. Raia wa Malelejimema walikuwa wamekumbwa na umaskini usio kifani. Mwandishi anasema kuwa:

> *Hapo awali, Mkamandume aliishi katika hali ya umaskini na alijaa na tamaa ya kutoka katika hali hiyo siku moja. Hali ya umaskini ndiyo ilimsababishia kumsikiliza msemaji na kuamini kila alichosikia au kufikiria (uk 18).*

Kilimo ambacho ndicho tegemeo la watu wengi katika Malelejimema kinaanza kuangamia polepole na baada ya kipindi fulani, kunashuhudiwa ukosefu wa chakula kabisa. Mazao yanayopatikana kwa wale wakulima waliofanikiwa ni machache. Hali hii inasababisha kuwepo kwa visa vingi vya wizi. Wananchi wanaoshiriki wizi huu wanahatarisha maisha yao kwani wengi wao wanapigwa kibao ama kuuawa. Mwandishi anatuchorea picha halisi ya umaskini katika Malelejimema. Taswira ya wakulima ambao wanasalia kuwa magofu inamtisha Mkamandume. Anashangaa wanakoenda wakulima hawa huku wakiwa wamebeba majembe ilhali hakukuwa na mazao makondeni tena. Wana wa wakulima hawa wanaongozwa na vitumbo vya utapiamlo. Wana hawa walionekana wakiwa wanyonge mno. Aidha, watoto waliompita Mkamandume wakienda shuleni walikuwa wameinamisha vichwa vyao ambavyo vilionekana kuwa vikubwa kuliko miili yao. Wengi miongoni mwao walikuwa wameondoka makwao bila hata ya kiamsha kinywa. Huko shuleni hakukuwa na masomo kwa sababu ya ukosefu wa vitabu vya kusomea, madaftari, penseli na kalamu za kuandikia.

Hali hii ya umaskini inaendelea kukuzwa na baadhi ya Waafrika. Hali kama hii hutokea pale ambapo wakoloni huendelea kuwanyonya Waafrika wakisaidiwa na Waafrika wengine kwa sababu zao za kibinafsi. Waafrika waliochukua hatamu ya uongozi kutoka kwa mkoloni waliendeleza mbinu zile zile zilizokuwa za kibepari. Wakiongozwa na ubinafsi na tamaa, walianza kujinyakulia kila raslimali ili kuyakidhi mahitaji yao. Soud anaeleza kuwa:

> *Afrika, au waafrika ni maskini na hawajafanya maendeleo ya maana kwa sababu wamenyonywa kwa muda mrefu na wanaendelea kunyonywa. Na kwa bahati mbaya baadhi yetu tunaendeleza unyonyaji huo kwa maslahi yetu (uk 149).*

Hali si hali tena kwa wanamalelejimema. Vile visenti walivyokuwa wakivipata hapo awali haviko tena. Ukulima uliokuwa tegemeo la wengi sasa unaendelea kuzikwa katika kaburi la sahau. Hali kama hii inasababisha uchungu miongoni mwa wahasiriwa ambao wameshakuwa mabaradhuli. Hali za wengi zimekuwa sasa kupita kwa watu huku wakiomba chumvi na sukari. Linalowauma zaidi ni kuomba kwa watu ambao hawakushiriki katika mapinduzi ya kumwondoa mkoloni. Hali kama hii inawaumiza sana wale walioshiriki kwa vyovyote vile katika mapinduzi wakitarajia kupata nafuu baada ya mkoloni kuondoka. Kinyume na matarajio, wale wavivu wasiofanya chochote ndio wanaotamba kwa kutumia jasho la wengine.

Kupitia kwa mbinu rejeshi, mzee Mkasi anakumbuka namna alivyodhulumiwa katika vita vya Wazungu. Anadai kuwa alishurutishwa kwenda kupigana katika vita visivyomhusu yeye. Anakumbuka namna chatu alivyomvamia akamzongazonga ili kumvunja mbavu na

kutaka kummeza lakini akajiokoa kutokana na nguvu zake za ujana. Mwandishi anasimulia kuwa:

> *… mara nyingi mzee Mkasi kumbukizi za vita zilimletea kumbukumbu za mambo yaliyojaa uadui kuchukuliwa kwa nguvu vitani, vita visivyomhusu ndewe wala sikio* (uk 179).

Katika vita vya ukombozi, mzee Mkasi alidhulumiwa kutokana na msimamo wake. Alishiriki katika mapinduzi ya nchi kwa sababu alitaka sana nchi yake ipate ukombozi, iendeshwe na watu wake wenyewe. Hali hii ilimsababishia masaibu mengi. Anaeleza kuwa alichukuliwa kama gunia la makaa na kuwekwa kizuizini. Alisingiziwa kuwa ameitukana bendera na kula njama ya kuleta mafuriko nchini. Anasimulia kuwa:

> … *baada ya hapo nilikamatwa nikaambiwa nimeshiriki katika magendo ya karafuu. Adhabu yake ni kifo. Sikuuliwa. Niliachwa baada ya mateso mabaya (uk 187).*

Kristian (2006) anadai kuwa, katika nchi ya Afrika Kusini, utumwa katika enzi ya ukoloni ulichangia pakubwa kuibuka kwa jamii iliyojiweka katika misingi ya ubaguzi wa rangi. Jambo hili la kuwapa Waafrika kazi kwa mishahara duni halikudumu Afrika Kusini pekee, bali katika takriban nchi zote zilizotawaliwa kimabavu, zikiwemo nchi za Afrika Mashariki na ulimwengu mzima kwa jumla. Hili ni jambo lililochangia pakubwa katika kubaguana kwa rangi na kitabaka katika nchi zote zilizohusika ulimwenguni.

Mkamandume anakumbuka wakati wenyeji wa Malelejimema walinyang’anywa ardhi na baadhi ya wageni. Walilazimishwa pia kulipia kodi viwanja ambavyo havikuwa vyao. Mwandishi anaeleza kuwa:

*Makazi ya wenyeji yalisokomezwa ng'ambo na zaidi hadi mashamba kaskazini, kusini, mashariki na magharibi. Na hata huko iliwabidi walipie kodi za viwanja vilikuwa si vyao (uk 397).*

Katika riwaya ya *Mkamandume* ubaguzi unajitokeza baina ya mwajiri na wafanyakazi. Japo waliishi katika eneo moja, waajiri wao hawakuwaruhusu kuhusiana na jamaa zao kwa misingi ya rangi. Soud akiwa mdogo alienda kinyume na masharti ya wazazi wake na mara kwa mara alijipata akihusiana nao. Jambo hili halikuwafurahisha wazazi wake. Walimwonya dhidi ya kushirikiana na watu maskini. Hata hivyo, Soud hakuona sababu ya kunyimwa uhuru wa kucheza na watoto wenzake hivyo basi alikaidi amri ya wazazi wake na mara kwa mara aliadhibiwa kwa kutofuata amri. Soud anadai kuwa:

*Siku zote nilikatazwa kucheza na watoto wa kimaskini, lakini sikusikia. Kwangu mchezo haukuwa na utajiri wala umaskini. Nilikatazwa kuingiliana na watu wazima hasa waliotoka bara lakini mimi nilihusudu suhuba zao (uk 140).*

Ngugi wa Thiong'o (1982) katika riwaya ya *Shetani Msalabani* anasimulia historia ya Wariinga inayofichua dhuluma walizofanyiwa Waafrika wakati wa ukoloni. Mwandishi anaeleza kuwa:

*Walipoona ya kuwa walikuwa karibu kushindwa na mashujaa wa Mau Mau walianza kuwanyanyasa na kuwadhulumu wafanyakazi na wakulima wadogo vibaya sana humu nchini (uk 145).*

Wazazi wa Wariinga walishikwa na kutiwa gerezani na walipotolewa mwaka wa 1960 walipata shamba lao limenyakuliwa na kuuziwa wasaliti wa serikali ya kikoloni. Hali hii iliwasababisha kuishi maisha duni ya uchochole.

Katika riwaya ya *Shetani Msalabani* (1982) mhusika Mwireri wa Mukiraai anapinga wizi na unyang'anyi wa kimataifa kwa sababu wazungu wa tabaka la juu wanadhulumu waafrika wa tabaka la chini kwa kujinufaisha na mali inayozalishwa na Waafrika katika nchi za Afrika. Ushahidi unajitokeza anaposema kwamba:

> *Wananchi wakapanda wachache, walio na talanta wakaja wakavuna, wananchi wakapanda jasho na damu, walio na talanta wakaja wakagawanya mazao yatakayopatikana. Matajiri watano wakapachika mirija yao katika damu na majasho ya wafanyakazi hamsini (177).*

Wangari aliwasimulia abiria wenzake wakielekea Ilmorog kuhusu alivyoshirikiana na kundi la Mau Mau kupinga dhuluma na ukatili. Anasema kuwa:

> *Ushirikiano wa wasaliti na wabeberu ulikuwa wa kinyama kwani haukujali utu. Haukujali watoto wasiojiweza (uk 37).*

Kutokana na mazungumzo kati ya Mwireri wa Mukiraai na abiria wenzake suala la dhuluma dhidi ya Mwafrika linabainika wazi. Aliwafahamisha kuwa karamu ya wezi iliandaliwa na Shirika la wezi na wanyang'anyi kusherehekea ziara ya wezi na wanyang'anyi wa Amerika na nchi za ulaya ya Magharibi hasa Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, ltalia, Sweden na Ujapani yaani *lnternational Thieves and Robbers Ltd*. Anadai kuwa:

> *Hakuna ustaarabu wowote duniani ambao haukujengwa kwa kufuata misingi hii ya wizi na unyang'anyi. Amerika hii leo ingekuwa wapi kama si wizi? Na Uingereza na Ujapani, Ujerumani na Ufaransa? Nchi zote za Ulaya ya magharibi zimestawi kwa sababu ya wizi na unyang'anyi? (uk 81).*

Kubaguliwa kwa misingi ya rangi kumechangia pakubwa utengano baina ya makundi ya wazungu na Waafrika. Wazungu katika tabaka tawala wanawadhulumu Waafrika walio katika tabaka tawaliwa kwa misingi ya rangi na hali duni ya maisha.

### 2.5 Kudhulumiwa Kisaikolojia

Dhuluma hii imewaathiri wahusika wengi wa tabaka la chini kutokana na matendo ya kikatili waliyotendewa na wahusika wa tabaka nyonyaji. Hali hii imechangia migogoro ya kimawazo miongoni mwa wahusika wanyonge. Scott, G. (2020) anaeleza kuwa, migogoro ya kisaikolojia ni mivutano au mikinzano inayojitokeza akilini mwa mhusika mmoja au mawazo ya wahusika mbalimbali yanayotofautiana.

Katika riwaya ya *Mkamandume*, mhusika mkuu ambaye ni Mkamandume anakumbwa na migogoro ya kimawazo kutokana na uhuru wa nchi yake. Mkamandume alifyeka vichwa vya watu wote waliodhaniwa kupinga harakati zao za kupigania uhuru. Mawazo yake yanazozana iwapo ataweza kumuua Bw. Shombo au la kwani siye Mkamandume wa zamani. Hatimaye sauti inayomhimiza kwenda kumuua Shombo inashinda na kumfanya amfyeke Shombo kichwa. Mwandishi anasema kuwa:

> *Kama kufumba na kufumbua, Mkamandume aliruka kwa nguvu za ajabu na kwa dhoruba moja la panga alimkata kichwa Bw. Shombo. Bw. Shombo hakuwahi hata kutoa ukwenzi wa maumivu au kutetea roho yake (uk 402).*

Mkamandume anajutia maovu aliyomtendea mzee Mkasi. Nafsi yake inazua mjadala wa kumsuta kwa matendo ya dhuluma aliyomtendea mzee Mkasi. Hali hii inamkabili vilivyo alipokuwa akienda kukopesha pesa kwa mzee Mkasi ya kukidhi mahitaji yake. Pia anajipata katika hali hii ya majuto baada ya kufyeka shamba lao la mihogo. Nafsi yake inamsuta:

> *Kitu gani umefanya Mkamandume? Umetatua tatizo kwa kulitatiza tatizo? Kumesaidia nini kufyeka kila kitu kondeni mwako? Umezidi kuikata tamaa yako (uk 21).*

Kupitia mbinu rejeshi, Mkamandume anakumbuka namna mzee Mwemedi alivyokuwa akimweleza. Alieleza kuwa watu walionufaika si wale waliopigania uhuru. Alimkashifu Mkamandume kwa kujitolea mhanga kuikomboa nchi ya Malelejimema. Alieleza kuwa:

> … *sasa ndugu zetu wenyewe ndio wanaochukua mapanga yasiyoonekana kutukeketa* (uk 366).

Soud na Time katika riwaya ya *Mkamandume* wanadhulumiwa kisaikolojia na Mkamandume anapokataa posa ya Soud baada ya wawili hao kuchumbiana. Hali hii ilitokana na ugomvi wa asili kati ya Mkamandume na wazazi wa Soud. Time bintiye Mkamandume alikerwa sana na kitendo hiki cha kulipiza kisasi kwa kizazi kipya ambacho hakikuhusika kamwe. Msimulizi anaeleza kuwa:

> *Alimwazia babake na kusaili kimya kimya kwa nini aliongozwa na chuki katika posa za Soud? Kwa nini alimkataa Soud?' Kukataliwa kwa posa kulisababisha machungu na masikitiko miongoni mwa wapenzi hawa wawili. 'Soud aliathirika na hali hii kimaisha. Na labda kukataliwa posa zake kusingelikuwa kiroja lakini kukataliwa kwa uhasama wa tokea enzi na azali na tena uambatane na asili ya rangi na damu za watu (uk 92).*

Mgogoro wa kimawazo unatokea akilini mwa Time walipokuwa wameenda kutembea na Nadia kwenye msitu. Alizozana na kujiuliza kwa nini alimchukia na kumwonea wivu Nadia. Migogoro ya kimawazo ilimfanya kubaini kwamba Malelejimema kulikuwa na matabaka mawili makuu ya walalahoi na walalaheri. Anajiuliza kuwa:

> *Kwa nini kijiji kile kimekuwa na vibanda na vijumbe vile karne zote zile? Kwa nini nyumba mbili tatu tu ndizo zilizokuwa na maana ya nyumba? (uk 196).*

Mhusika Soud alipatwa na mgogoro wa kimawazo kutokana na dhuluma walizotendewa wafanyakazi wao akiwa mchanga. Mawazo yake yalikinzana na mawazo ya babake. Hakupendezwa na jinsi wazazi wake walivyowakandamiza wafanyakazi wao. Soud aliwachukulia akina Msafiri, Mpikachai na Maliyatabu kama binadamu waliostahili kutendewa wema na kuheshimiwa. Mawazo yake yalitofautiana kabisa na yale ya babake aliyeamini kwamba wafanyakazi hawakustahili kupewa heshima zozote. Mwandishi anasema kuwa:

> *Lakini Soud aliyapuuza yote hayo. Alihisi hiyo ilikuwa njia ya pekee kugomea kitu kisicho halali kinachotendwa na ukoo wake (uk 219).*

Mhusika Nadia katika riwaya ya *Mkamandume* anachangia migogoro ya kisaikolojia akilini mwa Time na Soud. Mgogoro huu unatokana na suala la mapenzi ambalo linawavutia Time na Nadia kwa Soud. Hali hii inajitokeza wazi wakati wa mazungumzo kati yake na Time. Anaficha siri ya uchumba wao na Soud kwa kuwa alishuku kwamba Time pia anampenda Soud. Anawaza kuwa:

> *Toba! Nani huyo Mungu wangu! Moyo wa Nadia ulimgutuka… Kweli au uongo…vipi miaka yote aliyoishi hapa asijue kwamba Time anampenda kijana mwenyeji wa pale (uk 360).*

Vilevile, katika riwaya ya *Shetani Msalabani* baadhi ya wahusika wanadhulumiwa kisaikolojia. Wariinga anakumbuka historia yake iliyo na machungu yaliyosababishwa na ukatili aliotendewa na tajiri wa Ngorika baada ya wazazi wake kutiwa gerezani. Mwandishi anasimulia kuwa:

> *Katika mwaka wa elfu moja mia tisa na hamsini na nane, babaye Wariinga, alikamatwa na kupelekwa katika kambi ya Manyani; mwaka mmoja baadaye mamaye akashikwa na kutokomezwa katika magereza ya Lang'ata na Kamiti (uk 145).*

Hali hii ilimwathiri kisaikolojia na kila mara alipowazia alipatwa na msongo wa mawazo. Wariinga alilazimika kuenda kuishi na shangaziye Nakuru. Mjomba wake alikuwa miongoni wa waliotumikia wazungu ili wanusuru nafsi zao. Baada ya uhuru, wenzake walibahatika kujinyakulia mashamba makubwa na mabiashara ya unyonyaji lakini yeye hakupata bahati ya kupata mali kwa urahisi

Hali ya uchochole ilimtatiza sana mjomba wake Wariinga kimawazo. Kila mara aliwaza na kuwazua kuhusu maisha magumu walioishi na utengano uliokuwepo baina yao na matajiri wa tabaka la juu. Alilazimika kutangamana na watu wa tabaka la juu kuliko yake ili kujinufaisha. Mwandishi anasema kuwa:

> *Yeye alifuatana na matajiri wawili, mmoja wa kutoka Njoro na mwingine wa Ngoriga. Matajiri hao walikunywa pombe katika Sportsman's corner katika hoteli ya Stags Head na katika vilabu vingi vya wazungu, ambamo hapo mbeleni, mwafrika asingedhubutu kuingia –kama Rift Valley Sports Club* (uk 149).

Tajiri wa Ngorika alimdhulumu kimapenzi Wariinga. Kutokana na utajiri wake alimshawishi Wariinga kwa kutumia pesa ili wafanye mapenzi naye na mwishowe akampachika mimba. Jambo hili lilimshtua sana Wariinga kwa kuwa alikuwa bado ni mwanafunzi wa shule ya upili. Alikumbuka namna tajiri huyo alivyokuwa aamemwahidi kuwa atamwoa awe mke wa pili au amtaliki mkewe wa kwanza wafunge ndoa kanisani naye. Baada ya kuamua kumweleza tajiri huyo kuhusu uja uzito, alikerwa sana. Tajiri alijitenga na mimba hiyo kwa kumwambia kwamba:

> *Kwa nini hukujihadhari kama wasichana wengine? Kwa nini hukumeza pills au kutiwa coil, au kudungwa sindano? Kwa nini hukuniambia tu ulipong'amua tu mambo yamekuwa hivyo?* (uk 154).

Hali hii ilibadili mkondo wa maisha yake. Aliwazia mambo mengi akajaribu kuavya mimba hiyo lakini haikuwezekana. Mwishowe, alijaribu kujiua lakini akaokolewa na msamaria mwema.

## 2.6 Ukiukaji wa Haki za Binadamu

Kwa mujibu wa Kamusi Kuu ya Kiswahili (2015) haki ni kitu au jambo ambalo mtu anastahili kupata. Pia, ni utendaji, ufuataji na utumiaji wa sheria na kanuni katika kutimiza jambo. Kila mwananchi ana haki na sharti serikali iheshimu na ilinde haki za wanajamii bila ubaguzi wowote wa kitabaka.

Azimio la Haki za Binadamu (1948) linaeleza kuwa haki za binadamu ni misingi ya maadili inayotakiwa kutumika kwa manufaa ya binadamu wote duniani na kwa usawa. Watu wote wamezaliwa huru na wana hadhi na haki sawa. Sharti haki ya kila mmoja izingatiwe kwa usawa bila mapendeleo yoyote ya kitabaka, kiuchumi, jinsia, rangi, taifa, hadhi, cheo, kabila, siasa na dini. Wanajamii wote wana haki mbalimbali kama vile; haki ya kuishi, kuabudu, kutangamana na wengine, kupata mahitaji ya kimsingi na kadhalika.

Katika riwaya za *Mkamandume* na *Shetani Msalabani* haki za wahusika wengi zimepuuzwa. Tabaka nyonyaji limeendeleza dhuluma dhidi ya wanyonge wa tabaka nyonywaji. Sehemu hii imeshughulikia dhuluma dhidi ya watoto, wafungwa na wapiga kura. Dhuluma hizi zimetokana na kupuuzwa kwa haki zao za kimsingi,

### 2.6.1 Dhuluma dhidi ya watoto

Serikali ina wajibu wa kutambua, kuheshimu na kulinda haki za binadamu ili kuiendeleza jamii. Ni jukumu la wazazi, familia na serikali kuwalea, kuwalinda na kuwaenzi watoto katika jamii. Watoto wana haki ya kupewa mahitaji ya kimsingi kama binadamu wengine.

Sheria za Watoto (2001) inaeleza kuwa, mtoto ana haki na anafaa kulindwa na kupewa malezi bora kuanzia utotoni hadi awe mtu mzima, anapotimiza miaka kumi na minane. Wazazi, walezi, jamii na serikali kwa jumla wana wajibu wa kuhakikisha kwamba haki za

mtoto zimelindwa ipasavyo. Mtoto ana haki ya kuishi, kuelimishwa, kupata mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, makazi na mavazi.

Kavuria (2008) anadai kwamba watoto huwa mikononi mwa watu wanaowaamini kama wazazi, jamaa na majirani na wanapotendewa maovu hawawezi kujitetea ama kupinga maonevu hayo. Baadhi ya watu hao waliopewa jukumu la kuwatunza watoto hutekeleza dhuluma hizi labda bila kujua, wakishikilia kufuata kanuni fulani za kitamaduni au za kidini.

Katika riwaya ya *Shetani Msalabani (*1982) wazazi wa Wariinga wanashikwa na kutiwa gerezani. Wariinga alikuwa na umri mdogo na hangeweza kujikimu kimaisha. Mwandishi anasema kuwa:

> *Wariinga alikuwa na umri wa miaka miwili. Shangazi yake aliyekuwa ameolewa huko Nakuru akamchukua na kumlea* (uk 145).

Hali hii inachangia masaibu mengi yanayomkumba Wariinga na hata kubadilisha mkondo wa maisha yake. Anatatizika kimawazo na walezi wake waliokuwa wakimlea wanakosa kumwelekeza ipasavyo.

Tajiri wa Ngorika anakiuka haki za Wariinga kwa kumpachika mimba ilhali alikuwa bado ni mwanafunzi katika shule ya upili. Baada ya kumpachika mimba anamwacha na mzigo wa kulea mimba. Anajitetea kwa kumwambia kuwa:

> *Kwa nini ukashika mimba upesi namna hiyo ulipoanza kutembea na mimi? Basi nenda zako ukamtafute huyo mvulana aliyekutia mimba umwambie akuoe au mwende mkaiharibu mimba hiyo huko kichakani au popote mtakapo* (uk 154).

Tajiri huyu licha ya kuwa mzee hakujali kushiriki mapenzi na msichana wa umri mdogo kwa kuwa alijua ana utajiri mkubwa.

Vilvile, katika riwaya ya *Mkamandume* (1982) haki za Viwe zinakiukwa anapopachikwa mimba akiwa mchanga na Bete. Anaachiwa mzigo wa kulea mimba hiyo hali inayomsababishia dhuluma kimaisha. Kulingana na jamii yao mwanamke aliyeolewa tu ndiye aliyestahili kuwa mjamzito. Viwe alikumbwa na wasiwasi kwa kuwa aliogopa wanajamii pamoja na babake. Mwandishi anasema kuwa:

> *... lakini leo mimba imekuwa mzigo kwa Viwe. lmekuwa balaa, na kwa hivyo lazima aifiche au aiharibu ikiwezekana* (uk 99).

Hali hii inamlazimu Bi. Tufaa, mamake Viwe kumwendea Bi. Reja, shoga yake ili waweze kuiavya mimba ile. Bi. Reja anamhakikishia Bi Tufaa kuwa:

> *Basi Viwe tutamchukua kwa kisingizio cha kumchezea unyago, lakini lengo letu ni kumtoa mimba kwa madawa ya kienyeji na fundi wa hayo n'naye hapa mikononi (uk 103).*

Mkamandume alipogundua kuwa bintiye alikuwa mjamzito alimpiga kikatili bila kujali umri na hali yake. Alishikwa na hasira za mkizi. Hakutaka kujua aliyempachika mimba hiyo bali alimrukia tu na kuanza kumwadhibu. Msimulizi anadai kuwa:

> *Mkamandume hakujibu kitu, alimvuta Viwe akamzaba kibao kikali. Huyo Viwe akaanguka chini kisha akamkamata Viwe na kumtupa chini. Akamwinamia kumkaba shingo (uk 112).*

Mamake na dadake Viwe walijaribu kumwokoa lakini hawakuweza. Walilazimika kupiga mayoye na majirani wakaja lakini wao pia wakashindwa.

> *… hata walipokuja majirani, kike kwa kiume, mwele aliyekuwa akielemewa na babake alikuwa akitoka kipovu kinywani. Time alikuwa akivuja damu puani na Bi Tufaa kavimba na kufusika vibaya vibaya usoni. Ilihitaji wanaume sita wenye nguvu zao kuweza kumng'ang'anua Mkamandume (uk.112).*

Kupitia kwa mawazo ya Soud tunabaini kwamba babake alikiuka haki za watoto kwa kuwaajiri na kuwatesa sana. Aliwafanyisha kazi kama punda. Anasema kuwa:

> *... mara kinda okota kuni. Kachote maji kisimani. Kachume mashelisheli shambani. Kangoe muhogo, kinda osha vyombo. Kachume mafenesi uuze halafu kaanike karafuu uwanjani, Mradi Kinda, Kinda, Kinda…Na aliposita kofi, alipozubaa kibao, alipokosea fimbo (uk 221).*

Kupuuzwa kwa haki za watoto kunachangia dhuluma ambazo huwaathiri pakubwa maishani.

### 2.6.2 Kudhulumiwa kwa Wapiga Kura

Katiba mpya ya Kenya (2010) inadai kuwa ni haki ya kila mwananchi kuteua viongozi wanaofaa bila kushurutishwa. Tume ya uchaguzi yafaa kuandaa uchaguzi ulio wa haki na usawa katika nafasi mbalimbali za uongozi.

Kulingana na Sheria za Kimataifa (1996) wapiga kura kote duniani wana haki ya kushiriki katika uchaguzi ulio huru na haki. Serikali pamoja na Tume ya Uchaguzi sharti izingatie haki zote za wapiga kura wakati wa uchaguzi.

Katika riwaya ya *Shetani Msalabani* viongozi wengi wa kisiasa wanapuuza haki za wapiga kura wakati wa uchaguzi. Kihaahu wa Gatheeca alipokuwa anawania kiti cha ubunge, alitenda matendo ya dhuluma wakati wa uchaguzi. Aliajiri wahuni, mabarubaru ambao kazi yao ilikuwa ni kuharibu mali ya wapinzani wake. Anadai kuwa:

> *Niliwaamuru wawachape bastola na kuwaambia wachague baina ya uhai na kifo. Wale waliokataa kusalimu amri waliuawa* (uk 112).

Wengine ambao walikataa kusalimu amri walipigwa na kujeruhiwa vibaya. Anaeleza kuwa:

> *Nikawaamuru wahuni wangu waende kwake wamvunje mguu, nao wakalitekeleza hilo (uk 112).*

Matendo haya ya kikatili yanakiuka haki za wapiga kura ambapo mgombea mmoja mwenye uwezo wa kiuchumi anawazuia wapinzani wake walio na umaarufu wa kisiasa kuwania uongozi. Wananchi wanajipata katika njia panda kwa kuwa wanashurutishwa kumteua kiongozi ambaye hawamtaki.

Kila mwananchi ana haki ya kuhudumiwa na viongozi waliochaguliwa. Viongozi katika Malelejimema wanaegemea upande mmoja wa tabaka la juu na kuwasahau wananchi wa tabaka la chini. Raslimali za nchi zinawanufaisha matajiri pekee ilhali maskini wanataabika kwa kukosa miundo misingi na mahitaji ya kimsingi. Hali hii inadhihirika katika sehemu za mjini ambako ndiko huishi viongozi au watawala, huko ndiko kuna maendeleo ya kijamii na kiuchumi ambapo watu wenye kipato cha juu huishi, lakini tabaka tawaliwa ambalo wengi wao wanaishi vijijini limeonyeshwa kutopewa huduma muhimu za kijamii.

Kupitia kwa mawazo ya Soud tunapata picha halisi ya namna uchumi ulivyozoroteka kutokana na kutowajibika kwa viongozi waliochaguliwa na wapiga kura:

> *Tazama mapato ya forodha sasa, bandari na viwanja vya ndege…mapato ya posta na simu, tazama misaada na kikopo, nafasi za elimu ya juu, tazama balozi zinavyokimbia Malelejimema… zamani Malelejimema iliongoza kwa hayo yote na sasa imekuwa ukurutu mtupu (uk 240).*

Mashamba yaliyonyakuliwa kutoka kwa wageni hayakuwafaa wananchi wa kawaida kwa vyovyote. Yale yaliyokuwa na rotuba nzuri yalinyakuliwa na viongozi ambao hawakuyatunza jinsi ilivyostahili. Mwandishi anasema kuwa:

> *... mashamba yote yameota magugu, minazi imeparama. Mikarafuu imesibiwa na maradhi yasiyopata kusikika. (uk 35*).

Kwa upande mwingine, wananchi wamekosa ardhi ya kulima. Licha ya kukosa ardhi, vile vishamba vidogo walivyo navyo haviwezi kutoa mazao yoyote kwa sababu ya kukosa rutuba na kutokana na magonjwa ambayo hayana dawa.

Serikali iliyochukua hatamu haikuwa na ruwaza ya jinsi ya kuiendesha miji. Matokeo yakawa uchafu uliotapakaa kokote huku barabara zikijaa mashimo. Majumba ambayo hapo awali yalikuwa yakivutia sasa yamechoka na hayana wa kuyashughulikia tena. Mengine yalikuwa yameporomoka na kuwaua watu lakini ajabu ni kuwa ndani mwa yale majumba yanayoonyesha ishara za kuporomoka wakati wowote bado mna watu walioishi humo. Si eti walipenda ila hawana pahala pengine pa kwenda. Maanake serikali haijawajibika kuwajengea wananchi nyumba nyingine za kuishi ila wananchi bado wanategemea nyumba zilizoachwa na wakoloni.

Viongozi walitumia propaganda za kisiasa ili wananchi wasigundue mbinu zao mpya za dhuluma. Mojawapo wa mbinu hizi ilikuwa kuwahimiza wananchi kufanya kazi ya kujitolea ili kuharakisha maendeleo. Huu wito ulikuwa mzuri ila dosari lilitokea pale ambapo wananchi wanatiwa ndani na kushtakiwa kwa kukataa kufanya kazi ya kujitolea. Kutokana na jina, kazi hii ni kazi ya hiari wala si kazi ya lazima. Mzee Mkasi alishikwa na kushitakiwa kwa kukataa kushiriki katika kazi ya kujitolea.

Wananchi walinyimwa haki yao kutokana na kutowajibika kazini. Viongozi ambao wamepewa wajibu wa kuwa kielelezo kwa wananchi wanaenda kinyume na kaida na kusababisha umaskini wa hali ya juu. Kiongozi anafaa kuyaweka maslahi ya nchi mbele wala hafai kujinyakulia mali kwa haraka bila ya kujali maslahi ya wananchi. Boss wa Mkamandume anawasili kazini baada ya saa nne asubuhi badala ya kuwasili saa mbili asubuhi ambayo ndiyo saa anafaa kuwasili kazini. Licha ya kufika kazini kama amechelewa, anaharakisha kuondoka ofisini

Serikali inamkandamiza mwananchi kwa kukosa kutekeleza majukumu yake. Mambo ya kimsingi kama vile matibabu yametelekezwa. Wagonjwa hawana hospitali za kwenda wala hakuna dawa. Wagonjwa wengi wanajifilia bure kutokana na magonjwa ambayo pengine yangepata dawa yangetibika. Mkamandume anapolazwa katika hospitali kwa muda wa siku ishirini na moja, anaona tofauti kubwa kati ya hospitali ya hapo awali na hospitali ya wakati huu ambapo mkoloni ameshaondoka. Wakati wa ukoloni hospitali ilikuwa safi na pia wauguzi walikuwa na matunzo mema.

Dawa zilikuwa zikiwatafuta wagonjwa, kulikuwa na chakula nadhifu kilichorutubisha miili ili kurudisha siha kwa wagonjwa. Aidha kulikuwa na vitanda, magodoro, mito, mabetishiti, foronya na vyandarua safi. Wakati Mkamandume anapolazwa, tofauti iliyopo ni kama

ardhi na mbingu. Wakati huu hakuna dawa, hakuna madaktari na hata malazi. Jambo hili linamuumiza Mkamandume anapokumbuka kuwa hiki ni mojawapo wa vitu alivyopigania ili vitoke kwa mikono ya mkoloni. Aidha uongozi mbaya umesababisha mazingira kuharibika.

Kulingana na mwandishi, wakati wa ukoloni, mazingira yalikuwa nadhifu na ya kuvutia. Machaka yalikuwa yameenea sana. Kupitia kwa kumbukizi za Mkamandume anasema kuwa:

> *Hali sasa imebadilika, misitu na machaka yamefyekwa ili kutoa nafasi ya nyumba kujengwa katika kila nafasi iliyopo. Hakuna matunda yaliyozaliwa kwa sababu mimea mizazi haipo tena. Watu hawaendi tena kuteka maji kisimani kwani kisima kimeharibiwa na hali mpya ya mazingira (uk 136).*

Dhuluma dhidi ya wapiga kura inatokana na kupuuzwa kwa haki zao na viongozi waliochaguliwa. Ubinafsi, tamaa na ufisadi unachangia maisha ya uchochole ya wananchi wengi wa tabaka la chini.

### 2.6.3 Dhuluma dhidi ya Wafungwa

Katiba ya Kenya (2010) inafafanua kwa kina haki zote za wafungwa na washukiwa. Wafungwa wana haki ya kuelezwa sababu yao ya kushikwa na pia kupewa fursa ya kujitetea wakiwa kortini. Licha ya hayo, wanastahili kupewa mahitaji ya msingi kama vile chakula, makazi na mavazi. Ngugi wa Thiong'o (1982) katika riwaya ya *Shetani Msalabani* anaeleza namna haki za Wangare zilivyopuuzwa alipofika mjini kung'ang'ana kutafuta kazi. Alikuwa tayari kufanya kazi yoyote atakayoipata hata ikiwa ya kufagia afisi

au vyoo. Kwa bahati mbaya alishikwa na kutiwa ndani kwa kushukiwa kuwa mwizi akiwa katika harakati ya kutafuta kazi. Anasimulia kuwa:

> *Moja kwa moja nilisukumwa ndani ya gari la polisi. Nilipelekwa kwenye kituo cha polisi nikatiwa katika kitundu (uk 41).*

Mazingira ya humo gerezani hayakuwa ya kupendeza. Wafungwa walitatizika sana. Wangari anasimulia kuwa:

> *Humo kitunduni mlikuwa ni makao makuu ya chawa, kunguni, mbu na viroboto. Huwezi kupata hata lepe la usingizi! Nilikaa huko kwa siku tatu: mimi Wangari ambaye sijamwibia mtu hata kiazi kimoja, nililala kwa siku tatu katika kituo cha polisi kitunduni mlimojaa kinyesi na mkojo (uk 41).*

Baada ya kufungiwa kitunduni kwa siku tatu alipelekwa mahakamani na kushtakiwa kwa mambo mawili; kudhaniwa wizi na uhuni. Kutokana na haya makosa alitozwa faini ya shilingi mia mbili kwa kuzurura mjini bila kibali. Hii inakiuka haki zake kwa kuwa hakufanya kosa lolote la kushikwa, kutiwa ndani na kutozwa faini.

Mzee Mkasi alimsimulia Time namna alivyodhulumiwa na polisi wakati wa vita vya ukombozi katika nchi ya Malelejimema. Alishikwa na kuwekwa kizuizini bila hatia yoyote. Alisingiziwa kwamba alishiriki katika njama ya kuleta vita nchini. Kule kizuizini aliteswa sana kwa kupigwa na hata kujeruhiwa. Licha ya miaka mingi kupita mateso haya yalisalia katika kumbukumbu zake.

Bwana Sleyyum pia anamwelezea Soud namna haki zake zilivyokiukwa wakati wa vita vya ukombozi. Alikumbwa na dhuluma alipotaka kujua sababu ya kuuawa kwa bwana Aziz na Bi. Mahfoudha. Aliwekwa gerezani akateswa na kuumizwa vibaya sana.

Kutokana na ukiukaji wa haki za wafungwa, baadhi ya wahusika wanaoshikwa na kutiwa gerezani bila hatia wanadhulumiwa na polisi. Hali hii inachangia utengano wa kifamilia, ugonjwa, maumivu na majeraha mwilini.

## 2.3 Hitimisho

Katika sura hii, tumejadili namna dhuluma za kitabaka zinavyojitokeza kwa kuzingatia riwaya za *Mkamandume* na *Shetani Msalabani.* Tumebainisha ubepari kama chanzo cha dhuluma za kitabaka. Tumeonyesha namna wahusika wanyonge wa tabaka la chini walivyodhulumiwa wakati wa ukoloni na wazungu waliokuwa wakitawala. Wao ndio waliomiliki nyenzo za uzalishaji mali na walitumia nguvu za Waafrika ambao hawakumiliki chochote kuzalisha mali zaidi kwa manufaa yao pekee. Hata baada ya wakoloni kuondolewa nafasi zao zilishikiliwa na viongozi Waafrika walioendeleza dhuluma dhidi ya wenzao.

Kutokana na nadharia ya uhakiki wa ki-Marx tumebainisha dhuluma tano kuu ambazo ni; kubaguliwa kwa misingi ya rangi, kudhulumiwa kisaikolojia, kudhulumiwa kazini, kudhulumiwa kwa mwanamke na ukiukaji wa haki za kibinadamu. Wanyonyaji wanaendeleza ukatili kwa wanyonge kwa kuwapiga na kuwajeruhi, kuwaua, kuwanyang’anya mali yao na kuwanyima mahitaji yao ya kimsingi. Dhuluma hizi zimewaathiri wahusika wanyonge wa tabaka la chini ambao jasho lao linanyonywa na matajiri wa tabaka la juu.

Dhuluma hizi za kitabaka zinasababisha utengano wa kiuchumi baina ya matajiri wa tabaka la juu na maskini wa tabaka la chini. Wanyonge wanaishi maisha duni ya uchochole ilhali matajiri wanastarehe kwa maisha ya kifahari kutokana na jasho la wanyonge. Athari za dhuluma hizi zimejadiliwa kwa undani katika sura inayofuata.

# SURA YA TATU

# ATHARI ZA DHULUMA ZA KITABAKA KWA WAHUSIKA WA RIWAYA TEULE.

## 3.0 Utangulizi

Katika sura ya pili tumeona namna dhuluma za kitabaka zinavyojitokeza katika riwaya za *Mkamandume* na *Shetani Msalabani*. Tumeangazia aina za dhuluma zinazowakumba wahusika wanyonge wa tabaka la chini. Katika sura hii, tumebainisha athari za dhuluma za kitabaka kwa wahusika wa riwaya teule. Athari tulizoangazia ni: utengano wa kifamilia, ukosefu wa mahitaji ya kimsingi, ukosefu wa ajira, uhasama baina ya wahusika, kuuawa kwa wanyonge, kutengwa kwa wanyonge na majuto.

Nadharia ya uhakiki wa ki-Marx inaeleza kuwa historia ya maisha ya binadamu inaweza kuelezeka katika misingi yakinifu ya kiuchumi ambayo huchunguza njia kuu za uzalishaji na usambazaji mali. Kutokana na sababu za kiuchumi, hutokea matabaka ambapo tabaka moja humiliki nyenzo zote za uzalishaji mali na hivyo kulifanya kuwa na nguvu zaidi na uwezo mwingi kiuchumi. Kwa upande mwingine, tabaka la chini ndilo la wengi wasiomiliki chochote ila jasho lao na nguvu zao ambazo hutumika kuzalisha mali zaidi kwa manufaa ya wanyonyaji. Kupitia kwa nadharia hii, tumeangazia athari zinazobainika kutokana na dhuluma wanazopitia wanyonge wa tabaka la chini. Aidha, tumebainisha namna tabaka nyonyaji linajinufaisha kwa kunyonya jasho la wanyonge wasiomiliki mali. Tumeangazia maisha ya kifahari ya matajiri na mali nyingi wanayomiliki kutokana na ubepari wao.

### 3.1 Ukosefu wa Mahitaji ya Kimsingi

Ukosefu wa mahitaji ya kimsingi ni kukosa uwezo wa kupata chakula, mavazi, makazi na matibabu kutokana na hali ya ufukara. Katika riwaya teule, dhuluma za kitabaka zimesababisha wanyonge wa tabaka la chini kukosa mahitaji muhimu ya kimsingi. Nadharia ya uhakiki wa ki-Marx inadai kuwa tabaka la juu lililo na watu wachache humiliki nyenzo zote za uzalishaji mali huku maskini wa tabaka la chini hutumia nguvu zao kuzalisha mali ambayo huwafaidi matajiri pekee. Kwa hivyo umaskini hutokana na utabaka ambao huendelezwa na mabepari wanaotawala jamii.

Ngugi wa Thiong'o (1982) katika riwaya ya *Shetani Msalabani* anasimulia historia ya Wariinga inayofichua dhuluma walizofanyiwa waafrika wakati wa ukoloni. Hali hii inachangia ukosefu wa makazi na chakula kwa kuwa shamba lao linanyakuliwa. Mwandishi anasema kwamba:

> *Walipoona ya kuwa walikuwa karibu kushindwa na mashujaa wa Mau Mau walianza kuwanyanyasa na kuwadhulumu wafanyakazi na wakulima wadogo humu nchini* (uk 145).

Wazazi wa Wariinga walishikwa na kuwekwa gerezani na walipotolewa mwaka wa 1960 walipata shamba lao limenyakuliwa na kuuziwa wasaliti wa serikali ya kikoloni. Hali hii ilichangia wao kuisha maisha duni ya ufukara.

Waringa analazimika kwenda kuishi na shangaziye Nakuru ili aweze kumsaidia kupata mahitaji ya kimsingi. Wao pia waliishi maisha ya ufukara. Mjomba wake aliamua kutangamana na matajiri wa eneo hilo ili aweze kupata msaada wa kifedha. Tajiri wa Ngorika alitumia uwezo wake kiuchumi kumshawishi mjomba ili kumchumbia Wariinga.

Kwa sababu ya umaskini alikubali kupewa nyumba na shamba karibu na makazi ya Sambugo. Mwishowe, alichumbiana na Wariinga na kumpachika mimba. Wariinga alilazimika kukatiza masomo yake ili kulea ujauzito wake. Hali ilikuwa ngumu zaidi kwa kuwa hakuwa na wa kumsaidia kujikimu kimaisha.

Mwandishi katika riwaya ya *Mkamandume* anaonyesha hali ya kiuchumi visiwani Pemba na Zanzibar katika kipindi cha ukoloni. Wakati wa ukoloni Waafrika waliishi katika mazingira duni. Hali hii iliwasababishia watu wengi kutamani kujinasua kutokana na hali hii ili kuwa na maisha bora kama vile mabwana zao walivyokuwa wakiishi. Kinyume na matarajio, baada ya mageuzi tunaona kuwa hali ambayo Waafrika walikuwa wakitarajia imekuwa mbaya zaidi. Raia wa Malelejimema walikuwa wamekumbwa na umaskini usio kifani. Mwandishi anasema kuwa:

> *Hapo awali, Mkamandume aliishi katika hali ya umaskini na alijaa na tamaa ya kutoka katika hali hiyo siku moja. Hali ya umaskini ndiyo ilimsababishia kumsikiliza msemaji na kuamini kila alichosikia au kufikiria* (uk 18).

Karanja (1990) anaeleza kuwa kipindi cha uhuru kilitoa viongozi wapya waliounda tabaka jipya katika jamii huru ambao kusema kweli halikutofautiana na lile la wakoloni. Katika riwaya ya *Mkamandume* Wananchi wengi wanaishi maisha yenye dhiki na taabu. Ni vigumu kupata mahitaji ya kimsingi ya maisha. Watu wengi wanaishia kuishi bila vitu hivi ama kwa wachache waliobahatika kama mamake Ki-Mwachu anamtuma mwanawe kuomba sukari kwa Soud. Ki-Mwachu anapopewa sukari anashukuru kwani kwao walikuwa hawajainywa chai kwa kipindi cha miezi mitatu. Hii inaonyesha jinsi hali ilivyo

ngumu kwa wenyeji ambao wamemaliza miezi kadhaa kabla ya kuonja vyakula vya kimsingi.

Kilimo ambacho ndicho tegemeo la watu wengi katika Malelejimema kinaanza kuangamia na baada ya kipindi fulani, kunashuhudiwa ukosefu wa chakula kabisa. Mazao yanayopatikana kwa wale wakulima waliofanikiwa ni machache. Hali hii inasababisha kuwepo kwa visa vingi vya wizi. Wananchi wanaoshiriki wizi huu wanahatarisha maisha yao kwani wengi wao wanapigwa kibao ama kuuawa.

Hali hii ya umaskini inaendelea kukuzwa na baadhi ya Waafrika. Hali kama hii hutokea pale ambapo wakoloni huendelea kuwanyonya Waafrika wakisaidiwa na Waafrika wengine kwa sababu zao za kibinafsi. Waafrika waliochukua hatamu ya uongozi kutoka kwa mkoloni waliendeleza mbinu zile zile zilizokuwa za kibepari. Wakiongozwa na ubinafsi na tamaa, walianza kujinyakuliwa kila raslimali ili kuyakidhi mahitaji yao. Katika riwaya ya *Mkamandume,* mwandishi anasema kwamba:

> *Afrika, au Waafrika ni maskini na hawajafanya maendeleo ya maana kwa sababu wamenyonywa kwa muda mrefu na wanaendelea kunyonywa. Na kwa bahati mbaya baadhi yetu tunaendeleza unyonyaji huo kwa maslahi yetu (uk 149).*

Hali si hali tena kwa Wanamalelejimema. Vile visenti walivyokuwa wakivipata hapo awali haviko tena. Ukulima uliokuwa tegemeo la wengi sasa unaendelea kuzikwa katika kaburi la sahau. Hali kama hii inasababisha uchungu miongoni mwa wahasiriwa ambao wameshakuwa mabaradhuli. Hali za wengi zimekuwa sasa kupita kwa watu huku wakiomba chumvi na sukari. Hali kama hii inawaumiza sana wale walioshiriki kwa

vyovyote vile katika mapinduzi wakitarajia kupata nafuu baada ya mkoloni kuondoka. Kinyume na matarajio, wale wavivu wasiofanya chochote ndio wanaotamba kwa kutumia jasho la wengine.

Wanajamii wa Malelejimema wanalazimika kujiunga na jeshi la wakopaji na waombaji. Na wale wanaoombwa hawapatikani kwani maisha yanazidi kuwa magumu kwa wananchi wengi. Wakati idadi kubwa ya watu inazidi kuangamia katika umaskini, nayo idadi chache inazidi kujilimbikizia mali na kufyonza zile raslimali za nchi zilizosalia. Walio wachache kila uchao wanaibua mbinu za kuzidi kubaki juu ilhali maskini wakiendelea kumaskinika.

Mwandishi anatupa taswira ya baadhi ya wananchi hawa wazalendo walioshiriki katika vita vya kimapinduzi. Anasema kuwa mkewe Suguru, Mbunjaki aliyekuwa hapo awali na sura ya kuvutia sasa si mwanamke tena. Alikuwa amekonda kakondeana, kabakia macho tu. Mwandishi anaeleza kuwa:

> *Alikuwa kavalia kanga regerege kifuani, na kwa vile linavyoonekana, lilikuwa halijaguswa na maji na sabuni kwa miaka. Kifua chenyewe sasa bapa. Utadhani kimepigwa randa! Hakikututumka hata chembe. Yale maboribo hapo kale sasa yamegeuka matambara mabovu yanayomning'inia nyuma* (uk 417).

Hii ndiyo taswira ya watu wengi ambao hapo awali walikuwa na sura ya kupendeza na miili yao ilikuwa na nguvu lakini kutokana na umaskini unaowakumba sasa hali zao zimebadilika na kuwa dhaifu.

Nadharia ya uhakiki wa ki-Marx inadai kuwa mabepari hutumia jasho la maskini ili kuendelea kujinufaisha. Hali hii inadhihirika katika riwaya ya *Mkamandume.* Wale watu

wachache waliofanikiwa kufanya kazi za vibarua, mishahara yao haikuweza kuwakimu kimaisha. Bei za bidhaa zinaendelea kupanda ilihali mshahara ni ule ule ama sivyo unaendelea kupunguzwa kutokana na matakwa mbalimbali. Baadhi ya vitu vya thamani vilivyoachwa nyuma na wageni waliofurushwa ni majumba yaliyokuwa ya wakoloni ambayo yalikuwa ya kuvutia mno.

Waafrika waliyakimbilia majumba haya na baada ya kipindi cha miongo minne, majumba hayo yalikuwa yamechoka kwani hayana wa kuyashughulikia tena. Wenyeji walioishi humo ndani walikuwa wamekataa kuhama kwa sababu hawakuwa na mahali pengine pa kuhamia. Walivumilia matatizo waliyokumbana nayo, hasa wakati wa mvua huku wakitazamana na mauti ambayo yangetokea wakati wowote. Wananchi wote wana haki ya kuwa na makazi ili waweze kuendeleza shughuli zao za maisha. Hali hii ilikuwa kinyume na wakazi wa eneo hili la Malelejimema kutokana na utabaka na uongozi mbaya. Viongozi na matajiri wa tabaka la juu ndio walioishi maisha bora katika mazingira ya kifahari. Hawakuwajali wanyonge walioteseka kwa sababu ya ubinafsi na tamaa waliyokuwa nayo.

### 3.2 Ukosefu wa Ajira

Dhuluma za kitabaka zimechangia pakubwa ukosefu wa ajira miongoni mwa wahusika wa tabaka la chini. Tabaka nyonyaji ndilo lililonyakua kazi za kudumu na ambazo zina mishahara mikubwa. Karl Marx kupitia kwa nadharia ya uhakiki wa ki-Marx anasisitiza kuwa tabaka la juu ndilo humiliki nyenzo za uzalishaji mali hivyo kulifanya kuwa na nguvu na uwezo mwingi kiuchumi.

Ngugi wa Thiong’o (1982) katika riwaya ya *Shetani Msalabani* anaonyesha namna ukosefu wa ajira umekithiri kutokana na dhuluma za kitabaka. Wangari analazimika kuhamia jijini

Nairobi kutafuta ajira baada ya kishamba chake cha ekari mbili kunadiwa na Benki aliposhindwa kulipa mkopo wao wa shilingi elfu tano. Wangari anaeleza kwamba:

> *… kwa hivyo nilijipa moyo nikajiambia siwezi kukosa kibarua angaa cha kufagia afisi au vyoo. Sitakuwa na hiari ya kuchagua kazi maana maskini hupokea apewacho (uk 40).*

Kule jijini Wangari aliandamwa na masaibu mengi akitafuta ajira. Alishikwa na kutiwa ndani kwa kushukiwa kuwa mwizi. Wangari anawasimulia marafiki wenzake kuwa:

> *Moja kwa moja nilisukumwa ndani ya gari la polisi. Nilipelekwa kwenye kituo cha polisi nikatiwa katika kitundu. Humo kitunduni mlikuwa na makao makuu ya chawa, kunguni mbu na viroboto. Huwezi kupata hata lepe la usingizi! Nilikaa humo kwa siku tatu: Mimi Wangare ambaye sijawahi kumwibia mtu hata kiazi kimoja (uk 41).*

Baada ya kufungiwa kitunduni kwa siku tatu alipelekwa mahakamani na kushtakiwa kwa mambo mawili: kudhaniwa wizi na uhuni. Alitozwa faini ya shilingi mia mbili kwa kuzurura mjini bila ya kibali.

Ukosefu wa ajira unamfanya Wariinga kushindwa kulipa kodi ya nyumba. Aidha, anakumbwa na dhuluma kutoka kwa tajiri aliyekuwa amemkodishia nyumba baada ya kuachishwa kazi kwa Bepari Kihara. Tajiri wa nyumba alimwendea Wariinga na kumtaka aongeze kodi ya nyumba. Hii ilikuwa kinyume na makubaliano yao hasa ikizingatiwa mazingira yalikuwa duni sana. Wariinga anachora taswira ya makazi yenyewe anaposema kuwa:

*… lakini jamani, hii ilikuwa nyumba au kiota cha ndege? Sakafu ilikuwa na mashimo, ukuta ulikuwa na mianya mingi mikubwa na paa lilikuwa linavuja* (uk. 6).

Wariinga alipokataa kuongeza kodi, tajiri wake alimletea majambazi wakamvurumisha nje bila kujali. Yule tajiri alimwambia Wariinga kuwa:

*Nimekuletea maafisa wa mahakama ya kodi za nyumba (uk 6).*

Vitu vyote vya Wariinga vilivurumishwa nje kama takataka na kijumba kikafungwa kwa kufuli nyingine. Hali hii ilimsababishia Wariinga masaibu mengi zaidi kwa kuwa hakuwa na ajira ya kuweza kujikimu kimaisha.

Katika riwaya ya *Mkamandume*, ukosefu wa ajira unajitokeza pakubwa. Ajira zilizopatikana zilikuwa duni na zenye mishahara midogo. Baada ya wakoloni kuchukua utawala na kujinyakulia mashamba ya Waafrika, wenyeji walilazimika kufanya kazi ya vibarua katika mashamba ya mikarafuu. Aidha, baada ya viwanda kadhaa kujengwa visiwani, watu walihamia mijini na kuanza kufanya kazi katika viwanda hivyo. Hii ilikuwa njia moja ya wakoloni kuhakikisha kuwa Waafrika walikuwa wategemezi wao. Kwa kufanya hivi lengo lao lilikuwa kuendeleza utabaka katika jamii.

Baada ya mapinduzi ya mwaka wa 1964, wananchi walitarajia kuwa nafasi za kazi zingepatikana kwa wingi. Waafrika walitarajia kuwa uongozi ukiwa mikononi mwao ama tuseme ukiwa mikononi mwa ndugu zao basi kungetokea nafasi bora za kazi na hata mazingira ya kufanyia kazi yangeboreshwa. Jambo hili halikutimizwa kwani tunawaona vijana wengi ambao wamemaliza vyuo lakini hawana ajira kwa kipindi kirefu. Soud ni

kijana ambaye amesomea uanasheria lakini kwa sasa miaka minane imepita bila ya yeye kuajiriwa au kujiajiri mwenyewe.

Ni ukosefu wa kazi ndio unawafanya wananchi wengi kuendelea kuvumilia dhuluma za wakubwa wao kwani hawakuwa na mahali pengine pa kwenda iwapo wangeziacha kazi ambazo walikuwa nazo. Baada ya mkoloni kuingia katika nchi za Kiafrika mfumo wa uchumi ulibadilika na watu kuanza kutegemea ajira ili kupata chakula. Hata baada ya mkoloni kuondoka mfumo huu wa kiuchumi uliendelezwa na Mwafrika huku akisahau maisha yake ya hapo awali ya ujamaa. Ni kutokana na mfumo huu ndiposa kazi inakuwa tegemeo kubwa kwa wananchi. Aidha, wananchi hawana mashamba ya kuendeleza kilimo kama ilivyokuwa hapo awali kabla ya mkoloni kuwasili. Hali hii imesababishwa na baadhi ya Waafrika waliokuwa na tamaa ya kujinyakulia mashamba kama watangulizi wao. Waafrika hawa wamejinyakulia mashamba makubwa huku wakiwawaacha wananchi wa kawaida kuangamia katika umaskini.

Marx na Engels (1959), wanasema kuwa ni kutokana na sababu za kiuchumi ambapo matabaka huibuka. Tabaka moja huhodhi nyenzo zote za uzalishaji mali hivyo basi kulifanya liwe na nguvu na uwezo kifedha huku tabaka la chini ambalo ndilo lenye watu wengi huwa hawana chochote ila jasho lao na nguvu zao wanaziuza kwa wenye mali ili wayakidhi mahitaji yao. Kwa wale wachache waliofanikiwa kupata kazi ambazo zinadhaminiwa, wanatumia fursa hii kuwanyanyasa wenzao. Mwandishi anasema kuwa:

> *Mke wa Bilal alichukuliwa na mkuu wa jeshi. Bilal alimpenda sana mkewe na kuondoka kwake kulisababisha aishi maisha ya majuto na ukiwa hadi kuwa mwehu (uk 46).*

Ukosefu wa kazi umekiathiri sana kizazi kipya kwani tunawaona vijana wengi katika jamii ya mwandishi hawana kazi. Viwe alipotorokea mjini baada ya kupigwa kikatili na babake, alitaabika kwa kukosa ajira. Alipambana na hali ngumu ya maisha ya mjini. Alilazimika kuanzisha biashara iliyomsaidia kupata pesa ya kurejea shuleni kuendelea na masomo yake.

### 3.3 Kuuawa kwa Wanyonge

Visa vya wahusika wa tabaka la chini kuuawa na wanyonyaji wa tabaka la juu kwa misingi ya kiuchumi na kisiasa vimesheheni katika riwaya teule. Ngugi wa Thiong'o (1982) katika riwaya ya *Shetani Msalabani* anasimulia namna wazungu wa tabaka la juu walivyowaua Waafrika wanyonge waliokuwa wakipigania haki zao. Mwaura alitumiwa na wazungu kuwaangamiza Waafrika bila huruma. Mwandishi anasema kuwa:

> *Alianza kazi hiyo wakati wa hali ya hatari. Wakati huo alikuwa msaliti mkali kama pilipili. Alikuwa katika kikundi cha wauaji kilichoongozwa na mzungu aliyeitwa Nyangwecu kutoka Rift Valley. Wakati huo Mwaura alilipwa shilingi tano kwa kila kichwa kimoja cha Mau Mau; mwanamke, msichana, mtoto, mwanamme, Mwaura hakuchagua (uk 207).*

Aliendelea na kazi hii ya mauaji hata baada ya wakoloni kuondoka. Alijiunga na kikundi kingine cha wauaji na kuendelea kuwaangamiza watu. Walifadhiliwa na tabaka nyonyanyi lenye ubinafsi na tamaa ya mali.

Maelezo ya Wariinga yanaonyesha ukatili waliotendewa maskini wa tabaka la chini. Aanasema kwamba:

> *Kimenderi wa Kinyuanjii alikuwa mtu katili sana. Alipewa jina hilo wakati wa hali ya hatari kwa kuwasaga wafanyakazi na mafalahi. Alikuwa hayawani kabisa. Aliwaamuru wanaume na wanawake walale barabarani halafu akapitisha gari la Land Rover juu ya miili yao* (uk 198).

Alipandishwa cheo akawa katibu wa kudumu. Baadaye aliajiriwa na makampuni ya wageni hasa yaliyohusika na pesa. Anapendekeza mbinu dhalimu itumiwe dhidi ya wafanyakazi wanyonge. Anadai kuwa kuajiriwe wahubiri wa kuhubiri unyonyaji na kuanzishwe shule zinazofundisha kuhusu unyonyaji wa damu.

> *Shule ambazo watoto watakuwa wakishindiliwa na kuimba kama kasuku nyimbo za kusifu unyonyaji wa damu na miili ya watu (uk 201).*

Anapendekeza pia majumba ya sinema na michezo ya kuigiza yajengwe. Mahali ambamo uzuri wa mabepari utasifiwa; kunyonya damu na kula miili ya watu.

Ushahidi wa Kihahu wa Gatheeca katika karamu ya kujisifu na kufundishana mbinu za kuwanyanganya maskini mali yao unadhihirisha dhuluma dhidi ya wanyonge. Anaeleza namna viongozi walitenda matendo ya ukatili wakati wa uchaguzi. Anadai kuwa:

> *Hata mnajua ya kuwa baadhi ya watu wamepata kuwahamisha wenzao duniani kwa sababu ya kiti hicho. Niliajiri wahuni mabarubaru ambao kazi yao ilikuwa kuharibu mali ya watu. Niliwaamuru wawachape bastola na kuwaambia wachague baina ya uhai na kifo. Wale waliokataa kusalimu amri waliuawa* (uk 119).

Aliendeleza ukatili huu wa kuwaangamiza wapinzani wake hadi akachaguliwa kuwa kiongozi.

Katika riwaya ya *Mkamandume,* mauaji ya wanyonge yanasababisha majonzi miongoni mwa wanajamii waliofiwa. Kupitia kwa mazungumzo kati ya Mzee Mkasi na Time tunafahamu majuto yaliyomkumba Mzee Mkasi baada ya kifo cha mkewe Biti Sahera. Mzee Mkasi anakataa katakata kumchinja kuku kwa kuwa hakutaka kukumbuka vita vya pili vya dunia vilivyofanyika kikatili. Pia, aliomboleza kifo cha mwanawe Masudi aliyekufa katika vita vya wenyewe kwa wenyewe. Wakati wa vita vya ukombozi katika nchi ya Malelejimema alishikwa na kuwekwa kizuizini bila hatia yoyote. Alisingiziwa kuwa alishiriki njama ya kuleta uchochezi nchini. Anasema kuwa:

> *Baada ya hapo nilikamatwa nikaambiwa nimeshiriki katika magendo ya Karafuu. Adhabu yake ni kifo. Sikuuliwa. Niliachwa baada ya mateso mabaya* (uk 187).

Bwana Aziz, babake Soud pia anaangamizwa kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe. Bwana Sleyyum anamsimulia Soud kuhusu kifo cha babake ambaye hakuwa na hatia yoyote. Bwana Sleyyum alipotaka kujua sababu ya mauji hayo yaliyotokea aliwekwa gerezani na kuteswa vibaya sana. Anaeleza kuwa:

> *Niliteswa vibaya sana. Mateso yasiyoelezeka (uk 302)*

Hali hii inamuathiri sana Bw. Sleyyum kisaikolojia na kumfanya aishi maisha ya upweke na huzuni. Pia ilisababisha utengano kati ya familia ya Bw. Aziz na Mkamandume.

### 3.4 Kutengwa kwa Wanyonge

Kutokana na dhuluma za kitabaka, utengano baina ya matajiri na maskini kwa misingi ya kiuchumi na kisiasa unajitokeza katika riwaya za utafiti. Sarara (1997), akimnukuu Ngara (1985), anasema kuwa; katika jamii yenye matabaka, nguvu za kiuchumi huwa na

watawala ambao huhodhi nyenzo za uzalishaji mali. Anaendelea kusema kuwa tabaka hili hili ndilo pia husimamia elimu na itikadi katika jamii. Mawazo, imani na itikadi ya tabaka tawala huchukuliwa kuwa ya jamii nzima.

Katika riwaya ya *Shetani Msalabani*, mwandishi anaonyesha utengano uliopo baina ya mazingira ya Milima ya Dhahabu na mtaa duni wa Jerusa. Matajiri wa tabaka la juu waliishi katika eneo la kifahari la Milima ya Dhahabu kutokana na uwezo wao kiuchumi. Mwandishi anachora taswira ya mandhari ya kuvutia kwa kusema kuwa:

> *Majumba yalinakishiwa kwa fito za dhahabu na sakafu zilipambwa kwa mazulia ya Uajemi. Huko kuliendelea kupanuka kwa sababu ya wingi wa mali na pesa (uk 247).*

Kwa upande mwingine, mtaa duni wa Jerusa ulitawaliwa na wanyonge wa tabaka la chini. Mazingira hayakuwa ya kupendeza kamwe. Msimulizi anaeleza kwamba:

> *Jerusa nako kuliendelea kupanuka. Vijumba vibovu, mitaro ya maji machafu yanayonuka. Moshi unaotoka katika viwanda vya wageni (uk 247).*

Wafanyakazi wasio na kazi, maskini wote, wauzaji pombe, mandazi na wauza miili yao wote huishi eneo hili. Wakazi waliishi maisha duni ya ufukara kutokana na uwezo wao wa chini wa kiuchumi. Tabaka nyonyaji liliendelea kuwanyonya kwa njia ya kujinufaisha kiuchumi.

Wariinga aliishi katika mazingira duni jijini Nairobi. Licha ya hali duni ya nyumba aliyokodisha, tajiri wake alimshurutisha aongeze kodi. Wariinga analalamika kwa kusema kuwa:

> *… lakini jamani, hii ilikuwa nyumba au kiota cha ndege? Sakafu ilikuwa na mashimo, mashimo, ukuta ulikuwa na mianya mingi mikubwa na paa lilikuwa linavuja (uk 6).*

Wariinga alipokataa kuongeza kodi, tajiri wake alimletea majambazi wakamvurumisha nje bila kujali. Yule tajiri alimwambia Wariinga kuwa:

> *Nimekuletea Maafisa wa mahakama ya kodi ya nyumba. Vitu vyote vya Wariinga vilivurumishwa nje kama takataka na kijumba kikafungwa kwa kufuli nyingine (uk 6).*

Wariinga alikerwa sana na jambo hili, hasa akikumbuka kuwa alikuwa amefutwa kazi na pia kukataliwa na mchumba wake. Kutokana na masaibu haya alijaribu kujitia kitanzi lakini akaokolewa na kijana mmoja.

Katika riwaya ya *Mkamandume* kuna matabaka ya viongozi na wananchi, matajiri na maskini, wenye haki na wasio na haki, wasomi na wasio wasomi. Suala la kutengwa kwa wanyonge linaenea zaidi hata baada ya Waafrika kujikomboa. Mkamandume na familia yake waliishi katika mazingira duni ya uchochole licha ya kupigania ukombozi wa nchi yao. Walilala katika chumba duni ambacho hakikuwa na mlango ila kigunia kibovu kilichoning'inia. Ukuta ulizibwa na matambara na makaratasi ili kuzuia macho ya wapita njia yasiingie ndani. Waliumwa na kunguni pamoja na mbu. Time anadai kuwa:

> *Huyu alikuwa kunguni wa mia moja aliyemtafuna tokea alipoupata ubavu wake hapo tandikoni. Kisha anasikia minong'ono ya mbu… (uk 93).*

Hali hii ilimkera sana Mkamandume kwa kuwa alihusika pakubwa kupigania uhuru wa nchi yake kisha anakosa kufaidika.

Wanyonge walitengwa katika ugavi wa raslimali ya umma. Usawa haukuwepo katika kugawa ardhi kwa wananchi wa Malelejimema. Tabaka la juu ndilo lilijigawia mamia ya ekari ya ardhi yenye rutuba na utoshelevu huku wanyonge wakipewa vishamba vidogo. Baada ya wananchi kugundua kuwa jambo la ugawaji ardhi kati ya wananchi halikuwa na usawa walisonononeka sana. Vile vishamba walivyopewa havikuwa na rutuba kwa hivyo havingeweza kuzalisha hata robo ya mazao waliyokuwa wakizalisha hapo wali.

Ugavi wa resheni pia uliwanufaisha matajiri pekee. Wananchi walilazimishwa kuchukua vitu mbalimbali kama vile ratili ya mchele na sukari mara moja kwa juma. Huku haya yakitokea, waheshimiwa walikuwa wakipata magunia ya michele, sukari, unga na vyote muhimu walivyotaka. Hali hii inaleta chuki miongoni mwa wale ambao hawakufanikiwa kupata mgao mkubwa. Mahitaji ya kimsingi kama vile maji, umeme, matibabu yalipatikana kwa wale wachache waliobahatika. Katika baadhi ya mitaa, maji yanapatikana kwa wingi na wenyeji wanakoga kila wakati wanapotaka. Mengi ya maeneo haya ni yale yaliyokuwa karibu na Ikulu. Bwana Sleyyum anamshukuru Mungu wake kwa kumwepusha yeye na mkewe udhia ya maji, kisirani ya umeme na ukosefu wa chakula. Hii ni kwa sababu alikuwa miongoni mwa wale walioishi karibu na Ikulu, eneo ambalo halikufahamu msamiati wa ukosefu wa mahitaji haya ya kimsingi.

Soud anapomtembelea Bwana Sleyyum, chakula kinachoandaliwa kingewatosha watu wengi. Yeye na wenzake wachache wanapoendelea kuishi katika maisha ya starehe, kwa upande mwingine maskini kama vile; Mkamandume, Suguru na Silima na familia zao hawana chochote cha kuyasitiri matumbo. Pia, serikali haikuachwa nyuma katika kuendeleza ubaguzi. Sababu moja ya ukosefu wa kazi kwa vijana waliohitimu kama Soud ni ubaguzi ambao umeenea kazini. Nafasi chache za kazi zinazopatikana ziwaendea wale

walio na uhusiano wa karibu na maafisa wa kiserikali. Njia za uteuzi kazini hazitegemei stakabadhi alizonazo kijana ila unategemea: kabila la mtu, uaminifu wa chama ama mahusiano na watu wanaotambuliwa na serikali tu. Imemchukua Soud kipindi cha miaka kumi na mitatu tangu atoke Uingereza alikokuwa ameenda kusomea uanasheria bila kupata kazi yoyote. Kila alipotuma maombi ya kazi ya wakili maombi yake yalikataliwa na serikali kwani hakuwa miongoni mwa wale walioaminiwa na serikali kuifanya kazi hasa kama ya uanasheria.

Utengano wa kiutabaka uliendelezwa na wachache waliokuwa mamlakani. Viongozi wenye ubinafsi walijinyakulia vile vifaa vichache vilivyosalia ili kujinufaisha wenyewe. Kazini anakofanya kazi Mkamandume, kulikuwa na choo kimoja tu ambacho daima huwa safi licha ya vyoo vingine kuwa vichafu. Hii ni kwa sababu Mkamandume alipewa vifaa vya kutosha vya kukiosha choo hicho. Choo hicho hufungwa kila mara na funguo huwa mikononi mwa Bi. Sekretari. Choo hicho kinatunzwa vizuri kwani ni cha bosi, maafisa wenzake na wageni wakubwa. Huu ulikuwa ni unafiki wa kuficha ukweli wa mambo hasa wageni wa kutoka maeneo mbalimbali walipozuru ofisi hizo. Choo kimoja kinaashiria ubaguzi maanake ni wale wachache tu ndio wanaenziwa ilhali wale wafanyakazi wengine walifaa kuvitumia vyoo ambavyo vilikuwa vichafu kwa sababu ya ukosefu wa maji na vifaa vya kuosha.

Wafanyakazi wa viwango vya chini kama Mkamandume wanafaa kufika kazini asubuhi kabisa na kuanza kazi zao ambazo kwa kawaida huchukua masaa marefu ilhali mishahara yao ni midogo sana. Kinyume na waliokuwa na vyeo ambao wanawasili kazini wakiwa wamechelewa na mishahara yao ni ya juu. Bi. Zuhuru Juma, sekretari wa bosi alikuwa akiwasili kazini baada ya saa nne za asubuhi masaa machache tu kabla ya boss wake.

Wafanyakazi wanabaguliwa kwa misingi ya vyeo na walio na vyeo vya chini ndio hufanya kazi nyingi ilihali malipo yao ni duni. Hali hii ni kinaya kwa kuwa viongozi wa tabaka la juu wanafaidika kutokana na jasho la wanyonge wanaofanya kazi kwa bidii.

### 3.5 Uhasama Baina ya Wahusika

Uhasama ni hali ya kukosa kupatana kwa sababu ya ugomvi. Dhuluma za kitabaka zinasababisha uhasama baina ya wahusika wa matabaka. Katika riwaya ya *Mkamandume* suala hili linajitokeza wazi miongoni mwa wahusika. Posa ya Soud kwa Time inakataliwa kwa misingi kuwa Soud alikuwa mwana wa adui wa Mkamandume tangu jadi. Licha ya Soud kumsamehe Mkamandume kwa kumuuwa babake, bado ana machungu moyoni. Anaeleza namna alivyomtendea babake dhuluma. Soud anasema kuwa:

> *Mkamandume ndiye aliyemfyeka babake, yeye Soud anajua. Siku nyingi yeye Soud amekuwa akienda na uchungu moyoni na kutafuta njia ya kulipiza kisasi (uk 236).*

Hali hii ilimtatiza Soud maishani hatimaye aliamua kumsamehe Mkamandume lakini alikerwa zaidi posa yake ilipokataliwa mbali kutokana na hiyo chuki. Anadai kuwa:

> *… lakini chuki za Mkamandume zilithibitika pale Soud alipoenda kumposa Time. Akafahamu kwamba mambo bado yalikuwa hayajesha (uk 236).*

Soud aliathirika kisaikolojia kutokana na kukataliwa kwa posa yake licha ya kuwa alimpenda Time na tayari alikuwa amemsamehe Mkamandume.

Mkamandume anakataa katakata kupata msaada kutoka kwa Mzee Mkasi ambaye kwake Mkamandume alikuwa muasi kwani alishirikiana na wakoloni. Mzee Mkasi kwa sasa anaweza kujikimu kimaisha baada ya kujitenga na wanajamii waliomtenga baada ya

kukataa kushiriki katika vita vya mapinduzi. Mzee huyu aliamua kukiendeleza kilimo katika konde lake. Mimea katika konde lake ilikuwa ikinawiri sana kinyume na makonde ya wananchi wengine kama vile Mkamandume. Hata hivyo wananchi waliokuwa na msimamo mkali kuhusu watu kama Mzee Mkasi, wanakataa kujihusisha naye kwa vyovyote hata ikiwa ni kupata msaada wa chakula.

Mkamandume alipolemewa kwa kukosa chakula kabisa, analazimika kwenda kwa Mzee Mkasi ili apewe msaada. Lakini kabla ya kufika huko anakumbuka kuwa huyu ni adui wa milele kwa hivyo anakufa moyo na kuikatiza safari yake. Aidha, Sleyyum ambaye alimpoteza rafiki yake bwana Azizi katika vita hivi, haoni sababu ya Soud kumsaidia Mkamandume ambaye ndiye alikuwa katika mstari wa mbele kuwafyeka watu wakati wa vita hivi. Nadia anapomtajia umuhimu wa kuungana mikono katika harakati za ukombozi, anapinga kwa kusema kuwa:

> *Mimi niwaunge mkono? Nimekuridhia mengi Nadia kwa ajili ya asili zetu na kwa ajili ya Soud na pia kwa ajili ya wazee wako walivyokuwa na insafu na wazee wangu, lakini hili unalotaka sasa ni ngumu kwangu mimi kulitekeleza. Hujui namna watu hawa walivyonitesa (uk 403).*

Uhasama huu unakuwa kikwazo kwa maendeleo ya kiuchumi na kisiasa kwani makundi mawili haya hayawezi tena kutangamana hata kama ni kushirikiana katika suala muhimu kama kupigania haki zao. Chuki hii inasababisha visasi kwa vizazi ambavyo havikuwepo wakati wa vita hivyo. Hii ndiyo sababu kuu ya ombi la Soud kumposa Time inakatiliwa na Mkamandume kwa misingi ya uadui uliokuwepo wakati wa vita. Ni baada ya Sleyyum kumwelezea Soud siri ya maisha yalivyokuwa katika seli za Malelejimema ndiposa alimpasulia mbarika kuhusu msimamo wake juu ya Waswahili. Sleyyum anamwambia

Soud jinsi alivyokuwa ameteswa kwa kutiwa kamba ndani ya shingo na kuvutwa huku akichanikachanika vibaya shingoni.

Pia, alikuwa amevutwa sehemu zake za siri kwa kamba kana kwamba wavutaji walikuwa wakivuta maji kwenye kisima. Anaendelea kusema kuwa, alilala sakafuni bila hata ya kirago na kila asubuhi alibebeshwa debe lililojaa kinyesi. Haya madhila yanayoshuhudiwa baada ya ukombozi wa bendera hayana tofauti na yale ya wakoloni waliyokuwa wakiwafanyia Waafrika ambao hawakuwa na hatia. Ni kutokana na uchungu huu ndiposa bwana Sleyyum anamwonya Soud dhidi ya Waswahili. Anasema:

> *Usiwasaidie Soud Waswahili, epukana nao, usijishughulishe na mambo yao. Ni watu wabaya. Mara wanaweza kukupotezea maisha yako (uk 303).*

Mtazamo kama huu miongoni mwa wananchi ni hatari sana kwani wakati wowote kunaweza kutokea mlipuko wa kujaribu kuyatatua matatizo haya.

Vilevile, katika riwaya ya *Shetani Msalabani,* Wariinga anaishi na machungu moyoni baada ya kupachikwa mimba na tajiri la Ngorika kisha anatemwa. Anapata fursa ya kulipiza kisasi wakati wa sherehe ya kufunga ndoa kati yake na Gatuiria ambaye alikuwa mwanawe tajiri huyu. Anapojaribu kupinga ndoa hiyo ya mwanawe, Wariinga anakerwa sana na anaamua kumuua kwa kumfyatulia risasi.

### 3.6 Utengano wa Kifamilia

Utengano wa kifamilia ni hali ambapo jamaa wa familia moja hutengana na kwenda kuishi maeneo tofauti kwa sababu ya migogoro ya kifamilia, kijamii, kisiasa au kiuchumi. Waandishi wa riwaya za utafiti wameangazia suala hili kwa kina. Katika riwaya ya *Shetani Msalabani* Wariinga analazimika kutoka nyumbani kwao na kwenda kuishi na shangaziye

Nakuru baada ya wazazi wake kushikwa na kutiwa gerezani. Shamba lao linauzwa na anakosa mahitaji ya kimsingi. Kutokana na umaskini anashawishiwa na Tajiri wa Ngorika ambaye anampachika mimba na kuvunjilia mbali uhusiano wao. Baada ya kujifungua analazimika kuhamia Nairobi kutafuta kazi ili kujikimu. Alitengana na familia yake kwa muda mrefu sana.

Gatuiria anasimulia chanzo cha utengano baina yake na babake. Anaeleza kuwa babake alikuwa tajiri wa kupindukia na alimiliki mali chungu nzima. Aliishi maisha ya kifahari katika maeneo ya kifahari. Anamwambia Wariinga kuwa:

> *Baba yangu ni mfanya biashara. Ana maduka mengi sana Nakuru. Ana mashamba mengi sana Rift Valley. Ana biashara nyingine nyingi za kuagiza na kupeleka vitu ulaya kwa eropleni. Mimi ndiye mwana wa pekee. Alikuwa anapendelea sana niende Amerika nijifunze taaluma ya Uchumi na Biashara. Lakini tangu zamani sikupendelea kufuata mienendo ya baba. Wafanyakazi walikula vyakula duni na kuvaa matambara. Mara kwa mara babangu aliwapiga bakora huku akiwatukana vibaya na kuwaita ng'ombe (uk 139*).

Matendo haya ya kikatili dhidi ya wanyonge ndiyo yalichangia Gatuiria kuondoka nyumbani na kwenda jijini hali iliyosababisha utengano wa kifamilia.

Utengano wa kifamilia ulisababisha utangamano kati ya Wariinga na Gatuiria. Gatuiria alijitokeza kama msamaria mwema ambaye alimfaa wakati wa shida. Wariinga alimsimulia masaibu yote yaliyomwandama tangu wazazi wake walipotiwa gerezani, kuuzwa kwa shamba lao, kupachikwa mimba na kujaribu kujiua, kisha kuhamia Nairobi kutafuta kazi.

Pia, alimweleza namna alivyofutwa kazi na kuhamishwa alikokuwa amekodisha nyumba. Baada ya wao kuchumbiana wanaamua kufunga ndoa. Wanasafiri kwenda nyumbani kulikoandaliwa sherehe ya kukata na shoka. Mwandishi anasema kuwa:

> *Maandalizi ya sherehe ya ndoa kati ya Gatuiria na Wariinga ilikuwa ya kifahari. Wageni walielekezwa katika maduka ambako wataweza kununua zawadi (uk 252).*

Wariinga anagutushwa anapogundua kwamba babake Gatuiria ndiye yule tajiri wa Ngorika aliyempachika mimba. Kutokana na machungu ya awali anampiga risasi na kumwangamiza papo hapo. Gatuiria mpenziwe anajipata katika njia panda. Mwandishi anasema kuwa:

> *Gatuiria alipigwa na bumbuazi, Asijue la kufanya. Hakujua amshughulikie babake au mpenziwe Wariinga (uk 272).*

Katika riwaya ya *Mkamandume,* kuna utengano katika familia ya mhusika mkuu Mkamandume. Utengano huu unatokana na mgogoro kati Mkamandume na mkewe Tufaa. Mkewe alijutia mabadiliko aliyoyashuhudia kwa mumewe. Mwandishi anasema kwamba:

> *Alifanya hivyo alipogundua kwamba yule si mume aliyemfahamu. Ni kivuli cha mtoto cha mwanamme mpya!* (uk 17).

Tufaa alikumbuka namna mumewe alivyompenda zamani. Anadai kuwa mapenzi hayo yaliyotoweka na sasa analazimika amridhi mumewe zaidi kuliko alivyomridhi tokea kufungamana naye.

Migogoro zaidi inajitokeza katika familia ya Mkamandume baada ya bintiye kupachikwa mimba. Viwe anapachikwa mimba na Bete, rafikiye Fikirini. Hali hii ilimlazimu mamake, Bi Tufaa kumwendea Shoga yake Bi. Reja ili waavye mimba hiyo. Jambo hili halikufua dafu na babake alipogundua kuwa alikuwa mjamzito alimpiga kikatili. Mwandishi anasema kuwa:

> *Mkamandume hakujibu kitu. Alimvuta Time akamzaba kibao kikali. Huyo Time akaanguka chini. Kisha akamkamata Viwe na kumtupa chini. Alimwinamia na kumkaba shingo (uk 112).*

Mamake pamoja na dadake walijeruhiwa vibaya walipojaribu kumwokoa. Baada ya kushindwa waliwaita majirani kuwasaidia. Mwandishi anadai kuwa:

> *Hata walipokuja majirani, kike kwa kiume mwele aliyekuwa akilemewa na babake alikuwa akitoka kipovu kinywani. Time alikuwa akivuja damu puani na Bi Tufaa kavimba na kufusika vibaya vibaya usoni. Ilihitajika wanaume sita wenye nguvu zao kuweza kumng'ang'anua Mkamandume (uk 112*).

Time alitoweka na kutengana na familia yake kwa muda mrefu. Hali hii ilimfanya Mkamandume kupatwa na msongo wa mawazo. Alitatizika sana na akaamua kwenda mjini kumtafuta bintiye ili kumwomba msamaha kwa ukatili aliyomtendea.

### 3.7 Majuto

Dhuluma za kitabaka zimesababisha wahusika katika riwaya teule kujutia matendo yao. Aidha, matendo ya awali waliyotekeleza bila kujua athari zake yanawaathiri sana na kuwafanya kujuta. Katika riwaya ya *Mkamandume*, mwandishi anaangazia wahusika ambao wana majuto kutokana na dhuluma zilizowakumba. Mhusika mkuu Mkamandume

anajutia ukatili aliotenda baada ya nchi yake kujinyakulia uhuru. Alijutia vitendo alivyovifanya miaka arobaini iliyopita. Alifyeka mazao yote shambani kutokana na hasira alizokuwa nazo. Jambo hili lilimshangaza sana bintiye, Time alipoandamana naye kisimani Msera. Time alitoa kauli ya unyonge zaidi kwa kusema kuwa:

> *Tazama baba, umeifanya nini ile konde ya muhogo na migomba? (uk 46).*

Ukarimu wa Soud unamfanya Mkamandume kujutia matendo yake maovu ya awali. Mkamandume alijipata katika njia panda aliposhindwa kulipa bili ya shilingi themanini na tano elfu, mia tano sabini na mbili baada ya kula vyakula na vinywaji hotelini. Mkamandume alikataa kata kata kulipa akidai kuwa ilikuwa ni mali ya wananchi hali iliyomtia taabani. Soud alimwokoa kwa kumlipia bili yake yote. Mwandishi anadai kuwa:

> *Soud alijitolea kumlipia naye Mkamandume akabaki kushangaa. Naam ndiye Soud, katokea wapi? Kashuka kutoka wapi? Mbinguni? Soud kaja tena kumwokoa katika mzozo mwingine? (uk. 144).*

Tukio hili linamtatiza sana Mkamandume kimawazo kwa kuwa hakutarajia wema kama huu kutoka kwa Soud.

Mkewe Mkamandume, Tufaa alijutia mabadiliko aliyoyashuhudia kwa mumewe katika ndoa yao. Alishangazwa na namna mumewe alivyobadilika na kukosa upendo aliokuwa nao siku za awali. Msimulizi anaeleza kuwa:

> *Tufaa alikumbuka namna mumewe alivyompenda zamani. Anadai kuwa mapenzi hayo yalitoweka na sasa analazimika amridhi mumewe zaidi kuliko alivyomridhi tokea kufungamana naye (uk 17).*

Suala hili linachangia ugomvi katika ndoa ya Mkamandume. Hali inayosababisha chuki na uhasama miongoni mwa jamaa wa Mkamandume. Upendo na uhusiano bora unakosekana baina ya mume na mke na pia wazazi na watoto. Bi Tufaa, mkewe Mkamandume anaishi kwa hofu na masikitiko nao wanawe wanakosa uhuru wa kufanya maamuzi yao. Time alikuwa na machungu ya kutengwa na mama pamoja na dadake. Jambo hili lilimfanya Time kulia ndani kwa ndani kutokana na ubaguzi anaofanyiwa na mamake.

> *Kila siku alimpendelea Viwe waziwazi. Time alishangazwa vipi mama aliweza kumchukia mwana aliyemzaa mwenyewe! (uk 108).*

Ubaguzi huu ulimfanya Time kujichukia na kujuta kuwa mtoto wa familia ya Mkamandume. Bete rafikiye Fikirini, anapompachika mimba Viwe anamsababishia mawazo chungu nzima kutokana na ujauzito. Baada ya kupachikwa mimba, Viwe anasema kuwa:

> *Tokea siku ya mwanzo, macho ya Bete yalijaa ulaghai. Kwa nini Viwe alidanganyika? Aligundua maneno yake yalijaa uwongo, hakujua kwa nini alimwamini? (uk 98).*

Kulingana na jamii yao mwanamke aliyeolewa tu ndiye aliyepaswa kuwa mjamzito. Viwe alikumbwa na wasiwasi na kwa kuwa aliogopa wanajamii pamoja na babake. Mwandishi anasema kuwa:

> *Lakini leo mimba imekuwa mzigo kwa Viwe. Imekuwa balaa na kwa hivyo lazima aifiche au aiharibu ikiwezekana (uk 99).*

Hali hii inamlazimu Bi Tufaa, mamake Viwe kumwendea Bi. Reja shoga yake ili waweze kuiavya mimba ile. Wanapanga njama ya kutekeleza kitendo hicho cha kuhatarisha maisha yake. Bi. Reja anamhakikishia rafikiye kuwa:

> *Basi Viwe tutamchukua kwa kisingizio cha kumchezea unyago, lakini lengo letu ni kumtoa mimba kwa madawa ya kienyeji (uk 103).*

Mpango huu unakosa kufaulu na mwishowe babake Viwe anagundua hali ya bintiye. Anapandwa na hasira za mkizi kisha anamwadhibu kikatili bila kujali ujauzito wake.

Lynch na Robert (1982) wanadai kuwa dhuluma zina athari nyingi katika maisha ya watoto. Wanaeleza kuwa ingawa mtoto anaonekana msahaulivu wa matukio fulani, hukumbuka zaidi vitendo vya dhuluma. Uchungu huo unaweza kusababisha huzuni isiyoisha moyoni mwake. Dhuluma za kitabaka zinawaathiri watoto pakubwa. Mkamandume anajuta anapogundua masaibu aliyopitia bintiye, Viwe kutokana na ukatili aliomtendea alipokuwa mjamzito. Baada ya kumfukuza bintiye alikaa kwa muda mrefu kisha akaanza kuwaza kumhusu na kumtafuta alikokuwa ameenda. Alisafiri hadi eneo la Mkomavu alipokutana naye. Mwananwe alimsimulia masaibu yaliyomkumba alipotimuliwa nyumbani kwao. Alipotoka Msera alikumbana na maisha magumu kule lakini akastahimili. Mwandishi anasimulia kuwa:

> *Alipoingia jijini alikuwa mjamzito na jiji lilimkaribisha kwa uzito mkubwa zaidi kuliko ule wa tumboni! Hakujua aende wapi, hakujua afanye nini* (467).

Alilazimika kutafuta kazi, akakodisha chumba na pia akajifungulia biashara. Alifaulu kuendelea na masomo yake na alipofaulu vizuri alijiunga na Chuo Kikuu na akapata Digrii

ya mwanzo. Mkamandume alimwomba msamaha kwa ukatili aliomtendea bintiye kutokana na kosa ambalo lilikuwa la kusamehewa. Pia anasikitika kwa kufeli kumwelekeza mwanawe kwa njia inayofaa kama mzazi.

Ngugi wa Thiongo (1982) katika riwaya ya *Shetani Msalabani* pia anaangazia wahusika wanaokumbwa na majuto. Wariinga ambaye ni mhusika mkuu katika hadithi hii anajutia kufanya uhusiano wa kimapenzi na Tajiri wa Ngorika ambaye anampachika mimba na kumtema. Wariinga anajilaumu kwa kushawishika kuingia katika uhusiano wa kimapenzi akiwa bado mchanga. Aliwazia mambo mengi akajaribu kuavya mimba hiyo lakini haikuwezekana. Mwishowe, alijaribu kujiua lakini akaokolewa na msamaria mwema. Alilazimika kukatiza masomo yake ili kulea ujauzito.

Wangari anajuta kwa kuamua kuhamia jijini kwenda kutafuta kazi. Alipokuwa kijijini alitamani kuhamia mjini kuliko na raslimali na miundo misingi bora. Aliamini kuwa ajira mjini ilipatikana kwa urahisi. Katika harakati za kutafuta kazi, alishikwa na kutiwa ndani kwa kushukiwa kuwa mwizi. Anasimulia kuwa*:*

> *Moja kwa moja nilisukumwa ndani ya gari la polisi. Nilipelekwa kwenye kituo cha polisi nikatiwa katika kitundu (uk 41).*

Baada ya kufungiwa kitunduni kwa siku tatu alipelekwa mahakamani na kushtakiwa kwa mambo mawili; kudhaniwa wizi na uhuni.

### 3.8 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia athari za dhuluma za kitabaka katika riwaya za *Mkamandume* na *Shetani Msalabani*. Tumebainisha lengo kuu la utafiti ambalo ni kuchunguza athari za dhuluma za kitabaka katika riwaya teule. Athari ambazo zimebainishwa ni; ukosefu wa mahitaji ya kimsingi, ukosefu wa ajira, kuuawa kwa wanyonge, kutengwa kwa wanyonge, uhasama baina ya wahusika, utengano wa kifamilia na majuto. Tumeonyesha namna wahusika wa tabaka la chini wanavyoathirika na dhuluma za kitabaka. Wahusika hawa ni wenye mapato ya chini kwa hivyo hawana nguvu za kiuchumi.

Nadharia ya uhakiki wa ki-Marx imetumika kuonyesha namna tabaka la juu linavyowanyonya wanyonge wa tabaka la chini. Tabaka nyonyaji ndilo linalomiliki nyenzo zote za uzalishaji mali na huwa na uwezo mwingi kiuchumi. Kwa upande mwingine tabaka la chini ndilo la wengi wasiomiliki chochote ila jasho lao na nguvu zao ambazo wanaziuza kwa wenye mali ili wayakidhi mahitaji yao. Utengano mkubwa unajitokeza baina ya matajiri na maskini ambapo wanyonge wanaishi katika mazingira duni ya uchochole. Wanakosa mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, matibabu, mavazi na makazi. Pia wanatengwa na raslimali muhimu ya kuwainua kimaisha. Hali hii imechangia masaibu mengi miongoni mwao. Sura inayofuata imeshughulikia mbinu wanazotumia wanyonge kujikomboa kutokana na dhuluma za kitabaka.

# SURA YA NNE

# MBINU WANAZOTUMIA WANYONGE KUJIKOMBOA KUTOKANA NA DHULUMA ZA KITABAKA

## 4.0 Utangulizi

Katika sura ya tatu tumebainisha athari za dhuluma za kitabaka miongoni mwa wahusika wa riwaya teule. Athari tulizoziangazia ni; utengano wa kifamilia, ukosefu wa mahitaji ya kimsingi, ukosefu wa ajira, uhasama baina ya wahusika, kuuawa kwa wanyonge, kutengwa kwa wanyonge na majuto. Tulibainisha kuwa athari hizi zinazowaathiri wanyonge katika jamii zinatokana na dhuluma kutoka kwa tabaka nyonyaji linalomiliki nyenzo za uzalishaji na usambazaji wa mali.

Katika sura hii, tumechunguza mbinu wanazotumia wanyonge kujikomboa dhidi ya dhuluma za kitabaka. Mbinu hizi zimeangazia namna wahusika wanyonge wanavyojikomboa kisiasa, kielimu na kiuchumi. Baadhi ya mbinu wanazotumia wahusika wanyonge kujikomboa ni kama vile; kupitia kufanya maandamano na migomo ya wafanyakazi, kuelimika kwa wahusika wanyonge, kuanzisha biashara ili kujikimu kimapato na uandishi wa vitabu vya fasihi kama vile; tamthilia, ili kuwazindua wanajamii kwa kumulika dhuluma zinazowakumba wahusika wa tabaka la chini.

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya uhakiki wa ki-Marx iliyoasisiwa na Karl Marx na Fredrich Engels (1959). Tumezingatia mhimili unaosisitiza kwamba ubepari kama njia ya uzalishaji mali utaharibiwa na kuvunjiliwa mbali na wafanyakazi wa tabaka la chini au wenyewe utaishia kujiangamiza kutokana na mbegu za maangamizi zinazozisheheni. Kutokana na mhimili huu tumeonyesha namna ambavyo wanyonge katika riwaya teule wanajiimarisha kiuchumi na kujikomboa kutokana na dhuluma wanazopitia.

## 4.1 Ukombozi wa kisiasa

Suala la ukombozi wa kisiasa limeangaziwa pakubwa na waandishi wa riwaya teule. Dhuluma za kitabaka zimesababishwa na uongozi mbaya unaomilikiwa na mabwenyenye kutoka tabaka la juu. Kutokana na tamaa na ubinafsi wa viongozi walio mamlakani wamejinyakulia mali nyingi ya umma na kuwatenga wananchi wa tabaka la chini waliowachagua. Hali hii imesababisha utengano baina ya tabaka la juu na la chini kwa misingi ya kiuchumi.

Kutokana na dhuluma zinazowakumba wananchi wanyonge kutoka kwa tabaka nyonyaji linalotawala, nia ya kujikomboa kwa wahusika wanyonge inajitokeza na kushika kasi. Kimeu (2006) anadai kuwa ukombozi wa kisiasa ni hali ambapo taifa au hata jamii hujaribu kujinasua kutokana na minyororo ya ukoloni hasa kupitia kupigana vita na wakoloni. Katika riwaya teule wanajamii waliodhulumiwa walipigania mapinduzi ya kisiasa kabla ya uhuru na hata baada ya wao kupata uhuru.

Katika riwaya za *Mkamandume* na *Shetani Msalabani,* wanajamii wa tabaka la chini wanaungana pamoja na kuwaondoa mamlakani viongozi katili wanaomiliki mfumo wa ubepari wa uzalishaji na usambazaji wa mali. Mfumo huu ulitumika kuwanufaisha matajiri wa tabaka nyonyaji pekee ilhali wahusika wanyonge hawakufaidika licha ya kudhulumiwa kazini kwa lengo la kuzalisha mali zaidi. Hali hii ilisababisha utengano mkubwa baina ya matabaka, jambo lililowachochea wanajamii kupigania mapinduzi. Ukombozi wa kisiasa katika riwaya teule unajitokeza kabla ya uhuru na baada ya uhuru.

### 4.1.1 Kabla ya uhuru

Vita dhidi ya mkoloni vilitokana na masuala mengi yaliyowaathiri Waafrika katika mazingira walimoishi kutokana na riwaya teule. Masuala haya ni kama vile; ubinafsi wa

waliokuwa mamlakani, ukosefu wa usawa wa raslimali katika tabaka la juu na chini, ubaguzi kwa misingi ya rangi na unyakuzi wa mashamba ya Waafrika. Ushahidi unajitokeza katika riwaya teule.

Katika riwaya ya *Mkamandume* mwandishi ameonyesha namna Waafrika wanavyoshirikiana kupigania ukombozi wao wa kisiasa kutoka mikononi mwa Wazungu waliowadhulumu. Utengano uliokuwepo baina ya Wazungu na Waafrika ulichangia mapinduzi ya kisiasa. Waafrika walidhulumiwa na wazungu waliojiona bora zaidi. Kupitia kwa mazungumzo kati ya Soud na Nadia tunafahamu namna Wazungu walivyowadhulumu Waafrika. Soud anaeleza kuwa:

> *Afrika au Waafrika ni maskini na hawajafanya maendeleo ya maana kwa sababu wamenyonywa kwa muda mrefu na wanaendelea kunyonywa (uk 149).*

Pia, suala hili linajitokeza wakati ambapo mzee Mkasi anakumbuka namna alivyoungana na wengine kupigania mapinduzi. Katika vita vya ukombozi wa nchi ya Malelejimema mzee Mkasi alidhulumiwa kutokana na msimamo wake. Alishiriki katika mwenendo wa nchi kwa sababu alitaka sana nchi yake ijikomboe iendeshwe na watu wake wenyewe. Hali hii ilimsababishia masaibu mengi. Anaeleza kuwa alichukuliwa kama gunia la makaa na kuwekwa kizuizini. Alisingiziwa kuwa ameitukana bendera na kula njama ya kuleta mafuriko nchini:

> *Baada ya hapo n ilikamatwa nikaambiwa nimeshiriki katika magendo ya karafuu. Adhabu yake ni kifo. Sikuuliwa. Niliachiliwa baada ya mateso mabaya (uk 187).*

Kutokana na ukatili huu alibadili msimamo wake wa kimaisha. Aliamua kuzamia shughuli za kilimo ili kujipatia mahitaji yake ya kimsingi.

Mkamandume anakumbuka wakati wenyeji wa Malelejimema walinyang'anywa ardhi na baadhi ya wageni. Walilazimishwa kulipia kodi viwanja ambavyo havikuwa vyao. Mwandishi anadai kwamba:

> *Makazi ya wenyeji yalisokomezwa ng'ambo zaidi hadi mashamba kaskazini, kusini, mashariki na magharibi. Na hata huko iliwabidi walipie kodi za viwanja vilikuwa si vyao (uk397).*

Kutokana na dhuluma walizopitia, Waafrika waliamua kumwondoa mkoloni kwa matarajio kuwa hali ingekuwa bora kuliko jinsi ilivyokuwa wakati huo. Waafrika walitarajia kuwa baada ya kumwondoa mkoloni, yale majumba mazuri na miji ingekuwa yao. Kwa hivyo, waliamua kushiriki katika vita vya kimapinduzi. Waafrika walihamasishwa kuhusu umuhimu wa kumwondoa mkoloni. Wengi wa waafrika walishawishika kuwa palikuwa na haja ya kumwondoa mkoloni. Mwandishi anadai kuwa:

> *Mkamandume aliamini vita vile vilikuwa halali na vya manufaa kwa wote (uk.20).*

Hali hii ilimpa motisha ya kuungana na wengine kutetea haki za wanajamii.

Waafrika walijitolea kwa vyovyote vile kupigania mapinduzi katika jamii yao. Vijana walijitolea kwa nguvu zao zote wakati wa kupigania mapinduzi. Walitimka mbio kutoka kijiji kimoja hadi kingine kwa lengo la kueneza chama chao na kueneza habari za mapambano. Walijitolea kwa hali na mali wakasahau nyumba zao na watoto wao. Usiku na mchana walikuwa katika huduma za chama. Miongoni mwa vijana hawa walikuwemo:

Mkamandume, Silima na Suguru. Wakati huo walikuwa bado na nguvu za ujana na ari ya kuikomboa nchi yao. Hawa watatu walishiriki kikamilifu katika vita hivi. Licha ya kuwahamasisha Waafrika wengine, walikuwa katika mstari wa mbele katika kuwaua wageni waliokuwa wakiwadhulumu Waafrika wa tabaka la chini.

Riwaya ya *Shetani Msalabani* pia inaonyesha namna wanajamii wanavyojikomboa kisiasa. Wariinga anasimulia namna wazazi wake walivyoshiriki katika vita dhidi ya mkoloni. Vita hivi vilichangia masaibu mengi kwa Wariinga na familia yao. Wakoloni waliwadhulumu waafrika waliokuwa wakipigania uhuru. Mwandishi anasema kwamba:

> *Walipoona ya kuwa walikuwa karibu kushindwa na mashujaa wa Mau Mau walianza kuwanyanyasa na kuwadhulumu wafanyakazi na wakulima wadogo humu nchini (uk 145).*

Wazazi wa Wariinga walishikwa na kutiwa gerezani na walipotolewa mwaka wa 1960 walipata shamba lao limenyakuliwa na kuuziwa wasaliti wa serikali ya kikoloni. Hali hii ilichangia wao kuishi maisha duni ya ufukara.

Wangari pia anasimulia namna alivyoshika bunduki kupigania uhuru wa wanajamii. Akiwa na wenzake garini wakielekea Ilmorog Wangari aliwasimulia namna alivyoshirikiana na kundi la Mau Mau kupinga dhuluma na ukatili. Anasema kuwa:

> *Ushirikiano wa wasaliti na wa beberu ulikuwa wa kinyama kwani haukujali utu. Haukujali watoto wasiojiweza. Yeye alijitolea kuikomboa nchi yake (uk 37).*

Alidhihirisha uzalendo wa kweli kwa kujitokeza kwa hali na mali ili kuipigania nchi yake na kuwakomboa wanajamii.

### 4.1.2 Baada ya Mapinduzi

Baada ya kujipatia uhuru, wanajamii wa riwaya teule hawakufaidika walivyotarajia. Mali ya wakoloni ilichukuliwa na kugeuzwa kuwa mali ya serikali. Wale waliokuwa uongozini ndio waliojinyakulia mali ya umma bila kuwajali wenzao wa tabaka la chini. Hali ngumu zaidi ya kiuchumi ilishuhudiwa kutokana na ukosefu wa chakula. Mkamandume anadai kuwa:

> *Nilishiriki katika mwenendo wa nchi kwa sababu nilitaka sana nchi yangu ijikomboe, iendeshwe na watu wake wenyewe. Lakini nilitaka wanaotuongoza waiweke mbele Malelejimema kuliko maslahi yao (uk 184).*

Wanajamii wanakosa imani na watawala walio uongozini hali inayowachochea kupigania ukombozi wa pili dhidi ya Waafrika wenzao waliowadhulumu.

Osango (2015) akimnukuu Nyerere (1968), anaeleza kuwa *Azimio La Arusha* lilikuwa na lengo la kuleta usawa na heshima miongoni mwa wananchi wa Tanganyika. Yaani kushirikiana katika kutumia mali inayotokana na juhudi za wananchi na kuwepo kwa kazi kwa kila mtu ili unyonyaji ufutiliwe mbali. Ili kutekeleza haya kwa urahisi, watu walipelekwa kwenye vijiji vya ujamaa ambapo waliishi kwa pamoja. Licha ya juhudi hizi maisha ya wanajamii hayakubadilika kutokana na ubinafsi wa viongozi waliokuwa mamlakani. Hali hii pia inajitokeza bayana katika visiwa vya Zanzibar. Katika riwaya ya *Mkamandume***,** viongozi waliopewa nafasi za uongozi waliwadhulumu wanajamii. Kwa mfano; Katibu mkuu wa chama tawala ambaye kisirisiri huitwa bwana Chochote kwa tabia yake ya kutaka chochote hata kabla ya kufanya chochote aliwadhulumu wanajamii kazini. Mwandishi anaele za masaibu ya wanajamii anaposema:

> *… na mtu atake asitake, angekwenda kumsujudia kwa huduma za lazima; kuoa, kuolewa, kufa, kuzikwa, kujenga, kubomoa, kusafiri na kurudi, kuuza na kununua hiki na kile. Mradi bwana Chochote hudhibiti maisha ya kila mtu mikononi mwake (uk 114*).

Kamunde (1983) anasema, mifumo itumiwayo kuwadhalilisha wanyonge ni; siasa, uchumi na masuala ya jamii. Kulingana naye kiini cha uovu ulimwenguni ni; mali, cheo, madaraka, ubinafsi, uroho, chuki na kadhalika. Hali hii hutokea katika jamii ambapo mifumo ya siasa, uchumi, jamii na utamaduni imemilikiwa na watu wachache katika jamii. Anasisitiza kuwa hapatakuwa na amani mpaka matabaka ya kijamii yatakapovunjwa na kupondwapondwa na haki zitakapotambuliwa. Hali hii inajitokeza bayana kupitia kwa wahusika mbalimbali katika riwaya za utafiti.

Ajira serikalini ilitolewa kwa misingi ya ukabila jambo ambalo liliwakera wanajamii waliopigania mapinduzi. Kwa mfano; Meneja wa Shirika la Biashara alikuwa mwanawe mwenyekiti wa chama tawala na mwakilishi wa jimbo la Kaskazini. Hakupewa cheo hicho kwa sababu ya uwezo wake bali kwa sababu ya babake. Mwandishi anasema kuwa:

> *Jengine ni la mwanawe mwenyekiti ambaye ni Meneja wa Shirika la Biashara-Cheo alichopewa si kwa uwezo, ujuzi au busara bali kwa sababu tu alikuwa mtoto wa mwenyekiti wa chama na mwasisi (uk 114).*

Vilevile, katika riwaya ya *Shetani Msalabani* ajira kwa wananchi ilitolewa kwa njia ya mapendeleo sana. Waliotoka kijijini kutafuta kazi jijini walitatizika sana kwa kuwa hawakumfahamu mtu yeyote aliye ofisini. Jacinta Wariinga anakumbana na hali ngumu anapoenda jijini kutafuta ajira. Mwishowe, Wariinga alipata kazi kwa Boss wake Kihara

ambaye alimlazimisha wafanye mapenzi naye lakini akakataa katakata. Hali hii ilimkera Kihara na akaamua kumpiga Wariinga kalamu. Alimweleza kuwa:

> *Siku hizi yaonekana wazi kuwa hutaki kazi. Naona vizuri nikuruhusu ufanye linalokupendeza. Afadhali uende nyumbani kwanza. Ukiwa na haja ya kazi kama wasichana wengine, sikukufungia mlango (uk 21).*

Masaibu haya yalimchochea Wariinga kusimama kidete na kupigania haki zake. Aliungana na wafanyakazi wengine waliokuwa wamedhulumiwa na kujikomboa kwa kuyafichua maovu yanayotendeka maofisini.

Hali hii ndio iliyokuwa kichocheo cha kupigania ukombozi dhidi ya viongozi Waafrika walioendeleza dhuluma kwa wenzao. Kutokana na kuendelea kudhulumiwa kwa wanajamii wanyonge hata baada ya kujipatia uhuru, nia ya kujikomboa tena ilishika kasi miongoni mwa wachochole. Kundi la tabaka la chini liliungana ili kuwaondoa Waafrika wenzao wa tabaka nyonyaji.

**4.2 Ukombozi wa kiuchumi**

Kwa mujibu wa nadharia ya ki-Marx, historia ya maisha ya binadamu inaweza kuelezeka katika misingi yakinifu ya kiuchumi ambayo itachunguza njia za uzalishaji mali hizo pamoja na miundo ya kiuchumi na pia huathiri uzalishaji na usambazaji wa mali hizo. Kumilikiwa kwa mbinu za uzalishaji mali na tabaka nyonyaji huendeleza dhuluma za kitabaka kwa wanyonge wa tabaka la chini ambao hutumika tu kuzalisha mali kwa manufaa ya watu wachache.

Ngugi wa Thiong'o (1986) kupitia kwa wahusika Wariing'a na Gatuiria anaeleza jinsi wanavyoikomboa jamii yao kiuchumi kutokana na dhuluma za kitabaka. Babake Gatuiria

alikuwa tajiri sana aliyemiliki maduka mengi na mashamba makubwa sana. Alikuwa na biashara nyingine nyingi za kuagiza na kupeleka vitu Ulaya.  Alisafirisha bidhaa nyingi kwa Eropleni. Yeye ndiye aliyekuwa mwanawe wa pekee. Licha ya utajiri wa babake Gatuiria anajitenga naye kutokana na dhuluma dhidi ya wafanyakazi wanyonge waliokuwa wameajiriwa kwao. Gatuiria hakusita kufichua maovu aliyoyatenda babake. Anasema kwamba:

> *Kutoka zamani sikupendelea kufuata mienendo ya baba. Wafanyakazi wao walikula chakula duni na kuvaa matambara. Mara kwa mara babangu aliwapiga bakora huku akiwatukana vibaya na kuwaita ng'ombe (139).*

Kutokana na ukatili huu Gatuiria anajitenga na babake na anapotoka kwao anakutana kisadfa na mzalendo Wariinga kule jijini. Baada ya kuchumbiana wanashirikiana kupigania ukombozi wa kiuchumi katika jamii yao. Wanaonekana mstari wa mbele kuwazindua wanajamii na kuwaongoza katika kukabiliana na mabepari, akiwemo babake waliokuwa wakiwadhulumu wanyonge.

Ndoa kati ya Gatuiria na Wariinga inachangia ukombozi wa kiuchumi kutokana na kushirikiana kwa wazalendo hawa kuwaangamiza mabepari waliokuwa wanawanyonya maskini bila kujali. Siku ya harusi yao ilibainika kuwa babake Gatuiria ndiye aliyekuwa tajiri wa Ngorika. Tajiri ambaye alimpachika mimba na kumtema alipokuwa mwanafunzi wa shule ya upili kule Nakuru. Alijaribu kupinga ndoa hiyo kwa kumshawishi Wariinga kwa mali nyingi ya dhamani lakini ombi lake linakataliwa vikali. Kwa hamaki, Wariinga anampiga risasi tatu za kichwa na kumwangamiza papo hapo. Pia, anawaangamiza mabepari Kihaabu wa Gatheeca na Gitutu wa Gatanguru waliokuwa wamehudhuria

sherehe hiyo ya harusi. Huu unakuwa ni mwamko mpya kwa kizazi kipya kutokana na kuvunjiliwa mbali kwa tabaka nyonyaji la mabepari.

Eagleton (2011), anadai kuwa unyonyaji wa kibepari ni mfumo wa ulaji, ukandamizaji na anaushutumu vikali. Kutokana na viwango vya chini vya ujira waajiri wa kibepari hutofautiana na wafanyakazi wa kiwango cha chini wanaojaribu kupigania haki zao. Hali hii huchangia mapinduzi ya ki-Marx. Tabaka la juu ambalo ni nyonyaji linawatenga wanyonge kwa misingi ya kiuchumi. Wanyonge wanaungana pamoja kupigania ukombozi wao wa kiuchumi.

Katika riwaya ya *Shetani Msalabani,* mwandishi ametuchorea picha halisi ya namna tabaka la juu linavyowanyonya maskini kupitia kwa ushahidi uliotolewa kule Ilmorog wakati wa mashindano ya wizi na unyang’anyi. Mashindano haya yalichangia ukombozi wa kiuchumi kwa sababu mabepari wanafichua mbinu dhalimu walizotumia kujinyakulia mali huku wanyonge wakidhulumiwa.

Ushahidi wa Nditika wa Nguji unadhihirisha wazi kuwa alikuwa wa tabaka la juu. Alikuwa na mwili wa jitu la miraba minne mwenye mavazi ya bei ghali na magari mengi ya kifahari. Watoto wake walisomea shule ya kifahari ya *Nairobi Highclass Riding School.* Walifundishwa kupanda farasi.

Kutokana na ushahidi wa mabepari kuhusu namna walivyowanyonya wanyonge wa tabaka la chini wazalendo waliokuwa wanafuatilia matukio yote wanajitokeza kujikomboa kiuchumi. Wazalendo walikusanyika kumsikiliza Muturi aliyekuwa kiongozi wao. Anasema kuwa:

> *…na sisi wafanyakazi hujenga nyumba wengine wakaingia kujisitiri kwa baridi, mvua na jua na sisi wajenzi tukaachwa nje. Hushona nguo wengine wakazivaa na sisi tuliozishona tukavaa matambara. Hulima chakula, wengine wakakila na sisi tukalala njaa. Tazameni sisi hujenga mashule mazuri, watoto wa wengine wakasomea humo nao watoto wetu wakaenda kuzurura wakitafuta chakula mapipani (uk 221).*

Nadharia ya ki-Marx inasisitiza kuwa Ubepari kama njia ya uzalishaji mali utaharibiwa na kuvunjiliwa mbali na wafanyakazi wa tabaka la chini au wenyewe utaishia kujiangamiza kutokana na mbegu za maangamizi zinazosheheni. Baada ya hotuba ya Muturi kulishuhudiwa makabiliano makali baina ya wazalendo na Mabepari. Tayari Wangari alikuwa amewafahamisha Polisi kuhusu mabepari waliokuwa wamejumuika Ilmorog kwa mashindano ya unyang'anyi. Baadhi ya mabepari waliuawa na wengine wakatiwa gerezani. Hali hii iliashiria kuvunjiliwa mbali kwa tabaka nyonyaji lililokuwa limemiliki nyenzo za uzalishaji mali. Hali hii inaleta matumaini kwa wanyonge ambao walikuwa wametengwa katika jamii.

Ukombozi wa kiuchumi pia umejitokeza katika riwaya ya *Mkamandume.* Mwandishi anafafanua sababu zinazochangia wananchi kuungana na kupigania ukombozi wa kiuchumi. Hali ya uchumi ilidorora pakubwa hasa baada ya kujipatia uhuru kutokana na uongozi mbaya wa Waafrika. Viongozi katika Malelejimema waliegemea tu katika sehemu za mjini ambako tabaka lao lililo na kipato liliishi. Kinyume na tabaka tawaliwa linaloishi kijijini lilitengwa na huduma muhimu. Wanajamii wachochole waliishi maisha duni ya kimaskini. Kuzorota kwa uchumi kulishuhudiwa kupitia kuporomoka kwa miundo misingi pamoja na sekta za usafiri.

Mashamba yaliyonyakuliwa kutoka kwa wageni hayakuwafaa wananchi wa kawaida kwa vyovyote. Yale yaliyokuwa na rotuba nzuri yalinyakuliwa na viongozi ambao hawakuyatunza jinsi ilivyostahili. Mwandishi anasema mashamba yote yameota magugu, minazi imeparama, mikarafuu imesibiwa na maradhi yasiyopata kusikika. Kwa upande mwingine, wananchi wamekosa ardhi ya kulima. Licha ya kukosa ardhi, vile vishamba vidogo ambavyo wanamiliki haviwezi kuzaa mazao yoyote kwa sababu ya kukosa rotuba na kutokana na magonjwa ambayo hayana dawa.

Masaibu haya ndiyo yaliyokuwa chanzo cha ukombozi wa kiuchumi. Wanajamii wa tabaka la chini wakiongozwa na Mkamandume walishirikiana ili kuwaondoa viongozi wenye tamaa na ubinafsi mamlakani. Kuondolewa kwao kulisaidia katika kusambaratika kwa tabaka nyonyaji lililokuwa linamiliki nyenzo za uzalishaji na usambazaji mali.

Ngara (1985) anasema kuwa, katika jamii yenye matabaka, nguvu za kiuchumi huwa na watawala ambao huhodhi nyenzo za uzalishaji mali. Hali hii inashuhudiwa katika nchi ya Malelejimema ambapo uchumi ulivurugwa wakati mkoloni alipoingia mamlakani. Kabla ya kuja kwa mkoloni wanajamii walitegemea kilimo na uvuvi kwa mahitaji yao. Wakoloni walipofika walijinyakulia mashamba ya waafrika. Wenyeji walilazimika kufanya kazi ya vibarua katika mashamba ya mikarafuu. Aidha baada ya viwanda kadhaa kujengwa visiwani, watu walihamia mijini na kuanza kufanya kazi katika viwanda hivyo. Hii ilikuwa njia moja ya wakoloni kuhakikisha kuwa Waafrika walikuwa wategemezi wao. Kwa kufanya hivi lengo lao lilikuwa kuendeleza utabaka katika jamii.

Baada ya mapinduzi ya mwaka wa 1964 katika Taifa la Zanzibar, wananchi walitarajia kuwa nafasi za kazi zingepatikana kwa wingi. Waafrika walitarajia kuwa uongozi ukiwa mikononi mwao suala la ajira litashughulikiwa ipasavyo. Pia changamoto walizopitia ya

mazingira duni kazini itaboreshwa vilivyo. Jambo hili halikutimizwa kwani tunawaona vijana wengi ambao wamemaliza vyuo lakini hawana ajira kwa kipindi kirefu. Soud ni kijana ambaye amesomea uanasheria lakini kwa sasa miaka minane imepita bila ya yeye kuajiriwa au kujiajiri mwenyewe. Ni ukosefu wa kazi ndio unawafanya wananchi wengi kuendelea kuvumilia dhuluma za wakubwa wao kwani hawakuwa na mahali pengine pa kwenda iwapo wangeziacha kazi ambazo walikuwa nazo.

Baada ya mkoloni kuingia katika nchi za Kiafrika mfumo wa uchumi ulibadilika na watu kuanza kutegemea ajira ili kupata chakula. Hata baada ya mkoloni kuondoka mfumo huu wa kiuchumi uliendelezwa na Mwafrika huku akisahau maisha yake ya hapo awali ya ujamaa. Ni kutokana na mfumo huu ndiposa kazi inakuwa tegemeo kubwa kwa wananchi. Aidha, wananchi hawana mashamba ya kuendeleza kilimo kama ilivyokuwa hapo awali kabla ya kufika kwa mkoloni. Hali hii imesababishwa na baadhi ya Waafrika waliokuwa na tamaa ya kujinyakulia mashamba kama watangulizi wao. Waafrika hawa wamejinyakulia mashamba makubwa huku wakiwaacha wananchi wa kawaida kuangamia katika umaskini.

Wafanyakazi waliobahatika kuajiriwa walikumbana na changamoto si haba kazini. Mkamandume analalamikia mazingira duni ya kazi. Licha ya hayo alifanyishwa kazi nyingi na kulipwa mshahara mdogo. Mwandishi anaeleza kuwa*:*

> *Na kwa kawaida yake huanza kazi ngumu kwanza na kazi ngumu ni ipi zaidi kuliko ya kufagia vyoo vya ofisi hii hasa siku hizi ambapo mara nyingi hakuna maji wala vifaa. Kuvisafisha vyoo bila ya maji, bila ya sabuni. Tena kwa fagio bovu (uk 323).*

Kutokana na ugonjwa uliompata Mkamandume alilazimika kuomba likizo ya miezi mitatu ili aweze kutibiwa. Jambo la kusikitisha ni kwamba serikali ilimpa likizo bila mshahara wowote. Mwandishi anasema kwamba:

> *Barua ilisema wazi kwamba amepewa likizo ya miezi mitatu, lakini wizara ilisikitika sana kwamba haikuwa na pesa za kumpa kwa ajili ya matumizi (uk 332).*

Wafanyakazi wengi kazini walifanyishwa kazi nyingi za sulubu na kukejeliwa kila mara na bosi wao. Mwandishi anadai kuwa:

> *Vicheko vya wafanyakazi wake wengi havikuwa vicheko vya furaha hata chembe. Vilikuwa vicheko vya maumivu. Bosi aliwadunisha wafanyakazi na kuwaona kama wajinga (uk 250).*

Masaibu haya yaliwachochea wafanyakazi na kuwapa ari ya kujikomboa kiuchumi kupitia kwa migomo na maandamano ya kupigania haki zao. Maandamano haya yalichangia kuwepo kwa mabadiliko ya kiuchumi kwa kuwa viongozi waliokuwa mamlakani waliondolewa hali iliyovunjilia mbali tabaka nyonyaji. Baadhi ya wafanyakazi kama vile Viwe, wanaamua kuanzisha biashara ili kujiimarisha kiuchumi. Hali hii iliwazindua wanajamii kutokana na mapato yaliyoboresha maisha yao na pia kuimarisha uchumi wa nchi. Mzee Mkasi pia anajikakamua katika suala la kilimo. Baada ya kutengwa, alizamia kilimo katika konde lake. Mimea ilinawiri, alipata mazao na mapato ya kutosha ya kujikimu kimaisha.

Mapinduzi yanashuhudiwa kupitia kwa maandamano ya wanamalelejimema. Siku ya maandamano ilidhihirisha moto uliokuwa umewaka na ingekuwa vigumu kuuzima moto

huo tena. Licha ya kuwa siku ya kazi, watu wachache sana walienda kazini. Wakulima walidinda kuyapeleka mazao sokoni, wavuvi hawakwenda kuvua baharini kwa hivyo hakukuwa na hata kidagaa sokoni, magari yalikuwa yakienda na kurudi kwa wingi huku yakiwasomba watu kutoka vijijini yakiwapeleka mjini kwenye maandamano. Kote kulikuwa kumejaa watu wazima, watoto wa shule, vijana na wazee. Watu walipangana na kushikana mikono kuonyesha umoja wao.

Baadhi yao walibeba bendera ya nchi huku wakilaani maovu ya viongozi wao. Maandamano hayo yalijumulisha kila mtu. Waliokuwa maadui hapo awali, siku hiyo walikuwa pamoja katika mapambano.  Mkamandume tena alikuwa mstari wa mbele katika mapinduzi ya pili. Kwanza, aliamua kumfyeka Mzee Shombe ambaye alikuwa akishirikiana na serikali kuwanyanyasa Wanamalelejimema kisha akamfyeka Mtemi ambaye hapo awali alikuwa boss wake. Aidha hakujali kile angekabiliana nacho baada ya kuwaua watu hawa ila alikuwa mstari wa mbele katika mgomo.

Kila mara panapokuwa na mapinduzi, hapakosi kuwa na wale ambao wanajeruhiwa na kupoteza maisha yao. Wakati polisi walifyatua risasi ovyo ovyo, risasi hizo ziliwapata watu kadha wakiwemo: Mtumwa, Mzee Mponda na Mkamandume. Kwa mara nyingine Mkamandume anashiriki katika vita vya ukombozi lakini wakati huu anauawa. Hata hivyo alipokuwa akiaga dunia alijua kuwa mapambano yataendelezwa na wanawe ambao walikuwa tumaini la kesho.

Bila ya kutarajia wala kuamini walishtukia risasi zikafyatuliwa na watu kadha waliokuwa wamekamatana pale mstari wa mbele walianguka chini, damu rovurovu. Mwandishi anasema kuwa:

> *Mmoja wao alikuwa Mkamandume ambaye risasi ziporushwa, alijichoma mbele ya Soud kumkinga nazo. Aaaaa, hayakuwa maandamano tena. Fujo, mtafaruku, kelele, ghasia, msukumano, mbio, taharuki na hofu imeganda usoni… wengi zaidi walikuwa wamemzunguka Soud kujaribu kumkinga na kumtorosha. Hawa walikuwa wanaitazamia kesho (uk 487).*

Kutokana na muktadha huu ni wazi kuwa chuki zilizokuwepo hapo awali miongoni mwa wananchi ziliwekwa kando kwani Mkamandume aliyekuwa hasidi wa Soud ndiye aliruka mbele ya Soud ili kumkinga kutokana na risasi kwa matarajio kuwa yeye akiwa kijana ataendeleza harakati za ukombozi iwapo siku hiyo hakungekuwa na mafanikio ya mapinduzi. Mwandishi anafaa kuonyesha matumaini ya kesho katika kazi zake. Mwandishi wa riwaya ya *Mkamandume*, amefaulu kuonyesha kuwa kuna matumaini anapomtumia mhusika Mkamandume kumkinga Soud ambaye ni kijana, anafanya hivi ili kuonyesha kuwa hata kama kizazi kilichopo cha wazee kinaangamia bado kuna vijana ambao wataendeleza harakati za kuleta mabadiliko katika jamii ya mwandishi.

### 4.3 Ukombozi wa kielimu

Suala la elimu huwapa mwanga wanajamii na kuwafichulia haki zao za kimsingi jambo ambalo huwazindua katika kupigania ukombozi wao. Katika riwaya teule waandishi kupitia kwa wahusika mbalimbali wameonyesha namna elimu imechangia ukombozi katika jamii husika. Kuimarishwa kwa viwango vya elimu pamoja na kuelimika kwa baadhi ya wanajamii kumechangia mapinduzi kwa wanajamii. Wakombozi wamepata maarifa na mwelekeo unaofaa katika kupigania usawa kutokana na dhuluma za kitabaka. Kupitia kwa elimu wanyonge huzinduliwa ili wajue kuwa matatizo waliyonayo ni ya kihistoria kisha huonyeshwa jinsi ya kukabiliana nayo.

Mhimili wa nadharia ya uhakiki wa ki-Marx unadai kuwa historia ya jamii ni historia ya mapambano baina ya matabaka. Marx anasisitiza kuwa matabaka huchangia mapinduzi kwani huzua mikinzano na migogoro kuhusu mfumo dhalimu wa ubepari. Kutokana na haya mageuzi ya kiuchumi na kisiasa hutokea. Kwa hivyo kudhulumiwa kwa tabaka la chini kwa muda huchochea wanyonge kuungana na kupigania ukombozi wao.

Kwanza, katika riwaya ya *Mkamandume***,** tunamwona Nadia akishirikiana na Soud kuandika makala mbalimbali yaliyolenga kuufunua ukandamizaji uliopo Malelejimema. Makala hayo yalichapishwa katika vyombo vya habari vya nje kwa kuwa vyombo vya habari vya ndani havingeruhusu kuchapishwa kwa habari hizo nchini ili wananchi wasifahamu ukweli wa mambo. Wanamalelejimema walipata fursa ya kujionea namna walivyodhulumiwa na tabaka nyonyaji lililokuwa uongozini. Maovu yote yalifichuliwa, hali iliyowazindua wananchi kupigania ukombozi wao.

Wananchi wengi walikuwa wamefahamishwa kuhusu umuhimu wa kusema. Wanawake walikuwa wamezungumziwa kisirisiri kuhusu haki zao za ndoa na hata haki za kila mwananchi. Zaidi ya hayo, hawa wawili walikuwa wamefungua ofisi ya kuwasaidia wananchi kisheria hata ingawa ofisi hii haikuwa imekubalika na serikali. Wahusika hawa walijitokeza kama watetezi wa haki za wanamalelejimema waliokuwa wakidhulumiwa kila mara.

Kutokana na changamoto alizopitia Viwe akiwa mjini, aliamua kurudi shuleni ili kujiendeleza kimasomo. Kwa bahati nzuri alifaulu katika mtihani wa kidato cha sita, kisha akajiunga na chuo kikuu alikofuzu na kupata digrii ya kwanza. Licha ya kuwa na kisomo cha juu aliamua kutotafuta kazi serikalini kwani alifahamu kuwa hiyo ingekuwa kazi ngumu kwa sababu kazi zenyewe zilikuwa adimu na malipo yake pia yalikuwa duni.

Aliamua kufanya biashara yake ambayo ingempa uhuru wa kufanya mambo mengine ya kisiasa. Ni baada ya kuvisoma vitabu vingi vya fani mbalimbali ndiposa alifahamu siasa zote za dunia. Kwa sasa aliweza kutambua kuwa umaskini unasababishwa na binadamu mwenyewe. Aidha, kupitia kwa tamthilia zilizokuwa zikiigizwa, Mkamandume alichukua fursa ya kukifunza kijukuu chake kuhusu umuhimu wa mikinzano na kukihimiza kuona nyuma ya maisha kisha kutazama mbele kwenye maisha yao.

Kijukuu hiki kinawakilisha kizazi kijacho. Kwa hivyo, wazee katika jamii hii walianza kuafikiana na wito wa vijana wa kusafisha ago kabla ya kuondoka kwao. Mwandishi anakitumia kijukuu hiki ili kuwasilisha jamii changa anaposema kuwa*:*

> *Kwa hivyo wazee walikuwa wameamka na sasa walikuwa wanatoa mafunzo kwa vizazi vipya ili visifanye makosa kama yale yaliyofanywa na wazee wao ya kushiriki mapinduzi bila ya kuona mbele* (uk 59).

Mhimili wa nadharia ya uhakiki wa ki-Marx unaeleza kuwa njia ya kusaidia na labda kuharakisha kuangamizwa kwa mfumo wa kibepari ni kudadisi, kukosoa, kushutumu, kulaumu na kufichua dhauluma zilizopo katika itikadi za tabaka la juu zinazoimarisha ubepari. Mwandishi kupitia kwa wahusika anafichua maovu yanayoikumba jamii. Wananchi wanapata ufahamu wa kina kuhusu dhuluma za kitabaka katika jamii husika.

Soud alipohamia jijini, yeye pamoja na Viwe walianzisha harakati za kuwahamasisha vijana kwa kutumia fasihi. Harakati hizi ziliendelezwa na pesa zilizokuwa zikitoka kwa wadhamini na wahisani wema pamoja na pesa zilizokusanywa kutokana na maonyesho ya michezo. Mwandishi anadai kuwa:

> *Harakati hizi sasa zimekuwa kubwa na zinaendeshwa dhahiri. Zinaendeshwa kwa michango mingi ya kujitolea kutoka kwa watu kadhaa miongoni mwao akiwemo; Nadia, mzee Sleyyum, Soud, Viwe na Mkamandume (uk 470).*

Michezo hii iliweza kuwafungua watu wengi macho kwani ndani yake kulikuwa na historia katika ukweli wa maneno ya wahusika kuliko vile maisha yalikuwa yamezoeleka. Ndani ya historia hii, maisha yalikuwa ya mtitimo mtupu ambamo kila mara watu walipotaka kujikwamua walipigwa rungu kali lililowadididimiza chini vibaya.

Licha ya serikali kujaribu kupinga juhudi zao, wanamapinduzi hawakufa moyo. Tayari ujumbe ulikuwa umewafikia wengi kwa hivyo ikawa vigumu kuwadhibiti washirika. Hamasisho la akina Viwe lilikuwa limewavutia vijana wengi na wakati wenye nchi walisikia ujumbe huu harakati hizi zilikuwa zimefikia kilele na wenye nchi walikuwa wamechelewa. Harakati hizi zilikuwa zimesambaa nchini kote. Hali ya wakati huo sasa ilikuwa hatari kwani hakuna aliyeogopa tena wala kuchelea kile ambacho kingetokea. Mwandishi wa riwaya anaelezea hali hii ilivyokuwa kabla ya mapinduzi ya pili. Aanaeleza kwamba:

> *Wasiwasi wa wenye nchi kwa hivyo umeenea pande nyingi. Ilibidi washughulikie mambo makubwa makubwa kwanza. Na wasiwasi huo unatokana na kutowaamini raia wote. Hata miongoni mwa wale wa zamani walioaminika* (uk 477).

Wasiwasi uliojitokeza ulikuwa kama wimbi kubwa la utakatifu linajipinda, tayari kuiangukia nchi wakati wowote ule. Na wenye nchi hawakujua lingelieanza kupiga lini na

upande gani. Licha ya kuwa wananchi walikuwa wamejiandaa walishindwa wataanzia wapi ili waweze kujikinga.

Pia, kupitia kwa michezo ya kuigiza Viwe anawahamasisha vijana kuhusu umuhimu wao wa kuungana na kuwakumbusha wazee walio uongozini kuwa wakati ulikuwa umefika wa mabadiliko. Wazee walistahili kubadilisha mienendo yao ya uongozi mbaya kwa kujali vizazi vya kesho. Katika hotuba yake Viwe anasema:

> *Hii tamthilia isiwe mchezo wa kuigiza tu, iwe tamthilia yenye fikra nzito za ruwaza! Wakati umefika vijana kuyafumbata maisha yetu mikononi mwetu. Tunatoka kugumu, lakini tunakokwenda kugumu zaidi na wazee wetu wameshindwa kutuongoza. Wameshindwa kutuekeleza yapasayo kutueleza (uk 465).*

Vijana walikuwa mstari wa mbele kupigania ukombozi. Tunaambiwa kuwa Viwe aliendelea kuwahimiza vijana waungane ili kuwakumbusha wazee kwamba wao ndio wanapaswa kuwajibika. Alizidi kuwapa ari ya mapinduzi alipowaambia kuwa lazima vijana wawalazimishe wazee kuwaelekeza ipasavyo ili wasiache pengo wakati wanapoondoka. Ukombozi hauwezi kutekelezwa na mtu mmoja bali huwa ni ushirikiano wa kundi la wanajamii.

Ili kuwe na ufanisi wahusika wanafaa kutia kando tofauti zao ili kuwawezesha kufanya kazi pamoja. Kwa muda mrefu, kulikuwa na tofauti kati ya Viwe na babake, Mkamandume. Tofauti hiyo ilitokea wakati Viwe alipatikana kuwa mja mzito. Bila kufikiria, babake alimpiga vibaya nusura amuue. Viwe alipoponyoka katika mikono ya babake katili, alitorokea mjini ambako alijipata akipambana na maisha ya ulitima kama ilivyokuwa kwa

wengi mijini. Hata hivyo hakufa moyo kwani alijaribu bahati yake hapa na pale mwishowe akafanikiwa kufanya biashara iliyomsaidia kupata pesa za kumrudisha shuleni. Mwandishi anaeleza kuwa:

> *Alitafuta kazi, akakodi chumba na pia akajifungulia biashara. Alifaulu kuendelea na masomo yake na alipofaulu vizuri alijiunga na chuo kikuu na akapata digrii ya mwanzo (uk 468*).

Ni kutokana na masomo haya ndipo anapata motisha ya kuwahamasisha na kuwapa elimu vijana wenzake.

Katika harakati hizi za kuwahamasisha wananchi ndiposa anakutana na babake ambaye walikuwa hawajakutana kwa muda mrefu. Walipokutana waliweka kando chuki zao za kipumbavu na hamaki za miaka mingi iliyopita. Matokeo yakawa kumbatio la baba na mwana. Huu ukawa mwanzo mpya, yaani kuyasahau yaliyokuwa yamepita kisha kuanza maisha mapya. Baadaye waliweza kushirikiana katika shughuli za ukombozi. Aidha Mkamandume anaporudi kijijini mwao ili kuendeleza harakati za ukombozi, watu wengi walikuja kumwarifu kuwa walikuwa wamechoka na unyanyasaji uliokuwepo. Miongoni mwao walikuwemo wale waliokuwa adui wake wa zamani. Mfano ni; Mzee Mponda aliyekuwa adui na mgomvi wake wa kudumu. Hii ni ishara kwamba wananchi wako tayari kushikiriana ili kuyaondoa maisha magumu. Jambo hili liliwachochea wanajamii kupigania mapinduzi ya nchi ili waweze kuboresha na kubadilisha maisha yao.

Ngugi wa Thiong'o (1986) katika riwaya ya *Shetani Msalabani* anaonyesha suala la ukombozi wa kielimu kupitia kwa wahusika Wariing'a, na Gatuiria. Wariing'a alijikakamua masomoni. Alikuwa amesoma mpaka kidato cha nne. Akafanya mtihani wa

*school certificate* akajipatia shahada iliyoonyesha kuwa amefaulu katika Kiingereza, Kiswahili na Dini. Tajiri wa Ngorika anakatiza ndoto yake ya masomo kwa kumpachika mimba. Hali hii inachangiwa na umaskini uliokuwa umewazingira. Wazazi wake walikuwa gerezani baada ya kushikwa wakati wa vita vya Mau Mau. Alilazimika kuishi na shangaziye ambaye pia alikumbwa na changamoto ya mapato.

Tajiri alimshawishi kupitia kwa mali nyingi aliyokuwa nayo. Baada ya kupachikwa mimba tajiri alimtema na kujitenga naye, jambo lililomzidishia masaibu maishani. Alilazimika kuacha shule ili kulea ujauzito. Licha ya hali ngumu iliyomkabili hakufa moyo, baada ya kujifungua alirejea shuleni akaendelea na masomo yake. Mwandishi anasema kwamba:

> *Wazazi wake waliamua kumpeleka katika Nairobi Secretarial College akafundishwe kupiga tapureta na hati ya mkato (uk 16).*

Baada ya kumaliza masomo yake, alianza kutafuta ajira. Boss wake wa kwanza alitaka awe mchumba wake ili apewe kazi. Alikataa katakata na akaenda kwa ofisi nyingine kuomba kazi. Wariinga alifahamu haki zake vyema na kwa hivyo alijikomboa mwenyewe kutokana na dhuluma ya kimapenzi inayoendelezwa na matajiri kazini kwa misingi ya kiuchumi. Ingawa amepoteza ajira anafaulu kujitenga na usherati wa boss wake kazini aliye na mazoea ya kuwadhulumu wanawake kimapenzi bila hiari yao.

Gatuiria pia, alitumia elimu yake kupinga dhuluma za babake dhidi ya wafanyakazi wa tabaka la chini. Anamwokoa Wariinga mara mbili akitaka kujitia kitanzi kutokana na majuto aliyopitia. Kupitia kwa mazungumzo kati yake na Wariinga tunafahamu namna mataifa yaliyopata uhuru hivi karibuni yanaendeleza utabaka. Anasema kuwa:

> *Mataifa haya hayawezi kuepukana na taabu kwa sababu yalijifunza namna ya kustawisha uchumi kwa wataalamu wa Amerika.Yakafundishwa kufuata misingi ya ubinafsi. Kila mtu kuishughulikia nafsi yake tu. Mataifa haya yalipewa nasaha yasifuate misingi ya kijamaa. Yalifunzwa kushughulikia pesa! Wimbo wa pesa! pesa! pesa! (uk 12).*

Usemi huu unawachochea wahusika hawa kushirikiana na kupigania haki zao. Wanawazindua wazalendo wengine katika mapinduzi ya jamii yao. Kupitia kwa juhudi zao Mabepari waliokuwa wakimiliki nyenzo za uzalishaji mali waliangamizwa na tabaka nyonyaji likavunjiliwa mbali kabisa.

Kupitia kwa kifo cha Tajiri wa Ngorika mbele ya mwanawe aliyepinga maovu yake, mwandishi anafaulu kuonyesha matumaini kwa kizazi kijacho. Kifo chake kinakuwa mwisho wa dhuluma walizofanyiwa wananchi wa tabaka la chini. Gatuiria anafunga ndoa na Wariinga na kuanzisha kizazi kipya chenye usawa kwa kila mwananchi.

### 4.4 Hitimisho

Sura hii imeangazia mbinu ambazo zilitumiwa na wazalendo wakati wa kupigania ukombozi katika riwaya teule. Imechunguza ukombozi wa kisiasa, kiuchumi na kielimu kwa kuzingatia riwaya za *Mkamandume* na *Shetani Msalabani*. Harakati za mapinduzi kabla ya kupata uhuru na baada ya kupata uhuru zimeangaziwa. Mihimili ya nadharia ya uhakiki wa ki-marx imetumika kufafanua kwa kina ukombozi wa wanajamii.

Katika kupigania mapinduzi wahusika waliodhulumiwa walitumia mbinu mbalimbali kujikomboa kutokana na dhuluma za kitabaka. Wahusika waliodhulumiwa walishirikiana ili kuwazindua wanajamii kujikomboa kabla ya uhuru na hata baada ya uhuru. Pia, walianzisha harakati za kuwahamasisha vijana kupitia kwa fasihi. Fauka ya hayo, wahusika wa tabaka la chini walijikomboa kupitia kwa elimu na kuanzisha biashara ya kujikimu kimaisha.

Ukombozi ulikumbwa na changamoto nyingi zikiwemo; kuawa kwa waandamanaji wakati wa kupigania mapinduzi, unyakuzi wa ardhi na uharibifu wa mali uliowaathiri pakubwa wanajamii. Licha ya matatizo haya wanyonge kama vile; Mkamandume, Wariinga, Wangari na Viwe wanajitolea kufa kupona kutetea haki zao. Wanamapinduzi hawa walipigania usawa wa raslimali, ajira kwa wanajamii, elimu bora, matibabu bora, maendeleo ya miundo misingi na kufuatwa kwa sheria inavyofaa.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii, tumerejelea muhtasari wa yale tuliyoyafanyia utafiti na kuyatathmini kwa kuangazia nadharia ya uhakiki wa ki-Marx. Tumechunguza namna dhuluma za kitabaka zinavyojitokeza na athari zake katika riwaya za *Mkamandume* na *Shetani Msalabani*. Malengo ya utafiti pia yamezingatiwa vilivyo katika utafiti. Mwisho wa sehemu hii tumetoa mapendekezo kwa tafiti za baadaye kulingana na mada yetu.

## 5.2 Muhtasari wa matokeo

Katika utafiti huu, tumeshughulikia riwaya mbili za *Mkamandume* na *Shetani Msalabani*. Utafiti umejikita kwa maswali yafuatayo:

a) Dhuluma za kitabaka zinajitokeza kwa njia gani katika riwaya teule?

b) Dhuluma za kitabaka zina athari gani kwa wahusika wa riwaya teule?

c) Ni mbinu zipi wanazotumia wanyonge kujikomboa na kujiimarisha kimaisha katika riwaya teule?

Utafiti huu umefaulu kujibu maswali ya utafiti kwa kuzingatia malengo yafuatayo:

a) Kuonyesha jinsi dhuluma za kitabaka zinavyobainika katika riwaya teule.

b) Kubainisha athari za dhuluma za kitabaka kwa wahusika wa riwaya teule.

c) Kuchunguza mbinu wanazotumia wanyonge kujikomboa na kujiimarisha kimaisha katika riwaya teule.

a) Lengo la kwanza ni kuonyesha jinsi dhuluma za kitabaka zinavyojitokeza katika riwaya za utafiti. Utafiti wetu umebainisha kuwa wahusika wa tabaka la chini wanadhulumiwa na tabaka nyonyaji linalomiliki nyenzo za uzalishaji na usambazaji wa mali. Tumebainisha kwa kuangazia dhuluma zifuatazo zinazojitokeza katika riwaya teule:

i) Dhuluma dhidi ya wanyonge. Utafiti wetu umeonyesha namna wahusika wanyonge wa tabaka la chini wanavyodhulumiwa. Tumeonyesha changamoto zinazowakumba wahusika wanyonge katika riwaya ya *Mkamandume.* Vilevile, kupitia kwa riwaya ya *Shetani Msalabani,* tumeangazia namna matajiri walio uongozini wanavyoendeleza dhuluma dhidi ya wanyonge kwa kuwa wao ndio wanaomiliki nyenzo za uzalishaji na usambazaji wa mali.

ii)Dhuluma dhidi ya wanawake. Kupitia kwa riwaya ya *Mkamandume*. Tumeonyesha jinsi Viwe anapigwa kikatili na babake kwa sababu ya kuwa mja mzito. Hali hii inaonyesha ukatili kwa mwanamke kwa kuwa jamii haikumchukulia hatua yeyote Mkamandume kwa kuvunja sheria. Pia tumemwangazia Wariinga katika riwaya ya *Shetani Msalabani*. Anadhulumiwa na tajiri katili akiwa bado mwanafunzi wa shule ya upili.

iii) Kubaguliwa kwa misingi ya rangi. Utafiti wetu umeangazia utengano uliokuwepo kati ya wakoloni na waafrika wakati wa ukoloni. Kabla ya kujipatia uhuru waafrika walitengwa na wazungu kwa misingi ya kiuchumi. Wananyakua mashamba yenye rutuba ya waafrika kisha wanawaajiri Waafrika kuwa wafanyakazi wa kuzalisha mali zaidi kwa manufaa yao.

iv) Wahusika katika riwaya teule walidhulumiwa kisaikolojia. Katika riwaya ya *Mkamandume*, Soud anaathirika kisaikolojia baada ya posa yake ya kumchumbia Time

kukataliwa na babake. Kwa upande mwingine, Wariinga anakuwa na mawazo mengi alipopachikwa mimba na kutemwa na tajiri katili. Anajaribu kujiua lakini anashindwa.

v) Dhuluma dhidi ya wafungwa na wananchi wasiokuwa na hatia. Katika riwaya ya *Shetani Msalabani,* Wangari anashikwa na kutiwa kizuizini bila hatia yeyote. Alilala katika kituo cha polisi kwa siku tatu katika kitundu mlimokuwa na kinyesi na mkojo. Katika riwaya ya *Mkamandume,* Mzee Mkasi alidhulumiwa wakati wa vita vya ukombozi katika nchi ya Malelejimema. Alishikwa na kuwekwa kizuizini bila hatia yoyote.

b) Kwa kuzingatia lengo la pili, tumebainisha athari za dhuluma za kitabaka kwa wahusika wa riwaya teule. Utafiti umezingatia nadharia ya uhakiki wa ki-Marx ambayo inaeleza kuwa historia ya maisha ya binadamu inaweza kuelezeka katika misingi yakinifu ya kiuchumi ambayo huchunguza njia kuu za uzalishaji na usambazaji mali. Kutokana na sababu za kiuchumi, hutokea matabaka ambapo tabaka moja humiliki nyenzo zote za uzalishaji mali na hivyo kulifanya kuwa na nguvu zaidi na uwezo mwingi kiuchumi. Kwa upande mwingine, tabaka la chini ndilo la wengi wasiomiliki chochote ila jasho lao na nguvu zao ambazo hutumika kuzalisha mali zaidi kwa manufaa ya wanyonyaji. Utafiti wetu umebainisha athari zifuatazo katika riwaya teule:

i) Ukosefu wa mahitaji ya kimsingi. Tumebainisha namna wahusika wanyonge wanavyotatizika kwa kukosa mahitaji ya kimsingi. Katika riwaya ya *Shetani Msalabani* Wariinga anakosa makazi na mahitaji ya kimsingi baada ya wazazi wake kutiwa gerezani wakati wa vita vya Mau Mau. Mkamandume pia aliishi maisha ya ufukara kutokana na kutengwa hasa baada ya kupigania ukombozi wa nchi ya Malelejimema.

ii) Dhuluma za kitabaka zilisababisha ukosefu wa ajira miongoni mwa wanyonge katika riwaya za utafiti. Marx anasisitiza kuwa tabaka la juu ndilo humiliki nguvu za kiuchumi hali ambayo huchangia kuwepo kwa utengano baina ya tabaka hili nyonyaji na tabaka la chini. Wangari na Wariinga wanatatizika kupata ajira jijini kwa sababu walitoka katika tabaka la chini lisilomiliki nguvu za kiuchumi. Kwa upande mwingine Soud ambaye ni msomi aliyesomea masuala ya sheria anakosa ajira kwa muda mrefu zaidi.

iii) Kuuawa kwa wanyonge kunajitokeza katika riwaya za *Mkamandume* na *Shetani Msalabani.* Utafiti wetu umeangazia namna wazungu waliwaua Waafrika wanyonge bila kuwajali wakati wa ukoloni. Katika riwaya ya *Shetani Msalabani* mwandishi anadai kuwa Mwaura alitumiwa na Wazungu kuwaangamiza Waafrika bila kujali. Said Mohamed pia anaangazia vifo vya wanyonge vinavyojitokeza riwayani.

iv) Athari nyingine ni kutengwa kwa wanyonge kwa misingi ya kiuchumi. Tumebainisha kuwa tabaka la juu liliishi maisha ya kifahari katika mandhari nzuri tofauti na wanyonge wa tabaka la chini walioishi katika mazingira duni. Katika riwaya ya *Shetani Msalabani* kuna utengano baina ya mazingira ya Milima ya Dhahabu na mtaa duni wa Jerusa. Vilevile, katika riwaya ya *Mkamandume* utengano kwa misingi ya kiuchumi ulishuhudiwa kazini. Wafanyakazi wa kiwango cha chini walilazimika kufika kazini mapema na kufanyishwa kazi nyingi kwa masaa marefu ilhali walilipwa mishahara duni. Kinyume na wenzao wa tabaka la juu walifika kazini kuchelewa na kuketi tu afisini lakini walilipwa pesa nyingi kuliko wenzao.

v) Majuto yanajitokeza miongoni mwa wahusika kutokana na matendo maovu waliyoyatendea wenzao. Mkamandume alijutia kitendo chake cha kufyeka mazao yote shambani kutokana na hasira aliyokuwa nayo. Katika riwaya ya *Shetani Msalabani*

Wariinga ana majuto chungu nzima baada ya kupachikwa mimba na kutemwa. Pia anapoachishwa kazi na Boss wake na baadaye kufurushwa anakoishi anakumbwa na mawazo.

vi) Athari ya mwisho ni utengano wa kifamilia. Utafiti umebaini kwamba dhuluma zilisababisha utengano wa kifamilia katika riwaya teule. Mkamandume anatengana na bintiye Viwe kwa muda mrefu. Kwa upande mwingine, Gatuiria anatengana na babake kutokana na dhuluma za babake dhidi ya wafanyakazi wake. Wariinga pia anatengana na wazazi wanapotiwa gerezani wakati wa vita vya mapinduzi.

c) Lengo la mwisho lilikuwa kuchunguza mbinu wanazotumia wanyonge kujikomboa na kujiimarisha kimaisha katika riwaya teule. Nadharia ya ki-Marx inadai kuwa historia ya jamii ni historia ya mapambano baina ya matabaka. Marx anasisitiza kuwa matabaka huchangia mapinduzi kwani huzua mikinzano na migogoro kuhusu mfumo dhalimu wa ubepari. Kutokana na haya mageuzi ya kiuchumi na kisiasa hutokea. Kwa hivyo kudhulumiwa kwa tabaka la chini kwa muda huchochea wanyonge kuungana na kupigania ukombozi wao. Utafiti wetu umechunguza mbinu zilizotumiwa na wanyonge kujikomboa kisiasa, kiuchumi na kielimu.

i) Ushirikiano wa wanyonge kupigania ukombozi. Kwa kurejelea riwaya teule tumeangazia ushirikiano kama mojawapo ya mbinu waliyotumia wanyonge kujikomboa kutokana na dhuluma za kitabaka zinazowakumba. Ushirikiano huu unatumika wakati wa ukoloni na baada ya wakoloni kuondolewa mamlakani na wenyeji. Wananchi walichochewa kupigania mapinduzi kutokana na umaskini, ufisadi, ukabila, ukosefu wa ajira na kudhulumiwa kwa wafanyakazi kila mara kazini.

ii) Makala ya kuwazindua wanyonge**.** Katika riwaya ya *Mkamandume*, tunamwona Nadia akishirikiana na Soud kuandika makala mbalimbali yaliyolenga kuufunua ukandamizaji uliopo Malelejimema. Makala hayo yalichapishwa katika vyombo vya habari vya nje kwa kuwa vyombo vya habari vya ndani havingeruhusu kuchapishwa kwa habari hizo nchini ili wananchi wasifahamu ukweli wa mambo. Wanamalelejimema walipata fursa ya kujionea namna walivyodhulumiwa na tabaka nyonyaji lililokuwa uongozini. Maovu yote yalifichuliwa, hali iliyowazindua wananchi kupigania ukombozi wao.

iii) Maandamano ya wanyonge. Tumechunguza namna wahusika wa riwaya teule walivyoandamana kwa nia ya kutetea haki zao. Katika riwaya ya *Shetani Msalabani* wahusika wa tabaka la chini wanaandamana ili kupigania mapinduzi ya jamii yao. Wazalendo wa Ilmorog wakiongozwa na Muturi, Gatuiria, Wariinga na Wangari wanaungana dhidi ya mabepari wanaoshindana kuwanyonya maskini wa tabaka la chini. Kupitia kwa maandamano, baadhi ya mabepari wanaangamizwa na wengine wanatiwa gerezani na kushtakiwa. Hali hii inasaidia kuvunjiliwa mbali kwa mifumo dhalimu ya uzalishaji na usambazaji mali uliokuwa ukiwafaidi matajiri pekee ilhali wachochole wa tabaka la chini waliendelea kuteseka na kuishi maisha duni ya kifukara.

iv) Kuelimika kwa wahusika wanyonge. Tumechunguza namna elimu miongoni mwa wahusika wanyonge inavyowazindua kujikomboa. Katika riwaya ya *Mkamandume* mhusika Viwe, aliamua kurudi shuleni ili kujiendeleza kimasomo baada ya utengano wa kifamilia na babake.

v) Matumizi ya fasihi. Baadhi ya wahusika wakuu kama vile, Soud na Viwe walianzisha harakati za kuwahamasisha vijana kwa kutumia fasihi. Harakati hizi ziliendelezwa na pesa zilizokuwa zikitoka kwa wadhamini na wahisani wema kama Nadia, Mzee Sleyyum, Soud,

Viwe na pesa zilizokusanywa kutokana na maonyesho ya michezo. Michezo hii iliweza kuwafungua watu wengi macho kwani ndani yake kulikuwa na historia katika ukweli wa maneno ya wahusika kuliko vile maisha yalikuwa yamezoeleka.

Katika kuchunguza suala la mapinduzi utafiti umejikita kwa nadharia ya ki-Marx ambayo inaeleza kuwa njia ya kusaidia na labda kuharakisha kuangamizwa kwa mfumo wa kibepari ni kudadisi, kukosoa, kushutumu, kulaumu na kufichua dhuluma zilizopo katika itikadi za tabaka la juu zinazoimarisha ubepari. Mhimili huu umetuelekeza kuonyesha mbinu wanazotumia wanyonge kujikomboa na kujiimarisha kiuchumi katika riwaya teule. Tumebainisha maandamano, kuelimika kwa wanyonge, makala, vitabu vya fasihi, kuanzisha biashara na kuungana kwa wanyonge kama mbinu za kujikomboa.

### 5.3 Mchango wa utafiti

Utafiti huu umedhihirisha kwamba wahusika wa tabaka la chini wamedhulumiwa na tabaka nyonyaji linalomiliki nyenzo za uzalishaji na usambazaji wa mali. Aidha, utafiti huu umechangia kubainisha namna wahusika wanyonge wanavyoshirikiana kupigania ukombozi wao kutokana na dhuluma za kitabaka.

### 5.4 Mapendekezo

Tumechunguza dhuluma za kitabaka katika riwaya za *Mkamandume* na *Shetani Msalabani*. Riwaya hizi zilifaa kwa kuwa zimeangazia nchi ya Kenya na Visiwa vya Zanzibar na Pemba zilizoshuhudia dhuluma za kitabaka. Utafiti wetu umedhihirisha kuwa wanajamii wa tabaka la chini wanakumbwa na dhuluma kutoka kwa tabaka nyonyaji linalomiliki nyenzo za uzalishaji na usambazaji mali. Hata hivyo bado tafiti zingine zinaweza kufanywa kuhusu mambo yafuatayo:

1. Tafiti nyingine zifanywe kwa kutumia nadharia nyingine za kutafiti kuhusu aina zingine za dhuluma kama vile dhuluma dhidi ya walemavu katika tanzu zingine za fasihi kwa mfano; Hadithi fupi, ushairi au fasihi simulizi.
2. Pia, utafiti ufanywe kuhusu changamoto wanazokumbana nazo wanamapinduzi wakati wa kupigania ukombozi dhidi ya dhuluma za kitabaka katika fasihi andishi.
3. Vilevile, utafiti wa nyanjani unaweza kufanywa kuhusu dhuluma za kitabaka ili kubaini ukweli wa yale yanayoandikwa na waandishi katika kazi za fasihi.

## MAREJELEO


Bakhress, S. K. (2010). *Kamusi ya maana na matumizi*. Nairobi: Oxford U.P.E.A. Ltd.

BAKITA (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Eagleton, T. (2011). *Why Marx was Right*. New Haven: Yale University Press.

Gecaga, M. (1996). *Rape as a tool of Violence Against Women*. Nairobi: Act Publishers.

General Assembly Ressolution, (1996). *International Covenant on Civil and Political Rights*. Paris: United Nations Human Rights.

Gitau E. N. (2005). '*Unyanyasaji Dhidi ya Wanaume katika Fasihi Andishi ya Kiswahili'*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Gray, J. (1962). *The History of Zanzibar from the Middle Ages to 1856*. London: Oxford University Press.

Jabir, M. H. (1997*). '*The Plantation Economy During the Protectorate Period in Zanzibar' *(1890-1964).* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa).

Johnston, T. (2002). Violence and Abuse of Women and Girls in Kenya, Population Communication Africa. Nairobi: New World Printers.

Kahara, (2011). 'Tamthilia kama Utendi: Uchanganuzi Linganishi wa Tamthilia za Kinjeketile na Mzalendo Kimathi,' Chuo kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Kamunde, M. E (1983). 'Kilio cha Wanyonge katika Riwaya za Said Mohamed.'Tasnifu ya uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Karanja P. N. (1990). 'Tamthilia za Kikombozi, Taswira ya Mwafrika katika Vita vya Ukombozi Dhidi ya Ukoloni'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Kavuria, P. (2008). 'Dhuluma za Watoto Katika Riwaya za Kiswahili.*'* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Kenya Gazette Supplement No 95, (2002). *The Children Act, 2001*. Nairobi: Government Printer.

Kimani, C.W. (2003). 'Swala la Dhuluma Dhidi ya Wanawake katika Fasihi ya Kiswahili'. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Kimeu, N. A. (2016). 'Maudhui ya Ukombozi katika Wimbo Mpya na Msururu wa Usaliti'. Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Kipyegon, E. K. (2013). 'Nafasi na Utambulisho wa Mwanamke katika Natala na Kifo Kisimani'. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Kipyegon, H. (2017). 'lnfluence of parenting to Child Education.' Imepakuliwa: https://www.kenyaplex.com>resource, 30/06/2019.

Kristian, D. (2006). Slavery and Apatheid by Anotherr Name. Cape Town: Iziko Slave Lodge Museum.

Longhorn Kenya. (2011). *Kamusi ya Karne 21*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Lunacharsky, A. (1973). *Literature and Art (2nd Edition).* Moscow: Progress Publishers.

Lynch, M. A. and Robert, J. (1982). *Consequences of Child Abuse*. London: Academic Press Ltd.

Mandel, E. (1968). *Marxist Economic Theory*. London: Merlin Press.

Marx K. (1959). *Marx and Engels on Literature*. New York: lnternational General.

Mayieka, M. (2015). 'Masuala Ibuka katika Riwaya za Kisasa: Kidagaa Kimemwozea na Mhanga Nafsi Yangu.'Tasnifu ya Uzamili. Chuo kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Miliband, R. (1976). *Marxism and Politics*. London: Oxford University Press.

Mohamed, S.A. (2014*). Mkamandume*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mugambi, E. K. (1983). 'Kilio cha Wanyonge katika riwaya za Said Mohammed.'Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mutegi, N. (2014) ‘*Ajira ya Watoto ltawaathiri*: Taifa Leo, Machi 18, uk 11.

Ndungo, C.M. (1985). ‘Wanawake na mabadiliko ya kihistoria’ Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Ng’etich, B. (2011). ‘Dini kama Chombo cha Kuwadhulumu Waumini.’Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Ngara, E. (1985). *Stylistics Criticism of the African Novel.* London: Heimann.

Ngugi wa Thiong’o (1982). *Shetani Msalabani*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Njogu, K. (1987). ‘Maudhui ya Mapinduzi katika Riwaya za Visiwani Zanzibar.’ Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Osango, D. S. (2015). ‘Ukombozi wa Kisiasa na Kiuchumi katika Mkamandume’. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Republic of Kenya. (2010). *Katiba ya Jamhuri ya Kenya.* Nairobi: lnternational Institute of Legislative Affairs.

Sarara, M. M. (1997). ‘Maudhui Katika Tamthilia za S.A Mohamed.’ Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Nairobi. (Haijachapishwa).

Scott, G. (2020). ‘Migogoro ya Kisaikolojia katika Riwaya za Mkamandume na Unaitwa Nani? ‘Chuo kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Sengo, T. S. Y. (1973). *Dhima ya Fasihi kwa Maendeleo ya Jamii katika Kiswahili Juzuu* 43/2 Dar es Salaam: TUKI.

Shirika la AFP (2014). ‘*Wamtetea Mfungwa.*’ Taifa Leo, Juni 20, uk 13.

Suakei, A. (2013). ‘Usasa wa Mwanamke wa Kisasa Katika Nyuso za Mwanamke’. Tasnifu ya uzamili. Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Dar es Salaam: O.U.P East Africa Limited.

United Nation Assembly, (1948). *Universal Declaration of Human Rights*. Paris: General United Nations.

Wafula, R.M. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia, Historia na Maendeleo Yake.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wafula, R.M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2006*). Uhakiki wa Fasihi. Misingi ya Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wiliams, R. (1977). *Marxism and Literature*. London: Oxford University Press.

## KIAMBATISHO 1

### KALENDA YA KAZI

| | |
|---|---|
| Aprili- Juni 2017 | Kutafuta mada ya utafiti na kuandika Makala dhanishi. |
| Septemba-Disemba 2017 | Kuandika rasimu ya kwanza ya pendekezo la utafiti. |
| Aprili- Juni 2018 | Kuandika rasimu ya pili ya pendekezo la utafiti. |
| Septemba- Novemba 2018 | Kuandika rasimu ya mwisho ya pendekezo la utafiti. |
| Februari 2019 | Kutetea pendekezo la utafiti idarani. |
| Aprili 2019 | Kufanya marekebisho yaliyopendekezwa wakati wa utetezi. |
| Juni 2019-Disemba 2020 | Kuandika sura za pili, tatu, nne na tano za tasnifu. |
| Aprili 2021 | Kuwasilisha matokea ya utafiti kwa wasimamizi. |
| Septemba 2021 | Kufanyia marekebisho tasnifu. |
| Oktoba 2021 | Kuwasilisha rasimu ya pili kwa wasimamizi. |
| Novemba 2021 | Kuwasilisha rasimu ya mwisho. |
| Disemba 2021 | Kufuzu. |

## KIAMBATISHO 2

GHARAMA YA UTAFITI

| | |
|---|---|
| UCHAPISHAJI WA TASNIFU | 60,000 |
| GHARAMA ZA HUDUMA ZA MTANDAO | 30,000 |
| VITABU NA MAJARIDA | 30,000 |
| USAFIRI | 30,000 |
| GHARAMA ZA ZIADA | 20,000 |
| JUMLA | 170,000 |